

GPA 2004 PARTICIPANTS

Wanafunzi, Waalimu wa TCDC, na Mwalimu Moshi



Waandishi

1. **Natasha Appenheimer**
2. **Erin Ensley**
3. **Charles Elfer**
4. **Lynsey Farrell**
5. **Krisin Leefers**
6. **Anna Lewandowski**
7. **John Linsley**
8. **Shannon Montgomery**
9. **Rebecca Roeder**
10. **Rebecca Skiba**
11. **Sarah Smiley**
12. **Noelle Sullivan**
13. **Joanna Tague**
14. **Eugenia Williams**

YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA: RIPOTI ZA SAFARI YA PWANI (Trip report)

Anna Lewandowski	4
Erin Ensley	6
Rebecca Skiba	9
Eugenia Williams	10
John Linsley	11
Joanna Tague	12
Noelle Sullivan	14
Rebecca Roeder	16
Kristin Leefers	18
Lynsey Farrell	19
Natasha Appenheimer	21
Sarah Smiley	23
Shanon Montgomery	25

SEHEMU YA PILI: RIPOTI ZA VITABU

Anna Lewandowski: <i>Barua Ndefu</i>	28
Erin Ensley: <i>Bwana Shaaba Banila</i>	29
Joanna Tague: <i>Zimwi la Leo</i>	30
Rebecca Skiba: <i>Hadithi yangu</i>	32
John Linsley: <i>Kibuyu cha Ajabu</i>	34
Natasha Appenheimer: <i>Urithi wa Mtoto wa Fisi</i>	35
Noelle Sullivan: <i>Zimwi la leo</i>	37
Eugenia Williams: <i>Jitu Kali</i>	39
Lynsey Farrell: <i>Rosa Mistika</i>	40
Charles Elfer: <i>Debe la Dhahabu</i>	42
Rebecca Roeder: <i>Laba Msichana Shujaa</i>	43
Sarah Smiley: <i>Hawala ya Fedha</i>	45

Lynsey Farrell: <i>Shamba la Wanyama</i>	45
Kristin Leefers: <i>Mtoto wa Mianzi</i>	47
Shannon Montgomery	49

SEHEMU YA TATU: RIPOTI YA MRADI WA MWISHO

Charles Elfer: <i>Namna ya Kutambua Takataka; Maoni ya Jamii</i>	52
Joanna Tague: <i>Baada ya Miaka Arobaini; Maoni ya Ujamaa</i>	55
Sarah Smiley: <i>Elimu katika Tanzania</i>	57
Anna Lewandowski: <i>Kiswahili Kama Somo na Mada Katika</i> <i>Kiwango cha Chuo Kikuu</i>	60
Rebecca Roeder: <i>Lugha Katika Tanzania</i>	63
Natasha Appenheimer: <i>Ukimwi Tanzania</i>	64
Shannon Montgomery: Mashirika yasiyo ya kiserikali ya wanawake na WODSTA	67
Lynsey Farrell: Utamaduni wa vijana katika Afrika Mashariki	70
Noelle Sullivan: <i>Kikundi cha Maendeleo ya Wanawake</i>	72
Eugenia Williams: <i>Watu wa Mahitaji Maalum</i>	75
Rebecca Skiba: <i>Mbuga za Wanyama na Utalii</i>	76

1. RIPOTI YA SAFARI YA PWANI

Anna Lewandowski

Safari ya kwenda pwani ilinivutia sana. Kuna tofauti kubwa ya utamaduni hapa Arusha ukilinganisha na Dar es Salaam au Zanzibar. Tofauti moja niliyoiona ilikuwa dini. Hapa Arusha nimeona watu wengi ni wakristo. Wengi huenda kanisani Jumapili na kumwomba Mungu. Kule Dar na Zanzibar kulikuwa na mchanganyiko wa wakristo na waislamu. Niliona misikiti mingi na kusikia mwito wa sala kila mara. Watu wengi walivaa nguo za kiislamu ambazo ni kanzu na skafu ya kichwani. Tulipokuwa tukizunguka kwa basi, niliona maduka mengi yaliyouza nyama iliyohalalishwa kwa sababu kuna waislamu wengi. Mazingira yalibadilika sana. Hali ya hewa ilikuwa joto ingawaje kulikuwa na miti na mimea ya aina mbalimbali. Kwa mfano, niliona minazi mingi pamoja na maua mazuri. Mazingira yalikuwa ni ya kijani kuliko Arusha, na kulikuwa na unyevu hewani kutokana na maji ya bahari.

Nilishangaa kuona kwamba mjini Dar watu wachache tu walinisumbua kwa kuwa mimi ni mzungu. Sikuwaona watalii wengi mjini, lakini sikupata nafasi kubwa ya kutembelea maeneo mengi. Jioni moja nilipokwenda kutembelea hoteli iliyoitwa “Mango Garden” nikiwa pamoja na rafiki yangu Sarah, tulikuwa na wasi wasi kwani tulifikiri kuwa watu wengi wapitao mtaani wangelitusumbua, lakini watu wote walisikiliza muziki tu! Ilikuwa somo zuri la kujifunza mila halisi au utamaduni wa Tanzania kwa sababu tulikuwa tumejiandaa kukutana na rafiki yangu James, lakini alichelewa kufika, kwa hiyo tuliondoka kabla hajafika.

Kwangu, kutembelea chuo kikuu cha Dar es Salaam ilikuwa jambo safi sana. Mahali hapa palikuwa pazuri sana. Nilishangaa kuona majengo mapya (yalivyoonekana), miti, na pia mimea mingi. Nilifurahi kujifunza kwamba wanafunzi wanaweza kusoma fasihi kwa Kiswahili. Niliona maktaba na kununua vitabu vingi. Bahati mbaya katika maktaba hii hawakukuwa na riwaya za kiafrika zilizoandikwa kwa lugha ya kiingereza au lugha nyingine- kwa mfano “African Writers Series”. Naamini ni muhimu kupata vitabu kutoka katika bara lote la Afrika. Ningependa kujua kama wanafunzi wanaweza kusoma fasihi kwa ujumla na kama wanaweza, kuna darasa lo lote linalotumia riwaya nyingine? Ningelipenda kupata nafasi zaidi ya kuongea na Profesa Senkoro juu ya kitabu chake Tuseme Kiswahili na juu ya masomo ya Kiswahili chuoni na hasa nchini Marekani.

Pia, tulitembelea Bagamoyo na kuona magofu ya Kaole na kanisa muhimu. Hapa pia tuligundua kwamba zamani kulikuwa na waislamu katika sehemu hii kwa sababu tuliona magofu ya misikiti. Tuliambiwa kwamba magofu yale yalikuwepo tangu karne ya kumi na nne au hata mapema zaidi. Inaonekana waislamu walikuja Bagamoyo zamani sana. Bagamoyo ni mji wa

zamani zamani unaohusishwa na biashara ya utumwa. Kwa sababu Bagamoyo iko baharani na pia karibu na bandari, ilikuwa rahisi kuwapeleka watumwa nchi za nje. Livingstone alikwenda Bagamoyo akiwa na nia ya kukomesha biashara ya utumwa, na ndiyo maana leo hii kunaonekana magofu ya makanisa ya zamani. Kanisa la kwanza la Afika ya Mashariki lipo sehemu hii na tuliliona pia. Tuliingia katika kanisa moja na kuona michoro ya watumwa. Michoro hii ilionyesha watumwa wakifanya kazi ngumu. Ningependa kurudi Bagamoyo ili nione na kujifunza historia zaidi.

Nafasi nzuri ya kuzungumza Kiswahili ilikuwa katika soko la wachonga vinyago. Nilijaribu kuongea na kila mwuzaji niliyekutana naye. Kwangu ilikuwa ni rahisi zaidi kuzungumza na kuomba kupunguziwa bei nilipokutana na wanaume kuliko nilipokutana wanawake. Wengi niliozungumza nao hawajasoma kufikia kiwango cha chuo kikuu. Labda wanawake walitishika kwa kuwa walisikia mimi ni mwanafunziwa chuo kikuu. Nilizungumza na wanawake wachache, lakini kama mwanamume akifika kusikiliza juu ya kiswahili changu, wanawake waliniacha kabisa na kumpa mwanamume nafasi ya kuongea nami. Mara kadhaa nilipoingia dukani, nilianza na habari za kazi, n.k. Halafu, nilizungumzia juu ya masomo ya kiswahili tuliyopata katika kituo cha TCDC. Sikununua kitu chochote kwa haraka. Niliingia maduka mengi na kuuliza bei. Baada ya kuangalia kwa muda mrefu, niliamua kurudi katika maduka niliyotembelea awali ili ninunue vitu vichache. Ninaamini kwamba labda watu hawa waliitaka biashara yangu zaidi ya watu wanaotoka Arusha. Nilimwuliza mtu mmoja kama ana kitu fulani, aliniambia hana, lakini anaweza kuwauliza watu wengine. Nilitaka kununua mti wa mbuyu na mtu huyu alitafuta na kujaribu kuupata. Nadhani hapa Arusha kuna watalii wengi zaidi na ni rahisi zaidi kuuza vitu kwa bei nzuri. Labda kule Dar, kuna watalii wachache tu na kila mwuzaji anahitaji kuwahudumia wateja ili wapate pesa.

Nilifurahi sana kuona mradi wa wanawake kuhusu mwani. Sikujua kwamba inawezekana kulima mwani kwa haraka kama nilivyoona. Baada ya wiki tatu mwani unakuwa tayari umeshakomaa. Nilimwuliza mwalimu juu ya mashamba ya mwani, kwani sikuweza kutambua ni vipi wanawake wanaweza kutambua shamba hili au lile ni la nani. Mwalimu aliniambia kwamba wanawake wote wanajua kwa sababu wanalima wenyewe na ni mazingira yao, ingawaje bado kuna matatizo. Kama kuna mvua, upepo utaharibu mwani kwa sababu utajitenga. Mara nyingi, wanawake wanapata mwani huu na kushindana juu ya umilikaji. Nilifurahi pia kuongea kidogo na James anayetoka Bwejuu. Anafanya kazi Mji Mkongwe wakati wa msimu wa utalii, lakini anarudi nyumbani kwake kila wikendi ili amsaidie mamake na familia yake.

Kweli niliifurahia sana safari yetu, na ningependa kurudi Dar na Zanzibar tena. Watu walikuwa wazuri sana, majengo yalinivutia na nilifurahi kuona sehemu muhimu katika historia ya Afrika ya Mashariki.



Ana na Shannon Sokoni

2. Erin Ensley UCLA

Tukio letu lilianza alfajiri ya Jumamosi mbele ya ofisi ya mapokezi. Sisi wote tulikuwa tuingojea madereva wetu, ambao hawakukumbuka kutegeshea saa ya kuwaamsha. Hatimaye walifika, na tukapanda mabasi mawili bila kusubiri na kuondoka.

Baada ya safari ya takribani masaa tisa hivi, tulifika mjini Dar-es-Salaam. Hoteli yetu (iliyoitwa Courtyard) ilikuwa nzuri, na tulipoingia mlangoni kila mmoja alipewa glasi ya maji ya matunda. Haraka haraka tuliweka mizigo katika vyumba vyetu ili turudi ndani ya basi letu ili kuzunguka kidogo mjini kabla ya chakula cha jioni. Kwa bahati nzuri, tulipata nafasi ya kuogelea tuliporudi hotelini, na halafu tulielekea sehemu ya maakuli kula chakula ambacho kilikuwa kizuri

sana (crème brulee...). Kwa kuwa safari yetu ilikuwa ya kuchosha sana, nililala mapema baada ya kutazama idhaa ya BBC kwa muda mfupi.

Siku iliyofuata, Jumapili, tulikwenda mji mkuu wa zamani (siku za ukoloni) wa Tanzania, yaani Bagamoyo. Wakati wa kusafiri, Mwalimu Rehema alinieleza maana ya majina mengi ya maeneo mbalimbali. Kwa mfano, mji wa Bagamoyo ni muungano wa kitenzi cha kubwaga na jina la moyo (maana yake inawakilisha historia ya ubwana na utumwa).

Mjini Bagamoyo tulitembelea kwanza magofu ya majengo matatu: msikiti, nyumba waliyolala watu, na makaburi. Majengo yote haya yalijengwa karne ya kumi na mbili, na usanifu wake ulinivutia sana kwani niliweza kuona picha za ukumbusho ukutani. Nilipatwa na hofu kuona bomba la sindano karibu na pwani, lililokuwa miongoni mwa takataka nyingi sana.

Kisha tulitembelea kanisa la kwanza la Afrika ya Masharika; kanisa ambalo lilitumiwa na watumwa wa kwanza kupata uhuru. Karibu na kanisa hili tuliona nyumba ya David Livingstone, mmisionari wa Uingereza aliyehusika kukomesha biashara ya watumwa.

Tulikata shauri kurudi Dar ili tukapate chakula cha mchana, na baadaye kuweza kupata nafasi ya kutembelea gulio la mji ule. Katika gulio hili tuliendelea kuona makumbusho yaliyoelezea historia ya Tanzania. Sehemu hii ilionyesha nyumba za asili zinatoka kote nchini Tanzania. Wakati nikiwasubiri watu wote watoke katika jumba hili la makumbusho, nilisikiliza pati ya jikoni na nilisikia bila kukusudia mazungumzo ya walimu wakizungumza jinsi utamaduni wa Tanzania unavyobadilika. Ilikuwa karibu tumpoteze mwanafunzi mwenzetu Rebecca mdogo; yeye alifukuzwa na mwuzaji king'ang'anizi aliyetaka kumwuzia bidhaa kwa nguvu.

Jumatatu tulikutana na mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, aliyetueleza historia ya chuo hiki. John alikuwa akiumwa, hivyo alipelekwa kwa daktari kupata matibabu, na alirejea tulipokuwa tukienda bandarini kupanda meli ya kutupeleka kutembelea kisiwa cha Zanzibar. Usiku ule tulikula katika mgahawa mmoja ulioitwa Mercury's, na halafu tulisherehekea sikukuu ya kuzaliwa ya Charles. Nilipewa jukumu la kugawa keki zilizobaki jambo lililonisaidia kupata marafiki wengi. Wakati tulipokuwa tukirudi hotelini Rebecca mkubwa aliibiwa mfuko wake. Bila kufikiri, nilijaribu kumfukuza mwizi yule, lakini sikufaulu kumwona. Sisi sote tulikwenda kituo cha polisi ili Rebecca akatoe ripoti na maelezo yake huko. Baada ya usiku ule mrefu, tulilala fofofo.

Siku iliyofuata, tulianza kwa kuchelewa, kwa sababu Rebecca aliyeibiwa mfuko wake ilimlazimu kupigia simu kuiarifu benki yake kuhusu mkasa uliompata; kwani kadi yake ya kukopa ilikuwa ndani yamfuko ulioibiwa. Hata hivyo tulipata muda mwingi wa kutembea na kuangalia Mji Mkongwe. Tulitembelea kanisa katoliki ambapo maiti ya David Livingstone iliwekwa kwa muda mfupi, na pia tukaona msalaba uliotengenezwa kwa mti na chini yake moyo

wa mtu ulikuwa umezikwa. Karibu na kanisa hili tuliteremka katika mapango yaliyotumiwa kuwaweka watumwa wakati huo. Jambo hili lilinikumbusha nilipotembelea ngome za utumwa zilizopo pwani ya Ghana, mwaka uliopita. Haikuwa rahisi kwangu kuelewa na kukubali tulipotembelea sehemu iliyofuata; sehemu hii ilikuwa ni nyumba ya sultani fulani aliyekuwa na suria takriban mia moja. Tukio hili lilinikumbusha chumba kimoja cha ngome ya Elmina ambamo watumwa wengi walisongwa roho. Nilipita kwa ujasiri huku nikigusa picha za kucha zilizochorwa ukutani.

Mchana ule tulikwenda kutembelea shamba la viungo. Kiongozi mmoja alitugawia kiasi kidogo cha viungo hivi kama vile: tangawizi, kungumanga, pilipilimanga, karafuu, n.k. na alituelezea hadithi chache za majina ya viungo hivi na matunda yake ('tofaa'). Hatimaye tulimwangualia mtoto mmoja akipanda mnazi kuangusha nazi. Wakati wa kupanda, aliimba kuondoa mawazo ya kufikiria cho chote zaidi urefu wa mnazi ule.

Baada ya kununua viungo shambani, tulielekea pwani kula chakula cha mchana. Wanafunzi wengine walingojea chakula kivulini, lakini nilipatwa na tamaa ya kuogelea baharini kwani maji yalikuwa meupe kabisa na uliweza kujiangalia kama sakafu iliyokuwa inang'aa. Chakula kilikuwa kizuri kilitushibisha vema. Muda uliobaki baadhi yetu tuliutumia kuangalia vitu madukani, na baadhi ya wenzetu walichagua kupumzika. Usiku ule baadhi ya wanafunzi wenzetu waliamua kutafuta aiskrimu, bila mafanikio na hii itakuwa (hadithi ndefu sana...inayohusu vitunguu na tangawizi...).

Jumatano tulitembelea shamba la mwani. Hapa tulijifunza juu ya historia ya namna ya kushughulikia shamba la mwani. Tuliuliza pia kama wakulima wale wanapata faida kiasi gani au wakulima wa sehemu hii ambao wengi wao ni wanaume wanalazimika kulima mazao mengine pia. Tuligundua wanajitahidi sana lakini bei ya mwani imeshuka sana kwa miaka kumi iliyopita mfululizo. Tuliwasikitikia sana wakulima hawa kwani mfuko mmoja mkavu walipata shilingi themanini tu (na kama ujuavyo mfuko mmoja mkavu ni sawa na mifuko sita ambayo haijakauka).

Safari yetu ya mwisho ilikuwa kutembelea hifadhi ya mbega mwekundu. Tulipata nafasi kuwakaribia mbega wengi; na hawakutuogopa kabisa.

Asubuhi iliyofuata tulielekea uwanja wa ndege kuondoka kurudi Arusha, na wakati tulipokuwa hewani niliweza kuangalia kisiwa kizima, mandhari ambayo sitaisahau mpaka mwisho wa maisha yangu.



Siku ya Uhuru wa Amerika: Erin anafundisha watoto michezo

3. MRADI YA PWANI **Rebecca Skiba**

Wiki iliyopita, mimi, walimu, na wanafunzi tulikwenda Dar es Salaam kwa basi. Baada ya saa nane au tisa, tulifika mjini Dar. Tuliangalia masoko, na baadhi wanafunzi walinunua vitu mbalimbali. Vilevile, tulipotembea mjini tuliona mambo ya utalii kwa mfano watu waliozungumza katika lugha ya Kiingereza.

Tulipokuwa Dar es Salaam tulitembelea mji wa Bagamoyo. Bagamoyo ni mahali ambapo palinivutia na tulijifunza vitu vingi kuhusu utumwa. Pia, tulitembelea magofu ya mji wa kwanza Afrika Mashariki yaliyoitwa Kaole. Mahali hapa palikuwa na msikiti, makaburi, kisima cha bahati nzuri, na mahali pa kuomba. Hadithi kuhusu mahali pa kuomba walitambua kwamba kulikuwa na mtu ambaye alikuwa na kitambaa chenye maji. Mtu huyu aliomba mahali hapa na alikitupa kitambaa chake hewani na kilirudi kikavu. Sasa, watu wanapatembelea mahali hapa patakatifu na wanaomba misaada kwa shida zao mbalimbali.

Tuliona kanisa katoliki la kwanza Afrika Mashariki ambalo liliwasaidia watumwa baada ya kupata uhuru wao. Tuliona vyumba vya watumwa walipowekwa na vilikuwa vidogo sana. Tuliona kanisa ambapo mwili wa Bwana Livingston ulipita. Halafu, tulitembelea masoko ya vinyago. Tulinunua vitu vingi na tulifanya mazoezi ya lugha ya Kiswahili. Vilevile tulitembelea chuo kikuu cha Dar es Salaam na duka la vitabu. Tulimwuliza mkuu wa chuo maswali na aliyajibu vizuri.

Jumatatu, tulipokwenda Zanzibar kila mwanafunzi alifurahi kuona pwani na majengo ya Zanzibar. Tulipiga picha nyingi kwenye boti yetu. Tulisafiri katikati ya msitu na tulikuwa karibu sana na mbega wekundu. Tulitembelea mashamba mawili. Shamba la mwani lilinivutia sana. Wakulima wa mwani wanapanda mwani katikati ya vijiti ndani ya bahari kupunguza kasi ya mawimbi na pia kusaidia mwani kuota.

Baadaye, tulijifunza kuhusu viungo kama karafuu, tangawizi, iliki, mdalasini, na kadhalika katika shamba la viungo. Mchana mmoja tuliogelea katika bahari ya Hindi na tulikula samaki wa aina tofauti tofauti. Vilevile, tulitembelea magofu ya kasri ya Kiarabu. Katika kasri kuna vyumba vingi na sultani Barghash alikuwa na suria tisini na tisa. Pia ndani ya kasri kuna vyoo vitano na bwawa la kuogelea. Alhamisi tulirudi TCDC tukiwa na picha na maarifa tele.

4. Eugenia D. Williams Indiana University

Safari yetu ya wanafunzi wa GPA iliaanza asubuhi na mapema siku ya Jumamosi, tarehe kumi na saba. Nimetaja siku na tarehe hii kwa sababu ilikuwa ni siku ya kuzaliwa kwangu. Katika safari yetu tulitembelea Dar es Salaam, Zanzibar, Bagamoyo na sehemu nyingi tofauti. Ninafikiri wanafunzi wote walistaajabia uzuri wa kisiwa cha Unguja. Kisiwa cha Zanzibar kimewapa mawazo kukumbuka miaka mingi iliyopita kwa sababu matokeo ya safari yetu yalikuwa ya kufurahisha na ya ajabu.

Kuna vitendo vingi ambavyo tulifanya wakati wote wa safari hii; kwa mfano, sherehe ya siku ya kuzaliwa kwangu; magari ya abira yalioelekea Dar Es Salaam na Zanzibar, sherehe ya siku ya kuzaliwa ya mwanafunzi mwingine, kutembelea chuo kikuu cha Dar Es Salaam, kijiji cha Bagamoyo, na maelezo yaliotolewa kuhusu mvumbuzi wa Afrika, Dr. Livingstone. Pia kuna habari kuhusu historia ya watumwa iliyoendeshwa katika mji wa Bagamoyo, Kanisa katoliki, Askofu Steers, na shamba la viungo.

Sitaweza kuelezea juu ya kila mahali tulipotembelea hata kama ningekumbuka kila kitu kilichosemwa, kitu ambacho sikumbuki; kwa hivyo, ningependa kuzungumzia vitu vichache tu ambavyo ninakumbuka kuhusiana na matembezi yangu ya kwanza katika mitaa ya mji wa Zanzibar. Kisiwa cha Zanzibar, kama watu wengi wanavyojua, kinaitwa mji mkongwe kwa sababu mji huu ulijengwa na Waarabu. Mji huu una vichocho na mitaa miembamba. Nyumba nyingi za mji huu zina milango yenye madoido. Mtembezi anayeongoza watalii alitambia kwamba watu wa Zanzibar walijenga milango tuliyoiona. Mlango mmoja ulionyesha mtu mwenye mali na kuweka pembeza

tembo! Baadaye tulitembelea sehemu za pwani na tuliona ngome iliyojengwa wakati wa vita baina ya Waarabu, Wareno na Wajerumani; na ndani ya ngome hii kuna mahali pa kununua vitu mbalimbali. Pia, ngome hii ilikuwa na burudani za aina yake. Siku nyingine tulitembelea shamba la viungo kuona viungo tofauti na tulinusa viungo kama vile iliki, majani ya limau, karafuu, vanila, mdalasini, binsari, pilipilimanga na kadhalika.

Siku nyingine tulijifunza jinsi wanawake wanavyolima mwani. Tuligundua kuwa zao hili haliwapi faida kubwa.

Hapa nimejaribu kuonyesha na kuelezea juu ya safari yetu visiwani Zanzibar, na ninaweza kusema kwa ujumla kuwa safari yetu ilikuwa na mipango mizuri na wanafunzi walipata elimu ya hali ya juu.



Eugenia anafundisha juu ya Kwanzaa

5. HABARI ZA SAFARI YA UFUKWE John Linsley

Tarehe kumi na saba, mwezi wa saba, wanafunzi wa GPA 2004 tulisafiri kwenda ufukwe wa nchi ya Tanzania. Asubuhi ya tarehe hii, wanafunzi tuliampa saa kumi alfajiri kwa sababu tulihitaji

kuondoka TCDC saa kumi na moja asubuhi. Tulitumia usafiri wa basi la abiria. Bwana Slim alituendesha na ni dereva wa Zara Safaris Ltd.

Baada ya kufika pwani, wanafunzi walitembelea sehemu nyingi. Kwanza, tulijifunza kuhusu historia ya mji wa Bagamoyo. Mjini Bagamoyo kuna magofu ya Kaole. Zamani, katika karne ya kumi na tatu, kulikuwa na msikiti hapo, lakini sasa Kaole ni magofu tu. Vilevile, Bagamoyo ilikuwa mji muhimu kwa sababu kutoka mwaka elfu moja mia nane themanini na saba mpaka mwaka elfu moja mia nane tisini na moja, mji huu ulikuwa makao makuu ya Afrika Mashariki ya wakati wa utawala wa Kijerumani. Kwa sasa, Bagamoyo ni muhimu kwa utalii nchini Tanzania kwa sababu watalii na wageni wengi wanapenda kutembelea sehemu hii kujifunza historia ya pwani kupitia mji huu. Vilevile, kwa sasa, mafundi wanajenga na kutengenezea majahazi karibu na mji huu. Miaka michache iliyopita, barabara kutoka Dar es Salaam mpaka Bagamoyo ilikuwa mbaya, lakini, kwa kuwa serikali ya Tanzania ilitambua kwamba barabara hii ni muhimu kwa utalii nchini Tanzania iliamua kuijenga upya barabara hii. Kwa kuwa njia imejengwa upya, unaweza kufika Bagamoyo kwa muda saa moja kutoka mjini Dar.

Baada ya kutembelea Bagamoyo, tulisafiri kwenda Unguja kwa siku chache. Tulisafiri kwa boti iendayo kwa kasi kutoka Dar hadi visiwani. Tulitembelea mji wa mawe, na baada ya kutembelea kidogo sehemu hii tulitembelea mahali pengine tukiwa katika vikundi. Kusini mashariki ya kisiwa hiki, wanafunzi tulitembelea mradi wa wanawake kuhusu mwani. Tulijifunza na kugundua kwamba kulima mwani ni kazi kubwa na faida yake ni kidogo sana. Tulipewa taarifa kuwa soko la mwani liko nchini Denmark.

Tulijaribu kula chakula kipya, kwa mfano ngisi, konokono, na pweza, wakati wa chakula cha jioni katika migahawa mbalimbali. Tarehe ishirini na mbili, wanafunzi wote pamoja na walimu wetu tulisafiri kwa ndege hadi uwanja wa ndege wa Kilimanjaro, na tulipokelewa na kupelekwa TCDC na Bwana Slim aliyekuwa dereva wetu. Becky hakurudi nasi Arusha. Wakati wa safari kisiwani, mfuko wa Becky uliibwa na kibaka na alipoteza pasipoti yake pamoja na fedha taslimu kiasi fulani. Becky alienda ubalozi wa Amerika mjini Dar es Salaam peke yake ili kupata pasipoti mpya. Baada ya siku moja Becky alirudi TCDC kuendelea na mafunzo. Licha ya wizi uliotokea, safari ya wanafunzi wa GPA kutembelea Dar na Zanzibar ilikuwa nzuri sana.

6. DAR ES SALAAM, BAGAMOYO, NA UNGUJA **Jo Tague**

Jumamosi, tarehe kumi na saba, mwezi wa saba, tuliamka mapema sana. Tuliondoka kutoka TCDC saa moja asubuhi. Baada ya masaa nane, tuliingia katika mji wa Dar es Salaam. Tulipofika katika hoteli yetu tuliweka mizigo yetu na tuliamua kwenda kutembelea kuona mji wa Dar es Salaam

kwa basi. Muda huu, tuliona sehemu fulani tu katika mji wa Dar es Salaam. Halafu, tulirudi hotelini. Wanafunzi wengi waliogelea, na wengine walienda kujipumzisha. Tulikula chakula cha jioni pamoja. Halafu, tulikwenda kulala mapema.

Siku ya pili, tulikwenda kutembelea mji wa Bagamoyo. Mji huu una historia muhimu sana kwa nchi ya Tanzania. Maana ya mji huu ni mahali ambapo mtu hutupa moyo wake. Tulipofika Bagamoyo, tulikwenda kuona magofu. Jina la magofu haya yaliitwa Kaole. Magofu haya yalikuwa na misikiti na kaburi. Pia, tuliona takataka nyingi sana kutoka baharini. Hili lilikuwa tokeo la kutuonyesha maendeleo. Kisha, tulikwenda kuona kanisa Katoliki na tuliona nyumba ambayo mwili wa Dr. Livingstone ulipita. Baada ya kutembelea Bagamoyo, tulirudi Dar es Salaam kuona soko. Halafu, tulitembelea nyumba ya makumbusho kuona nyumba za kimila. Pale, nyumba ya makumbusho walitonyesha nyumba nyingi sana kutoka makabila tofauti ya Tanzania. Tulijifunza kwamba kuna makabila mengi sana hapa Tanzania. Pia, watu walitumia njia tofauti kujenga nyumba zao. Walitumia vifaa mbalimbali na walijenga nyumba zao kwa usanifu tofauti. Halafu, tulitembelea soko na wanafunzi waliweza kununua vitu mbalimbali na kujadiliana juu ya bei na wauzaji. Wanafunzi walio wengi waliweza kutumia Kiswahili tu kununua zawadi.

Jumatatu, tulikwenda chuo kikuu cha Dar es Salaam. Kabla, wanafunzi walinunua vitabu katika duka la vitabu. Halafu, tuliwaamkia walimu wa chuo hiki na kujifunza juu ya historia ya chuo kikuu cha Dar es Salaam. Chuo kikuu hiki kina wanafunzi elfu kumi na tatu. Baada ya kutoa msaada wa vitabu, tulikwenda kisiwa cha Zanzibar kwa mashua. Tulipofika kisiwani Zanzibar, tulitembea kwa miguu. Hii ilikuwa muhimu sana kwa vile tuliweza kujizoeza na hali ya hewa ya kisiwa hiki. Wanafunzi wengi walikwenda katika masoko kadhaa na kujadiliana juu ya bei ya bidhaa mbalimbali.

Siku iliyofuata, tulitembelea nyumba ya makumbusho ya watumwa katika mji wa Mawe. Pale, tuliona kanisa Katoliki pia. Tulijifunza juu ya nguzo fulani ambazo ziliwekwa katika kanisa hili. Halafu, tuliona msalaba kutoka mti ambao Dr. Livingstone alifika.

Kisha, tulikwenda kuona magofu ya Marahubi. Sultani Barghash alijenga kasri hii katika mwaka elfu moja mia nane themanini. Lakini, moto uliiharibu kasri hii mnamo mwaka elfu moja mia nane tisini na tisa. Sultani Barghash alikuwa na wanawake tisini na tisa. Sultani huyu alikataa kutumia choo kimoja mara mbili. Tulijifunza hadithi mbili juu ya Sultani Barghash. Hadithi ya kwanza ilisimulia kwamba Sultani Barghash aliwaua wanawake wenye mimba. Hadithi ya pili ilisema kwamba kila mwanamke alihitaji kupanda mti wa maembe ili kukaa katika kasri hii. Halafu, tuliona mfereji wa maji katika kasri hii. Tulijifunza juu ya mfumo wa kusafisha choo katika kasri. Watu walitumia bamvua kusafisha choo.

Baadaye, tulitembelea shamba la viungo. Tulijifunza juu ya pilipili, karafuu, iliki, tangawizi, na kadhalika. Tulijifunza juu ya matumizi ya viungo hivi, na tulijifunza juu ya mimea mingi. Baadaye

tuliangalia viungo hivi na, tulikunywa maji ya nazi. Pia, tulipata nafasi ya kununua viungo kwa ajili ya ukumbusho. Kisha, tulikula chakula cha mchana katika pwani ya kijiji tulichotembelea. Wanafunzi walikula samaki kama kambanti. Baada ya chakula tuliogelea katika bahari na kupumzika karibu na pwani. Tulifurahi sana kubadilisha rangi ya ngozi zetu. Tuliporudi mji wa Mawe, wanafunzi wengi walikwenda kununua vitu mbalimbali. Baada ya muda mfupi, tulikwenda kuangalia wacheza ngoma na kula chakula cha jioni katika ukumbi wa Old Fort.

Jumatano, tulikwenda kwa basi kuona shamba la mwani. Jina la kijiji hiki ni Bwejuu. Mwalimu fulani kutoka Bwejuu alitonyesha shamba la mwani. Wanafunzi tulitembea kwa kuzunguka kuona shamba hili. Tulijifunza vitu vingi juu ya mwani. Tuliporudi kijijini, tulikwenda kuangalia mahali ambapo watu wanapima uzito wa mwani. Kila mwanafunzi alishangaa kujifunza juu ya mashamba haya. Halafu, tulitembelea msitu wa Jozani kuangalia nyani. Baadaye, tulikula chakula cha mchana na kisha tulirudi mji wa Mawe kula chakula cha jioni katika hoteli ya Archipelago.

Kwa muda wa ya siku mbili mjini Dar es Salaam na siku tatu katika kisiwa cha Unguja, tulijifunza juu ya magofu, viungo, historia ya watumwa, mwani, na maendeleo. Safari hii ilitufundisha pia kwamba maendeleo yanaleta matatizo mengi. Wanafunzi walijifunza kwamba maendeleo si mabaya na ni muhimu kuwa na maendeleo, lakini kila chenye uzuri hakikosi ubaya wake pia. Kwa kawaida, matokeo ya maendeleo kama hayakuwekewa mipaka ya kutosha yanaweza yakaiharibu jamii.

7. TAARIFA YA PWANI

Noelle Sullivan

Tuliposafiri kwenda pwani ya Tanzania, sikujua tutaona nini. Sikuwa nimefahamu kwamba mtu anaweza kutumia chupa tupu ya fanta kutengeneza basi lililoharibika. Lakini, Slim alilitengeneza basi letu kwa kutumia chupa tu, bila vifaa vingine. Mbali zaidi, baada ya darasa kuhusu maadili na asili ya Tanzania, sikuwa nimetazamia kuona jambo kama hili. Slim alipocheleweshwa kufika TCDC siku ya Ijumaa, na pia alipochelewa siku ya Jumamosi asubuhi sikuwa nimeelewa sababu, lakini wenzangu walinisaidia kuelewa. Mwishowe, tulifika Dar es Salaam.

Pia, nilitazamia kuwa mjini Dar es Salaam na Bagamoyo, ningelijifunza vitu vingi kuhusu historia ya Tanzania na watu wake, lakini, nilijikuta nikijifunza zaidi kuhusu historia ya wazungu. Sikupenda kuona historia ya Wazungu bali nilitaka watu wanifundishe kuhusu historia ya Watanzania. Nimeshasoma vitabu vya historia ya Watanzania, na ninajua kuna historia kuhusu ukoloni ambao hata hivi sasa una athari kubwa nchini Tanzania, lakini sikupata mtu aliyetufundisha mambo yanayohusu maisha ya Watanzania wakati wa ukoloni. Ningelipenda kujua zaidi kuhusu maisha ya watu siku hizo, lakini hakuna aliyeweza kunisimulia barabara. Labda siku moja watalii

watakapofika Tanzania, watajifunza vya kutosha kuhusu maisha ya Watanzania badala ya kutembea kuona mahali wazungu waliojulikana kama Livingstone walipofika au kutembelea. Sauti za Watanzania zipo wapi katika historia ya Bagamoyo au sehemu nyingine ya pwani? Labda historia hiyo inapatikana kwa watalii, siyo kwa Watanzania wanaotaka kuijifunza, kwani sijaiona yeyote anayejishughulisha na historia ambayo ni muhimu sana.

Mjini Unguja niliona vitu vya kupendeza. Niliona maisha ya watu wa sehemu hii. Siku ya kwanza mjini Unguja, nilikuwa na kikundi cha Erin, Amsale, na Nia. Kiongozi wetu alitambulishwa na Mwalimu Moshi, na aliitwa James. James alianza kutuonyesha nyumba za enzi ya ukoloni, kama balozi tatu za Uingereza, lakini tulipenda zaidi kuona Ngome ya Waarabu. James alitutembeza sehemu mbalimbali, na tuliweza kuona watu wanavyoishi. Niliweza kulinganisha hali ya maisha ya watu wa Unguja, kwani ni tofauti na ilivyo kwa watu waishio mjini Arusha au Dar es Salaam, na niligundua kuwa maisha ya watu wa Unguja ni ya kimaskini na magumu zaidi kuliko ya watu waishio bara. Pamoja na umaskini wao wengi wanatabasamu, na wanaonyesha uzuri wao kwa wageni. Madukani, wauzaji wengi walitusaidia kutafuta vitu tulivyotaka, au kuona sehemu tulizokuwa tunatafuta. Sanaa za Unguja ni nzuri, na tuliweza kuwatembelea wasanii waliotengeneza sanaa tulizonunua. Ni tofauti kidogo na Arusha, kwa sababu Arusha wauzaji wananunua sanaa kutoka kwa wasanii na kutuuzia sisi wanunuzi.

Siku nzuri katika safari yetu ilikuwa siku ile ya mwisho. Tulikwenda mashariki ya Unguja, na tuliona mashamba ya mwani. Lakini, mashamba haya yalikuwa katika kijiji kidogo ambacho kilikuwa maskini. Kulikuwa hakuna mashamba makubwa mjini Unguja. Ninafikiri maisha ya sehemu hii ni magumu sana. Wakulima wanafanya kazi nyingi na ngumu sana, lakini mazao yao hayawapi pesa za kutosha. Karibu wakulima wote ni wanawake, na watoto wanawasaidia. Mfuko mmoja wa mwani mkavu ni shilingi themanini wakati aina nyingine ya mwani mfuko mmoja ni shilingi mia mbili tu. Mkulima mmoja anaweza kuvuna mifuko sita ya mwani kwa wiki tatu, na mifuko hii sita inafanya mfuko mmoja wa mwani mkavu. Maisha haya ni magumu sana, na ninafikiri ni muhimu kuelewa ni kiasi gani wakulima hawa wanateseka kulima vyakula tunavyoviona, kuvila, na kuvifurahia kila siku.

Kilichonifurahisha ni kupata nafasi kuona na kufahamu maisha tofauti na yale tunayoishi nchini Kanada, Marekani, na pia mjini Arusha. Nadhani safari hii na programu yote ya GPA kwa ujumla ilinifundisha na kunionyesha mambo mbalimbali wanayoyafanya Watanzania kila siku katika maisha yao. Historia hii imejificha na ni muhimu kuendelea kuitafuta kwa kuzisikiliza sauti za Watanzania zilizojificha nyuma ya majengo ya zamani ya Wazungu, Wajerumani au Warabu.



Noelle anafundisha jiografia ya Kanada

8. Safari yetu ya Pwani **Rebecca Roeder**

Wakati wa safari yetu katika Dar es Salaam, Bagamoyo na Zanzibar, niliona vitu vingi vipya. Nitaeleza vitu vichache ambavyo vilikuwa muhimu kwa mimi mwenyewe. Jumamosi, tuliposafiri mpaka Dar, niliona mashamba madogo na mashamba makubwa. Mashamba makubwa yanamilikiwa na serikali. Watu wengi wanafanya kazi katika mashamba haya, na wanalima maembe, korosho, mkonge na nazi. Lakini, wakulima ambao wana mashamba madogo wanaweza kulima mazao mabalimbali. Kwa hiyo, wanakula mazao mengine kutoka mashamba yao, na wanauza mazao mengine sokoni. Wanavyofanya kazi hii, hawahitaji msaada kutoka serikalini.

Bagamoyo na Kaole ilikuwa miji ya zamani, na miji hii ina hadithi nyingi. Magofu tuliyoangalia katika Kaole ni kutoka karne ya kumi na tatu mpaka karne ya kumi na tisa. Magofu ya kwanza, magofu ya Uarabu, ni misikiti miwili na makaburi kama kumi na tano hivi. Kuna ngazi juu ya msikiti mmoja kwa sababu mtu mmoja alienda juu ya msikiti kuwaita watu wote kusali. Pia, kuna

mahali ambapo watu walitia udhu kabla ya sala. Watu wa zamani waliamini kwamba maji hapa yaliingia kwa bahati nzuri. Bagamoyo ilikuwa muhimu katika biashara ya watumwa. Watumwa walishurutishwa kukaa katika vyumba vidogo sana. Walisubiri, halafu walitembea katika shimo mpaka pwani. Pwani, waliingia melini mpaka Zanzibar, na waliuzwa katika Zanzibar. Bagamoyo palikuwa mahali pa huzuni sana, na watumwa walibwaga nyoyo zao kule. Ingawa biashara ya utumwa ilimalizwa kwa urasmi mwaka 1873, iliendelea pwani ya Afrika Mashariki mpaka mwanzo wa karne ya ishirini. Watumwa wa awali walijenga kanisa mwaka 1876. Katika Zanzibar, tuliona mahali palipowekwa watumwa, pia, na karibu yake kuna sanaa nzuri ya uchongaji. Watumwa wanne wanasimama katika shimo na minyororo inazunguka shingo zao.

Katika Zanzibar, nilipenda sana safari kwa shamba la viungo na mashamba ya mwani. Sikujua kwamba viungo hivi vinaota pamoja. Tuliona, na tulinusa, viungo vingi sana, kama majani ya limau, karafuu, manjano, pilipili (nyeusi, nyekundu, na nyeupe), yasmini, kungumanga, vanila, hiliki, tangawizi na dalasini. Kila kiungo kinatumiwa kama dawa pia. Kwa mfano, tangawizi inasaidia tumbo na inaongeza nguvu. Baada ya kuona viungo, kijana mmoja alipanda mnazi na kila mtu katika kikundi alikunywa kutoka dafu. Maji kutoka madafu kama hayo ni maji matamu ya ajabu sana.

Kabla ya kutembelea mashamba ya mwani, sikujua kwamba kuna mashamba ya mwani, ingawa nilijua kwamba mwani umo katika vitu vingi—kama aiskrimu, sabuni na vyakula vingine. Wakulima ni wanawake na watoto kwa sababu hakuna pesa nyingi kutoka kazi hii. Kuna aina mbili za miwani katika sehemu tuliyoona. Aina moja ina thamani ya shilingi themanini kwa kilo; aina nyingine ina thamani ya shilingi mia mbili kwa kilo. Kila shamba linaleta kama shilingi elfu tatu hivi kwa majuma matatu. Mwani unahitaji majuma matatu kukua. Mara kwa mara, wanawake wanafanya kazi pamoja, ili waweze kusaidiana. Kampuni kubwa kutoka Ulaya inasababisha bei, na kampuni inataka kufaidi sana. Kwa hiyo, bei ni mbaya kwa wakulima. Ni kazi ngumu, ya hatari, na joto. Wanaume wengi kule ni wavuvi, na wake wao wana mashamba ya mwani kuletea familia pesa zaidi kidogo.

Mada ya mwisho kueleza ni safari yangu mpaka Ubalози wa Marekani, jijini Dar es Salaam. Baada ya kupoteza pasipoti yangu, nilihitaji kwenda ubalози na kupeleka barua kutoka polisi na picha ya pasipoti niliyopoteza. Nisingalikuwa nikijua namba ya pasipoti ambayo iliibiwa, ningalikuwa na matatizo zaidi. Lakini, hakukuwa na shida. Ubalози mpya ni nje ya katikati ya Dar. Aidha, ubalози unafanana na ngome, na milango minene na mizito. Wafanyakazi ni Watanzania, isipokuwa Wahindi wachache na Wamarekani wachache. Watu wote ambao walisubiri kuzungumza na ofisa wa ubalози walikuwa Watanzania, si Wamarekani. Ubalози uliweza kutengeneza pasipoti yangu mpya katika siku moja tu. Baadaye, nilizungumza sana na mtu kutoka World Jet ambaye anaitwa Arnold. Tulienda

hospitali kuona mke wake, ambaye alijifungua mtoto, na tulikula nyama choma ya mbuzi. Nilifurahi kurudi Dar kwa siku moja zaidi.

9. DAR ES SALAAM, BAGAMOYO NA ZANZIBAR

Kris Leefers

Nilienda mashariki ya Tanzania pamoja na wanafunzi wa GPA wiki iliyopita. Tulifurahia na tulijifunza kuhusu vitu vingi. Tuliondoka tarehe kumi na saba mwezi wa saba saa kumi na mbili alfijiri. Tulienda kwa basi kutoka Arusha mpaka Dar es Salaam. Walimu wetu walisafiri nasi pia. Hoteli yetu mjini Dar es Salaam ilikuwa nzuri sana. Iliitwa Courtyard na kulikuwa na bwawa la kuogelea. Siku ya kwanza hotelini wanafunzi wengi waliogelea.

Siku ya pili tulikwenda kutembelea mji wa Bagamoyo. Tulijifunza kuhusu historia ya Afrika mashariki. Zamani, Bagamoyo ilikuwa sehemu kuu ya biashara watumwa. Kwa kiingereza, Bagamoyo inamaanisha, “Leave your Heart“ hii ni kwa sababu ya biashara ya watumwa. Tulitembelea makanisa mawili mjini Bagamoyo pia. Tulirudi Dar es Salaam mchana na tulikwenda kutembelea kijiji cha makumbusho. Tuliona mfano wa nyumba nyingi za Tanzania.

Siku iliyofuata tulitembelea chuo kikuu cha Dar es Salaam. Tulizungumza na walimu kuhusu elimu chuoni. Baadaye tulisafiri kwenda Zanzibar kwa boti. Bahari ya Hindi ilikuwa nzuri sana na kulikuwa na jua kali. Tulikaa hoteli iliyoitwa Stonetown kisiwani Zanzibar. Siku ya kwanza mjini Zanzibar tulitembelea mjini tukiwa pamoja na Lynsey, Jo, na Shannon. Nilinunua kanga na kikoi.

Siku ya pili tulitembelea sehemu ya kihistoria. Tuliona nyumba za sultani. Tuliangalia magofu ya kasri ya sultani ambaye alikuwa na suria tisini na tisa. Katika kasri hii kulikuwa na miti tisini na tisa ya maembe, yaani, kila mti mmoja ukimwakilisha suria mmoja. Baadaye tulitembelea shamba la viungo. Wanafunzi walinunua viungo vingi kwa ajili ya zawadi za familia waliobaki Marekani. Baada ya tukio hili tulikwenda pwani. Tulikula vyakula vya baharini na kulala juu ya mchanga.

Siku ya tatu tulitembelea shamba la mwani. Tulizungumza na mkulima mmoja kuhusu mbinu za kulima baharini. Baadaye tulikula chakula cha mchana pwani. Baada ya chakula cha mchana, tulirudi katika hoteli yetu. Mimi, Jo na Lynsey tulinunua kanga na tulipumzika. Siku ya nne tulirudi Arusha kwa ndege. Nilifurahia sana safari hii ya pwani na ningependa siku moja kurudi kutembelea tena huko.

10. TAARIFA YA SAFARI YA PWANI

Lynsey Farrell

Wiki iliyoopita, wanafunzi wa GPA tulisafiri kwa basi kwenda Dar es Salaam. Tuliampa mapema sana, alfajiri ya Jumamosi na tulimsubiri dereva wa kampuni ya Zara. Mara alipofika Kituo cha Danish, tulianza safari yetu.

Kwanza tulisafiri hadi Dar es Salaam. Njiani, tulisimama katika kituo cha basi kujisaidia na kula chakula cha mchana. Mwanafunzi moja, anayelitwa Eugenia, alisherehekea siku yake ya kuzaliwa. Wanafunzi na walimu wote walikula keki na waliimba wimbo wa kumshangilia pia. Watu wote walisimka kufika Dar es Salaam baada ya safari ndefu. Tulifika Dar saa kumi jioni. Walimu waliwaambia wanafunzi kuona vyumba vyao na baadaye kutakuwa na safari fupi ya kwenda mjini. Ilikuwa ni safari fupi kuona mitaa ya Kariakoo, Ikulu, bahari na katikati ya mji. Baada ya kurudi wanafunzi wengine waliogelea katika bwawa la kuogelea lililokuwa katika hoteli tuliyofikia, na wengine walipumzika vyumbani. Wanafunzi waliochoka kuogelea walienda kula.

Siku ya pili, wote tuliondoka hotelini saa mbili na nusu asubuhi tukifuatana na walimu wetu na kusafiri kwenda kutembelea mji wa Bagamoyo. Kwanza tulikwenda katika magofu ya Kaole. Katika magofu haya, kulikuwa na msikiti wa tangu karne ya kumi na tatu. Pia, kulikuwa na makaburi. Kaole palikuwa ni mahali muhimu kabla ya mji wa Bagamoyo. Palikuwa mji mkuu katika Afrika Mashariki. Baada ya mazungumzo juu ya magofu haya, wanafunzi tulipiga picha karibu na mbuga, mvua ilinyesha kidogo na wanafunzi na walimu tuliondoka kuangalia sehemu nyingine.

Baada ya kuona magofu ya Bagamoyo, tulikwenda kuona kanisa katoliki, mti wenye mnyororo wa watumwa, na mlango ambao mwili wa daktari Livingstone ulipita. Tulisikia njaa na wote tuliondoka Bagamoyo kurudi mjini Dar es Salaam. Tulipofika Dar tulitembelea mtaa wa Samora na kula katika hoteli ya Pizza Inn na Chicken Inn. Tulifurahi sana kwa sababu chakula kilikuwa kizuri na kitamu. Baada ya kula, tulitembeatebea mjini kwa muda mfupi na baadaye tukaenda kutembelea "Village Museum". Katika ukumbi huu kulikuwa na nyumba nyingi zilizoonyeshwa ambazo makabila ya Tanzania wanazijenga. Mwanafunzi Rebecca, hakurudi kwenye basi wakati wengine tuliporudi. Alikuwa akiongea na mvulana aliyetaka kumwoa. Baadaye, tulitembelea maduka ya wachonga vinyago. Wanafunzi na walimu tulinunua zawadi nyingi, na baadaye tukarudi hotelini kula na kulala.

Siku ya tatu, tulitembelea chuo kikuu cha Dar es Salaam. Hapa tulikumbuka masomo ya "core values" kwa sababu watu wa chuo kikuu hawakuweza kufuata ratiba. Wanafunzi tuliongea na mwalimu mkuu wa kitivo cha sayansi na sanaa na mwalimu mkuu wa idara ya Kiswahili kwa muda mfupi. Wakati wa mazungumzo, mwanafunzi mmoja, aitwaye John, alienda hospitali kupata matibibu kwa kuwa alikuwa anaumwa. Yeye alikuwa na wasiwasi hatapata matibabu mazuri, lakini

alipata ushirikiano mzuri na matibabu yake hayakuchukua muda. Baada ya mkutano wa chuo kikuu, wanafunzi tulienda kula chakula cha mchana katika hoteli ya Steers. Tulikula kwa haraka kwa sababu mashua ilikuwa ikitungojea bandarini tayari kwa safari ya kwenda Unguja.

Tulipofika Unguja tulifurahi sana. Tulitembea katika Mji wa Mawe kwa masaa mawili hivi, na pia, tukaingia katika mgahawa ulioitwa Mercury's, kula chakula cha jioni na kusherehekea siku ya kuzaliwa ya mwanafunzi mwingine. Tulikula keki, pia tuliimba wimbo wa kuzaliwa kumpongeza mwanafunzi mwenzetu. Baada ya chakula tulirudi hotelini, lakini mfuko wa mwanafunzi mmoja, jina lake Becky ulibiwa na mwizi. Mwizi alikimbia na hakuonekana hivyo Becky alipoteza pasipoti na pesa zake. Alisikitika na kusikitisha sana. Wote tulikwenda kituo cha polisi na baadaye tukarudi hotelini kupumzika.

Siku ya nne, wanafunzi tulitembelea sehemu mbalimbali mahali katika kisiwa cha Zanzibar. Tulitembelea soko la watumwa na kanisa katoliki mjini Zanzibar. Kanisani kulikuwa na msalaba uliotoka nchini Zambia ikiwa ni kumbukumbu ya daktari Livingstone alipotembelea Zanzibar. Baada ya kuondoka mjini, tulienda magofu ya Marahubi. Sultani Barghesh alijenga jengo hili mnamo mwaka 1882 ili kuwahifadhi wapenzi wake. Idadi ya wapenzi wake ilikuwa tisini na tisa. Mnamo mwaka 1899 jengo hili liliharibika kwa moto. Baada ya kutembelea magofu haya, wanafunzi tulienda shamba la viungo. Tulijifunza kuhusu viungo vingi. Kulikuwa na iliki, pilipili, tangawizi, karafuu, vanilla, n.k. Watu wa kisiwani humu walitumia viungo hivi kutatua matatizo yao. Baadaye tulikunywa maji ya nazi na kununua viungo. Wanafunzi tulichoka sana na kusikia njaa. Kwa hiyo tulienda pwani ya Manga pwani kula samaki na nyama choma na "kukoga" kidogo. Baadaye, tulirudi mjini kuoga na kwenda kutembelea "Old Fort." Tulipoingiaa kwenye ngoma na tulikula tena.

Siku ya mwisho mjini Unguja, wanafunzi tulijifunza kuhusu shamba la mwani. Tulienda katika kijiji cha Bwejuu upande wa mashariki ya kisiwa cha Unguja. Mwalimu wa kijiji alizungumza kidogo kuhusu shamba la mwani na alionyesha shamba lililokuwa baharini. Baada ya kutembelea kijiji hiki, wanafunzi tulitembelea Msitu wa Jozani kuangalia nyani. Wanafunzi wengi waliwagusa nyani na walipiga picha wakiwa na nyani. Siku hiyo, tulikula pilau katika kijiji cha Pete na kutembea pwani kidogo. Tulirudi mjini mapema kwa sababu wote tulipenda kununua vitu mbali mbali au kulala kidogo. Tulikula chakula cha jioni katika mgahawa wa Archipelago. Baadaye tulikula aiskrimu katika hoteli tuliyokuwa tunalala. Wanafunzi wote tulilala mapema.

Wanafunzi wa GPA tulirudi mjini Arusha baada ya safari hii ndefu. Tulisafiri kwa ndege na hatukufurahia kuondoka mjini Unguja kwani pwani yake ilivutia na kufurahisha mno.



Wanafunzi Wanamtembelea Mkulima. Lynsey anaamkiana na mkulima

11. Natasha Appenheimer

Wiki iliyopita, wanafunzi wote wa GPA tulitembelea Dar es Salaam na Zanzibar. Tuliondoka Jumamosi. Tulikuwa na madreva wawili kutoka kwa wakala anayeitwa Zara Safari. Slim aliendesha basi. Tuliondoka TCDC saa kumi na mbili, na tulifika Dar es Salaam saa kumi. Safari ilikuwa ndefu sana. Jumamosi jioni, wanafunzi waliogelea kwa sababu hoteli ilikuwa na bwawa la kuogelea. Pia, baada ya chakula cha jioni, baadhi ya wanafunzi walikutana na dada yake Mwalimu Moshi.

Jumapili, wanafunzi na walimu tulisafiri kutembelea Bagamoyo. Asili ya jina la Bagamoyo ni kubwaga moyo. Hii ni kwa sababu Bagamoyo ni mahali watumwa kutoka Afrika Mashariki walipokusanywa kabla ya kusafirishwa kwenda Zanzibar na baadaye Marekani, Mashariki ya Kati, au Ulaya. Baada ya kuondoka Bagamoyo, watumwa wasingeweza kuwasiliana na familia au kuiona nchi tena.

Mjini Bagamoyo, tuliona vitu vingi. Kwanza, tulienda kuangalia magofu ya msikiti wa kutoka karne kumi na tatu. Magofu ya msikiti yaliitwa Kaole. Nilishangaa kuona mahali pa wanawake ndani ya msikiti. Nilidhani kwamba wanawake hawakuruhusiwa kuingia ndani ya msikiti mpaka walipopigania kufanya hivyo. Halafu, tuliona jengo ambalo ndipo mahali watumwa

walipowekwa kabla ya kupelekwa Zanzibar. Pia, tuliona kanisa Katoliki. Kanisa hili ni mahali watumwa walipopelekwa baada ya uhuru.

Tulirudi Dar es Salaam, na kula chakula cha mchana. Baada ya chakula cha mchana, tulikwenda kutembea sokoni. Baadaye tulikwenda kutembelea soko la wachonga vinyago, pia kuona jumba la makumbusho ya vijiji.

Jumatatu, tulitembelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tulikuwa na mkutano, na niligundua kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina masomo ya filamu. Halafu, tuliondoka kwenda Zanzibar. Tulipokuwa Zanzibar, tulitembelea maduka mbalimbali. Tulikula chakula cha jioni katika hoteli ya Mercury's. Wakati wa kurudi kwenye hoteli tuliyofikia mfuko wa Becky ulibiwa.

Jumanne, tulitembelea soko la watumwa. Tuliona vyumba viwili ambavyo ndipo mahali watumwa walipowekwa. Vyumba hivi vilikuwa vidogo sana, na watu sabini na tano walikaa katika chumba kimoja. Pia, tuliona kanisa la Anglikana. Lilijengwa sehemu iliyokuwa karibu na soko la watumwa. Halafu, tulitembelea magofu ya kasri ya Sultani. Sultani alikuwa na suria tisini na tisa, mke mmoja, na mtoto mmoja. Pia, tulitembelea shamba la viungo na tulipata nafasi ya kuogelea katika Bahari ya Hindi, pia tulikula chakula cha mchana katika hoteli moja ya karibu.

Jumatano, tulipelekwa kutembelea shamba la mwani katika kijiji kimoja. Mwalimu alitusimulia historia kuhusu mwani. Mwalimu alikuwa mtu wa kwanza kulima mwani katika kijiji hiki. Pia, tulipata nafasi ya kutembelea Msitu wa Jozani. Tuliona mbega wekundu. Baada ya matembezi haya tulirudi mjini, tukaenda madukani kujitafutia zawadi mbalimbali. Siku iliyofuata tulirudi TCDC.

Nilipokuwa Zanzibar, niliangalia vitu vingi kuhusu lugha. Kiswahili huko Zanzibar kina jina tofauti. Kinaitwa Kiunguja, na kinatofautiana na Kiswahili kinachozungumzwa mjini Arusha. Lafudhi ni tofauti na pia, watu wa Zanzibar wanatumia maneno kwa namna tofauti. Watu wa Zanzibar wanasema kukoga wakiwa na maana kuogelea. Mjini Arusha kukoga ni neno lingine linalomaanisha kuoga. Pia wenyeji wa Zanzibar husema skuli kwa maana ya shule. Hii ni kwa sababu Zanzibar ilikuwa koloni la Waingereza, wakati Tanganyika ilikuwa koloni la Wajerumani na baadaye kurithiwa na Waingereza.

Ipo tofauti nyingine pia inayohusiana na biashara ya watumwa. Watu wa Zanzibar hawasemi shikamoo kwa sababu wakati wa utumwa, watumwa walilazimishwa kusema shikamoo kitu ambacho walikuwa hawapendi. Hivi sasa, watu wanasema cheichei badala ya shikamoo. Pia, hawatunii neno soko, kwa sababu soko lilikuwa mahali walipouzwa watumwa. Badala yake soko wanaliita markiti. Nilijifunza vitu vingi, lakini kilichonifurahisha zaidi ni kujifunza lugha.



Wakati wa chai: Natasha (katikati) na wanafunzi wengine

12. Sarah Smiley

Nilifurahi kwenda pwani kwa sababu nilitaka kuona utamaduni tofauti na wa Arusha. Nilitaka kuona misikiti, Waislamu, ngome, na maisha ya mjini. Pwani ni sehemu bora kuliko nilivyofikiria. Ningelipenda kukaa pwani kwa muda mrefu zaidi lakini ninajua kwamba nitarudi tena siku moja.

Jumamosi (Tarehe 17), tulianza safari yetu saa kumi na mbili asubuhi. Safari yetu ilikuwa ndefu sana lakini niliona mandhari nzuri sana. Niliona vijiji vingi, watu wengi, na mimea tofauti kuliko iliyopo Arusha. Nilifurahia kuona mandhari inavyobadilika. Tulipofikia Dar es Salaam saa kumi mchana tulienda mjini kwa basi. Tuliona harusi nyingi za pwani. Vijana ambao wanaishi Dar es Salaam wanapenda kupiga picha za pwani. Kila harusi ilikuwa na bendi ambayo ilicheza muziki. Baada ya chakula cha jioni, nilienda kusikiliza muziki Mango Garden. Nilifurahia kuona Watanzania na utamaduni za Tanzania. Niliona watu wakicheza dansi na aina tofauti za nguo. Niliogopa wanaume waliponisumbua lakini watu wote walikuwa wazuri.

Jumapili (Tarehe 18), tulienda Bagamoyo kwa basi. Tuliona magofu ya Kaole. Kuna magofu ya msikiti, nyumba, na makaburi. Tuliona mahali pa historia kama kanisa ambalo mwili wa David Livingstone uliwekwa na jumba la biashara ya watumwa. Tulirudi Dar es Salaam na tulipata na nafasi kutembea mjini. Nilijaribu kwenda sokoni lakini nilipotea. Badala yake, niliona msikiti na maduka madogo. Watu wengi walinisalimu. Hakuna mtu ye yote aliyenisumbua au aliyeniita ‘Mzungu’. Tulienda kijiji cha makumbusho na tuliona nyumba za makabila mengi. Kila nyumba ina mahali pa kupikia, kulala, na kufuga mifugo. Tulienda sokoni na nilinunua zawadi kwa familia yangu. Nilisema kwa Kiswahili na nilipata bei nzuri. Wauzaji walishangazwa kwamba ninasema Kiswahili lakini walidadisi kuhusu masomo yangu. Jioni, nilikutana na rafiki ya mwalimu wangu. Anaitwa Walter Bgoya na alisoma katika Chuo Kikuu cha Kansas. Tulizungumza kuhusu Kansas, familia yetu, na utafiti wangu.

Jumatatu (Tarehe 19), tulienda Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. Chuo ni kizuri sana na mwaka ujao ningependa kusoma pale. Nilikutana na watu wawili ambao watanisaidia: mwanafunzi wa jiografia na mwalimu wa fasihi. Baada ya chuo kikuu, tulienda Unguja kwa meli. Nilipiga picha nyingi za maji, meli nyingine, majumba, na visiwa. Siku moja nitafundisha kuhusu jiografia ya Afrika Mashariki na nitatumia picha hizi. Tulifika hotelini na tulikuwa na nafasi ya kutembelea Mji Mkongwe na kununua vitu. Sikununua kitu cho chote lakini niliuliza bei za kanga, vitambaa, mashati, na vitabu kwa hivyo nitaweza kulipa bei nzuri siku nyingine.

Jumanne (Tarehe 20), tulienda sehemu nyingi. Tulienda katika kanisa muhimu na tulijifunza kuhusu biashara ya watumwa. Tuliona mti ambapo watumwa walipigwa mijeledi. Sasa, mti huu ni sehemu ya historia kwa hivyo watu hawawezi kusahau wakati uliopita. Hali ya watumwa ilikuwa mbaya sana: watu wengi waliwekwa katika vyumba vidogo na watu hawakuwa na chakula au maji ya kutosha. Tulienda katika magofu ya nyumba ya Sultani. Nilishangaa kujifunza kuhusu Sultani alivyokuwa na suria tisini na tisa na vyoo vitano. Alikuwa na shughuli! Tulienda shamba la Bahama kuona viungo. Sipendi kupika kwa hivyo sikujua kuhusu viungo. Tuliona pilipili, vanila, karafuu, kungumanga, tangawizi, iliki, mdalasini, na viungo vingine. Kiongozi wetu, alituuliza majina ya viungo na kila mara, nilikosea. Ni vigumu sana kujua viungo kwa kuangalia tu. Jioni, tuliona ngoma za Afrika. Mchezaji ngoma mmoja alicheza ngoma karibu sana na mimi. Sikumpenda lakini wanafunzi wengine walipiga picha nyingi.

Jumatano (Tarehe 21), tulienda shamba la mwani. Nimeshajifunza kuhusu mwani kwa sababu mwalimu wangu anafanya utafiti Unguja. Nilifurahia kuona wanawake wakifanya kazi lakini bei ya mwani iko chini sana. Kiongozi alituambia kwamba mkulima mzuri anaweza kupata shilingi elfu kumi na mbili tu kila mwezi. Tulienda msitu wa nyani pia. Niliweza kuwa karibu sana na nyani. Baadaye, kulikuwa na nafasi kununua vitu. Sikupenda maduka karibu na hotel yetu kwa sababu

wauzaji walisema kwa Kiingereza tu hata kama niliongea Kiswahili. Nilipoenda mbali na hoteli yetu nilisikia Kiswahili zaidi. Niliona soko la samaki na kulikuwa na samaki ambao ni wakubwa kuliko watoto!

Alhamisi (Tarehe 22), tulirudi Arusha kwa ndege. Nilitaka kukaa pwani kwa sababu nilipenda hali ya hewa na watu wote. Safari ya ndege ilikuwa nzuri kwa sababu niliona mandhari nzuri kwani tuliruka karibu na Mlima Kilimanjaro. Safari yangu ilikuwa nzuri sana. Nilikutana na watu wengi, niliona utamaduni, nilijifunza kuhusu historia ya Afrika Mashariki, na nilifurahi sana.



Wanafunzi darasani. Sara anakaa karib na mwalimu, kulia

13. Safari Yetu

Shannon Montgomery

Jumamosi wanafunzi wa GPA na walimu wetu tulisafiri kwenda Dar es Salaam kwa basi. Sisi tuliamba mapema sana, lakini kwa bahati mbaya, madereva wa basi walichelewa. Safari yetu ilikuwa ndefu sana! Tulifika Dar es Salaam saa kumi na moja jioni. Sisi tulitaka kwenda dukani, lakini tulichelewa na maduka yalifungwa. Kabla ya kurudi hotelini kwetu, “The Courtyard”, tuliona mahali pengi muhimu mjini, kama ofisi ya rais. Sisi tuliogelea katika bwawa la kuogelea, halafu tukala chakula cha jioni.

Siku ya pili tulikwenda Bagamoyo, mji mkuu wa kwanza wa Tanzania. Karibu na Bagamoyo tulitembelea magofu ya Kaole. Kule ni magofu ya msikiti na makaburi. Yalijengwa karibu karne ya kumi na tatu. Msikiti huo ni msikiti wa zamani kuliko misikiti ya Afrika Mashariki yote. Baadaye, tulikwenda mji wa Bagamoyo na tulitembelea kanisa la kwanza la Afrika Mashariki. Kanisa hili lilijengwa na wamishenari ambao walitoka Ulaya. Dr. Livingston alikuwa mmoja wa wamishenari huo. Vilevile tuliona kanisa la Katoliki ambalo lilijengwa kuwaongoza, kuwasaidia, na kuwafundisha watumwa ambao waliwekwa huru. Saa nane mchana tulifika Dar es Salaam na tukala katika Pizza Inn. Pizza zilikuwa nzuri sana. Mimi ninakosa vyakula vya Marekani. Baada ya kula, tulikwenda kijiji cha Makumbusho. Kule ni mifano ya nyumba na desturi ya makabila mengi ya Tanzania. Mimi nilipenda makumbusho haya sana! Sisi hatukukaa muda ndefu, kwa sababu tulitaka kwenda soko la vinyago. Katika soko, mimi nilikwenda katika maduka mengi na nilinunua vinyago vichache.

Jumatatu tulitembelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwanza, wanafunzi wengi nami tulikwenda katika duka la vitabu. Mimi nilinunua vitabu vingi. Baada ya kunywa chai na vinwaji vingine, tulizungumza na viongozi na idara ya sayansi ya jamii na kitivo cha Kiswahili. Professa hawa walitueleza juu ya chuo kikuu. Tulijifunza kwamba chuo kikuu hiki kina kiasi wanafunzi wa 13,000. Wanafunzi wengi wanatoka Tanzania, lakini wanafunzi wachache wanatoka nje ya Tanzania, kama Uganda, Zimbabwe, Ulaya, na Marekani. Vilevile, wanafunzi wengi wanasoma shahada ya kwanza, lakini wachache wanasoma shahada ya pili au zaidi. Kabla ya mwaka 1970, chuo kikuu hiki kiliitwa Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki, lakini jina lake lilibadilishwa kwa sababu kilikuwa na vyuo vikuu zaidi. Baada ya kuzungumza, tulikwenda mkahawa wa Steers. Mimi nilipenda chipsi na ice cream kule, lakini hamburger haikuwa nzuri! Baadaye, tulikwenda bandarini. Tulisafiri Zanzibar kwa meli. Baada ya kufika Zanzibar, tulikwenda hoteli yetu, Shanghai Hotel. Kris, Lynsey, Jo nami tulizunguka Mji Mkongwe, tukanywa vinwaji mbalimbali na tukapumzika kidogo. Wanafunzi wote na walimu wetu tulikula katika Mercury's Zanzibar kwa chakula cha jioni. Kule vyakula vilikuwa vizuri, lakini wahudumu wafanya kazi polepole sana! Sisi tulikuwa tumechoka, lakini chakula cha jioni kililiwa mpaka saa nne usiku.

Jumanne, tulisafiri kidogo mjini. Kiongozi wa watalii wetu alituonyesha majumba muhimu mbalimbali, kama Beit el-Ajaib (Nyumba ya Ajabu), Beit al-Sahel (Kasri ya makumbusho), chumba cha dawa cha zamani, ngome, n.k. Halafu tulitembelea kanisa kuu la Angalikana na mahali pa soko la biashara ya watumwa la zamani. Hali ya kuishi ya watumwa ilikuwa mbaya sana! Mimi sielewi vipi watu waliweza kutendea watu wengine vibaya. Baada ya kuona soko la watumwa la zamani, tulitembelea Kasri ya Marhubi. Kasri hii ilijengwa mwaka 1882 na Sultani Seyyid Barghash. Kule masuria wa sultani waliishi. Sultani huyo alikuwa na masuria tisini na tisa. Katika Kasri ya Marhubi, masuria saba walikaa pamoja. Alipochoka na masuria hawa, aliwauza katika soko na alichagua saba

zaidi. Sasa Kasri ya Marhubi ni magofu tu, kwa sababu kasri iliteteketwa mwaka 1899. Kasri hii ilikuwa na vyumba saba, chumba kimoja kwa kila suria. Sisi tuliona bafu ya sultani. Kulikuwa na dimbwi mbili, moja ilikuwa na maji moto, nyingine ilikuwa na maji baridi. Masuria wa sultani walimfurahisha sultani wakati wa kuoga. Kasri ya Marhubi ilikuwa na vyoo vitano. Vyoo hivi vilitumiwa na sultani tu. Bamvua ilitumiwa kusafisha vyoo hivi. Baada ya kutembelea kasri, tulikwenda shamba la viungo ambalo lilitwa Bahama Spice Farm. Kule tulijifunza sana juu ya viungo, kama basibasi, tangawizi, vanila, pilipili, n.k. Sisi tulipata nazi na tulitazama kiongozi wa watalii akitumia majani ya mnazi kutengeneza kikapu. Baadaye, kwenda katika mkahawa karibu na pwani. Kabla ya kula, sisi tuliogelea baharini.

Jumatano, tulisafiri katika kijiji ambacho kipo karibu na pwani ya mashariki. Kule wanawake wanaotesha mwani baharini. Mpango huu ulianza kusaidia wanawake kuchuma pesa zaidi. Wanawake hawa wanafanyakazi sana, lakini wanalipwa kidogo. Tulijifunza kwamba mwani ina sehemu mbili, spine na cotton. Kwa mfuko wa kilo moja ya spine, wanawake wanalipwa shilingi 80 tu! Kwa kilo moja wa cotton, wanawake wanalipwa shilingi 200 tu! Ni pesa ndogo sana, lakini wanawake wanahitaji pesa hizi kuendelea kuishi.



Sikukuu ya Uhuru wa Amerika. Wanafunzi wanasimula.

Baada ya safari ya kijiji, tulikwenda msitu wa Jozani kuwaona nyani. Zanzibar ni mahali tu penye nyani hawa wakundu Colobus. Sisi tulitembea msituni na tukawaona nyani wengi. Sisi tuliweza kuwa karibu sana na nyani. Mimi nilifurahi sana sana! Mimi ninataka kuchukua nyani hawa Marekani nitakaporudi! Baada ya safari, tulirudi Mji Mkongwe na kwenda dukani. Mimi nilinunulia rafiki na familia yangu zawadi nyingi.

Alhamisi tulirudi MS-TCDC kwa ndege na basi. Sisi hatukufurahi kuondoka Zanzibar, lakini sisi tulikuwa tumechoka sana!

1. **BARUA NDEFU**

Anna Lewandowski

Niliamua kusoma barua ndefu kama hii ya kitabu kilichoandikwa na Mariama Ba na kutafsiriwa na Profesa C. Maganga. Nampenda mwandishi huyu na ndiyo sababu nimependa kusoma kitabu hiki kilichoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Nilishasoma kitabu hiki lakini ilikuwa zamani na siikukumbuki hadithi yenyewe vizuri. Nilipokiona kitabu hiki katika duka la vitabu, niliamua kukisoma tena. Baadaye, nilikumbuka kwamba rafiki yake Sarah (aliyekutana naye huko Dar) ndiye mkuu wa kampuni iliyochapisha kitabu hiki. Kampuni hii inaitwa Mkuki na Nyota Publishers!

Hadithi imeandikwa kama barua kati ya marafiki wawili. Ramatulayi alimwandikia barua ndefu (riwaya nzima) rafiki yake Aisatu. Wanawake hawa wawili ni Wasenegali na dini yao ni dini ya kiislamu. Ramatulayi alimwandikia barua hii ili ampe taarifa rafiki yake kwamba mume wake amefariki. Ingawa habari yenyewe inahuzunisha, lakini Ramatulayi anajisikia kupata uhuru. Baada ya miaka ishirini na tano ya ndoa yao iliyokuwa nzuri, Modu, mume wake, aliamua kuoza mke mwengine. Tendo hili lilimshangaza sana kwa sababu walikuwa wameishi pamoja kwa furaha na bila matatizo. Walikuwa wanagawana pesa na madaraka yote ya nyumba sawasawa. Pia, walikuwa wamejaliwa watoto kumi na wawili.

Ramatulayi alimwelezea rafiki juu ya mke mpya na matukio yote yaliyotokea kumbe hakutambua Modu alikuwa ameshaoa mke mwingine tena. Ramatulayi alikuwa amekasirika kwa sababu Modu hakumwambia ukweli wa mambo yenyewe mpaka alipogundua mwenyewe. Binti mmoja, Daba, alikuwa na rafiki ambaye alimtaja mzee aliyependa. Mzee huyu alimnunulia zawadi nyingi na kumlipia kila kitu. Rafiki huyu, Binetuu, alimwambia Daba kwamba mzee huyu alitaka kumwoa. Binetuu hakutaka lakini wazazi wake walimshauri kwamba kama akikubali na akiolewa na mzee huyu, hatakuwa na tatizo lo lote kuhusu pesa za matumizi, pesa za kulipa ada ya shule, au jambo lolote linalohitaji pesa likitokea maishani. Ramatulayi hakujua jina la mzee huyu na baadaye alishangaa kuwaona ndugu na rafiki za mume wake wakifika nyumbani wakiwa wamevaa nguo za arusi. Walimwambia kwamba Modu alikuwa amemwoa mke mwengine. Siku iliyofuata Ramatulayi aligundua kwamba Binetuu ndiye mke mpya mwenye umri sawa na binti yake.

Ramatulayi alieleza katika barua kwamba mara nyingi alifikiria kumwacha mume wake, lakini hakuweza kufanya hivyo. Kama angalimwacha Modu, angefilisiwa kabisa. Asingekuwa na pesa za kutosha kuwatunza watoto wote kumi na wawili. Pia, katika jamii ya kiislamu, inajulikana wazi kuwa si kosa kuwa na zaidi ya mke mmoja kama una uwezo wa kuwategemeza na kuwatimizia. Alijaribu kuendelea na ndoa yake lakini Modu alijitenga kwa kutorudi nyumbani kwa Ramatulayi mara nyingi. Alichukua pesa zote kutoka kwenye akaunti yao na kumpa Binetuu na familia yake. Maisha yake Ramatulayi yalibadilika sana.

Binti yao, Daba, alikasirika sana na kumtaka mama yake aondoke ili kuanza maisha upya. Urafiki baina ya Binetuu na Daba ulivunjika kabisa, lakini Ramatulayi alikuwa na maoni tofauti. Aligundua kwamba Binetuu hakutaka kuolewa na mume tofauti na mume wake na baada ya kifo chake, hakuwa na msaada wowote. Ramatulayi alimlaumu Modu, siyo Binetuu kwa matatizo na jinsi maisha yake yalivyoharibika.

Aliendelea kumweleza katika barua kuwa watoto wake wamepata wachumba wazuri walio na heshima na wanajali usawa katika uhusiano wao. Ramatulayi anajiuliza vipi maisha ya waafrika yamebadilika lakini bado kuna matatizo ya miaka ya zamani kama vile tatizo la kuishi na mke mpya. Anajaribu kupambanua nafasi ya uislamu katika jamii, na pia kujaribu kuelewa vema jinsi mwanamke mwislamu anavyoishi huko nchini Senegal.

2. HADITHI YA BWANA SHAABA BANILA

Erin Ensley

Kwa muda niliokaa hapa TCDC nilizingirwa na watu walionishangaza kila siku. Hata hivyo, moyo wangu uliguswa na hadithi ya mtu mmoja zaidi kuliko hadithi nyingine. Mtu huyu anaitwa Shaaba Banila, na anafanya kazi hapa TCDC kama fundi nakshi.

Hadithi yake inaanzia nchini Msumbiji tangu mwaka 1934, wakati alipozaliwa kama mtoto wa kwanza wa familia yake ambayo ina watoto tisa. Alipokuwa mtoto alifundishwa ufundi wa kuchonga na baba yake na desturi hii ni urithi wa familia hii, yaani babu na baba yake walikuwa mafundi nakshi pia. Uchongaji ni muhimu katika kabila lake Wamakonde.

Mwaka 1954, akiwa na miaka ishirini, Shaaba aliamua kuhamia nchini Tanzania kwa sababu ya biashara ya utalii. Alifikiri kuwa kama mchongaji angekuwa na nafasi nzuri ya kuuza vinyago vyake. Lakini, hakuzungumza Kiswahili popote! Kwa bahati njema, alipofika Arusha alikutana na mjerumani mmoja aliyemfundisha kuzungumza Kiswahili na kiingereza.

Alianza biashara iliyofaulu na alipata pesa za kutosha. Mwaka 1978 alipata matatizo ya pesa na aliomba kuajiriwa TCDC kama askari, na alikubaliwa. Alifanya kazi ya uaskari kwa muda miaka kumi na tatu, na kustaafu mwaka 1991 akiwa na miaka hamsini na saba. Wakati huo alipendwa sana na wanachuo na hawakupenda aondoke chuoni. Kwa sababu ya kazi yake nzuri mkuu wa TCDC alimpa nafasi kuendelea kukaa chuoni na kuuza bidhaa zake.

Siku hizi mafanikio ya biashara yake yanategemea mazingira ya wanafunzi wa TCDC. Mara kwa mara kazi yake haina faida kubwa kwa sababu gharama za uchongaji zimepanda sana. Kwanza, anahitaji magogo yanatoka kijiji kinachoitwa Magadilisho. Kisha anatakiwa kumlipa mtu mwingine anayembebea mbao mpaka nyumbani kwake kijijini USA River. Zamani alibeba magogo mwenyewe, lakini sasa hivi hawezi kwa sababu ya umri wake. Wakati wa kumhoji alinielea kuwa meza moja humgharimu shilingi elfu tano, na huiuza kwa shilingi elfu sita. Ana uwezo wa kuchonga meza moja kila baada ya siku nne.

Alinielea kwamba desturi hii bado inaendelea katika familia yake na ana watoto saba (msichana mmoja na wavulana sita). Wavulana wote wanafanya kazi ya uchongaji vinyago. Watoto wake wote wanaishi nchini Tanzania. Watatu kati ya hao wanaishi mjini Arusha, na waliobaki wanaishi ukanda wa pwani. Ana wajukuu wawili ambao nao wamejiunga na uchongaji vinyago tangu utoto wao.

Nilipomwuliza juu ya uharibifu wa mazingira, hasa kukata miti ovyo alinijibu kwamba yeye huchukua magogo na hakati miti michanga. Anaelewa ukataji miti ovyo ni tatizo kubwa linalohusiana na uharibifu wa mazingira. Kwa sababu hii hatumii miti ya asili ya Tanzania kujaribu kuihifadhi kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Tabia yake inawapendeza watu wengi. Sijamwona akiwa na huzuni, wala hasira, muda mwingi anaonekana amefurahi na anatabasamu na kila mtu. Hucheka au kuchekesha kwa kuzingatia mazingira aliyopo. Kwa mfano, siku moja alikuja na kinyago kutuonyesha dansi ya Wamakonde, kama alivyokuwa ameahidi.

Sitaweza kusahau mazungumzo yetu nitakapoondoka kurudi nchini Marekani. Takriban kila siku, tunakaa pamoja wakati wa chai, huku tukiongea Kiswahili. Sitaweza kusahau dansi aliyotuonyesha na mawazo yake kuhusu uchongaji vinyago. Pia sitasahau mapenzi aliyoonyesha kwa watu wote aliokutana nao.

3. MUHTASARI: ZIMWI LA LEO

Jo Tague

Katika kitabu kinachoitwa *Zimwi la Leo*, mwalimu wa Kilo na Ketu anawataka watoto kusimuliwa hadithi ya kisasa na babu yao, Mzee Kanzi. Babu yao anawasimulia hadithi juu ya dunia ya zamani. Wakati huu, watu wa dunia walitenganishwa. Lakini, katika sehemu fulani, zimwi lilizuka. Zimwi hili lilikuwa na vinywa na makono mengi. Watu wa sehemu hii walilikaribia zimwi hili na walilipa chakula. Lakini Zimwi hili lilitaka kula na kumeza tu. Baada ya muda mfupi, zimwi liliwataka watu hawa kufanya kazi ili zimwi liliweza kula bila kazi binafsi. Zimwi lilitumia nguo na

mapambo kuwavutia watu. Aliwaambia, ‘Mkikubali kushirikiana nami, mtapata nguo hizi pamoja na vitu vingine vizuri’ (13). Waliliamini na kuliona kama rafiki. Watu walifanya kazi, na zimwi liliendelea kula tu. Baada ya muda mfupi, watu walianza kuliita Kabaila kwa sababu mazao ya juhudi zao yalilifaidi Kabaila tu.

Siku moja Kabaila liliamua kutayarisha mahali pa kuhifadhi chakula chake. Mwandishi anaandika, ‘Huo ndio uliokuwa mwanzo wa viwanda’ (18). Kabaila lilitumia hofu kusababisha watu kufanya kazi zaidi. Liliwaambia ilikuwa lazima walipe kodi kuishi kijijini. Hii ilikuwa mara ya kwanza katika maisha yao kusikia kitu kama hiki. Kabaila lilitaka pesa tu, lakini watu hawakujua maana ya pesa. Kabaila liliwaelezea maana ya pesa. Baada ya muda vile viwanda viliungana pamoja na kujenga miji midogo. Watu walianza kuhama kutoka mashambani. Halafu, Kabaila liliwaelezea watu juu ya mchezo uitwao kamari. Watu walianza kutumia sarafu na noti. Watu nao walifurahi kuwa kulikuwa na njia nyingine ya kuzipata pesa siyo tu kwa kufanya kazi kiwandani. Baada ya muda mfupi, jina la Kabaila lilibadilika. Watu walianza kuliita Bepari.

Lakini, watu walianza kujitenga kwa sababu watu wengi walilichukia Bepari. Walakini, watu wengine walilipenda Bepari zaidi. Mwandishi anaandika, ‘Utengano mkubwa ulianza kuingia baina yao’ (30). Watu waliopenda Bepari walikuwa tayari kuwa kama Bepari ili wapate pesa. Kwa sababu hii, Bepari liliwategemea watu hawa kufanya kazi zaida viwandani. Kila kitu kilihitaji pesa, na umaskini ulianza kuongezeka kila mahali. Watu wengi walianza kutafuta njia za mkato za kupata pesa, na watu walibadilika kabisa.

Siku moja, mzee mmoja aliona watu wawili waliotoka kijiji hiki. Nyuso zao zilijaa majonzi kwa sababu ya hali ya viwanda. Mzee aliwaambia hadithi fulani juu ya umoja katika jamii, na aliwaambia kwamba pesa si kila kitu. Kisha, mzee aliwafundisha, ‘Unajua hali inayokuzunguka mwanangu? Mwenye macho haambiwi tazama’ (40).

Kitabu cha *Zimwi la Leo* kinahusu ukoloni. Kitabu hiki kinafundisha juu ya umoja katika jamii. Baada ya hadithi ya babu yao, Kilo na Ketu walielewa umuhimu wa historia. Watoto wawili walielewa kwamba hadithi hii inahusu leo. Pia, watoto wawili walijifunza kwamba kuna matatizo mengi katika jamii kwa sababu ya ukoloni. Zaidi ya hayo, kitabu hiki kinaonyesha umuhimu wa umoja katika jamii. Mwandishi anaonyesha uwezo wa ulafi kuwatenga watu. Lakini, watu wanakuwa na uwezo kuona ulafi huu na kupata umoja tena.

4. HADITHI YANGU

Rebecca Skiba

Nilipanga kuandika juu ya kitabu cha pili, lakini niliamua kuandika hadithi yangu kwa sababu ni bora zaidi. Kwa hivyo, niliamua kuhusu vitu vya ajabu niliposafiri katika Tanzania.

Nilipofika uwanja wa ndege wa Kilimanjaro mimi na wanafunzi wenzangu tulikuwa tukipata mizigo yetu, lakini nilikuwa na matatizo na mizigo yangu. Niliona mizigo ambayo ilizunguka na nilijaribu kuipata. Nilikuwa katikati ya uwanja wa ndege katikati ya usiku niliokimbiza mizigo badala ya kusubiri mizigo iliyorudi tena. Walinzi walinikodolea macho wakijadiliana kuhusu mzungu huyu anayekuwa chizi kama ndizi.

Siku ya kwanza ya darasa nilijifunza kwamba muda wa chai ulikuwa kila saa na ni muhimu sana sana! Kwa mfano, Natasha, mwanafunzi mwenzangu, alikimbia ghafla kupata kikombe chake cha chai. Sasa, ninamwita "Superman". Nilijifunza pia kwamba unahitaji kusema maneno sawa au unasema maneno ya maana tofauti sana. Kwa mfano, siku moja darasani tuliambiwa kuhusu mkutano ulikuwa juu ya nini. Mimi nilijibu kwamba mkutano kuna mwenyekiti, katibu, na "kifua kikuu" badala ya "makamu". Mama Gaude alitaka kulia kwa kucheka sana. Siku nyingine, nilimwambia Mama Rehema kuhusu kitabu changu. Nilijaribu kueleza kwamba nilifikiri kitabu changu kilikuwa "pumba", lakini nilisema "punda". Sikujui nilisema neno sawa au baya mpaka nilipoona uso wa Mama Rehema. Alinikodolea macho na mdomo ulifunguka kama vile mtu mwingine alimpiga au mtu alikuwa na kichaa cha mbwa. Mara moja nilisema "mkundu", lakini sasa hivi sikumbuki nilijaribu kusema nini. Mfano zaidi ungekuwa niliposema "kuma" badala ya "kuna". Je, sasa umelewa umuhimu wa herufi na kusema sawa? Mimi ninaelewa!!

Kujifunza lugha ya Kiswahili ni rahisi ukilinganisha na kujifunza kuhusu utamaduni, hasa wanaume. Niliamua kwamba nilikuwa peke yangu, lakini binadamu hawakubali. Ninapenda kuzungumza kuhusu vitu vingi na ninajifunza kuhusu watu na misimamo yao. Watu wengi walifikiria wema wangu ni mapenzi. Kutokuelewana huku kulileta matatizo zaidi. Kwa mfano, mlinzi mmoja alinipenda sana. Siku moja tulizungumza kuhusu muziki na ghafla alipanga habari za disco. Niliwaleta kujilinda Kris na John, lakini hawakujaribu kuniokoa mara moja! Halafu mtu wa disco, sasa yeye ni J, na mimi tulikuwa katika disco, tulikaa na niliomba pombe kwa sababu nilijua kwamba usiku huu ulikuwa mgumu sana na nilihitaji msaada mwingi ningalioupata. J aliniuliza maswali mengi kwa hiyo niliondoka kwenda chooni mara kwa mara kupumzika kutoka maswali mabaya zaidi. Nilitumaini alifikiri kwamba niliendesha hivyo yeye angeacha kuonyesha mapenzi kwangu. Baada ya kucheza dansi kidogo tuliwafuata Kris na John katika bar na nilifikiri nilistahili pombe yote kama walivyokunywa. Nilifurahi sana tuliporudi TCDC. Wanaume wengine waliniambia kwamba walinipenda na walitaka kunioa. Kwa mfano, nilikuwa ndani ya soko la

vinyago nilipokutana na mtu mmoja ambaye alitaka kunipa chochote katika duka lake niki kubali kuolewa naye. Nilimwambia “hapana, hapana!”, lakini hakuacha. Sasa hadhi yangu imepanda kwa sababu waliniambia ninaweza kupata ng’ombe themanini kwa mahari yangu.

Niliposafiri kwa boti kwenda Zanzibar hali ya hewa ilikuwa na upepo sana. Sketi ilipeperushwa mpaka juu ya kichwa. Watu waliona chupi changu.

Nilipofundisha shuleni binafsi watoto walinipenda sana walicheka na walisema “Rebecca, Rebecca!”, Ghafla wanafunzi wengi walikuja kama wimbi lilinimeza na walinifungia ndani ya darasani lao. Halafu niliogopa kidogo.

Familia yangu Arusha walipenda kuomba sana. Baba yangu ni mchungaji wa kanisa. Familia yangu ina dini na walipenda kuomba na kuponya watu wengine. Niliponywa mara nyingi kwa kila kitu. Ni sawa lakini niliogopa kwa sababu mama na baba yangu walibadilika kuwa watu wajabu. Walianza kusema haraka haraka, kulia, na mara nyingine kutema mate pia! Kwa sababu Mama aliniambia ilisababisha watu kuwa na Roho Mtakatifu ndani ya moyo. Kanisani ni mahali pana watu walioomba kwa kutumia mbinu hii. Kanisa lilidumu kwa saa tatu na nusu au nne! Hata hivyo, mimi ninaipenda familia yangu.

Ninatumaini umefurahi kusoma hadithi yangu. Kila kitu ni kweli. Asante sana. Kwaheri.

MWISHO



Rebecca Skiba ma mama yake wa Tanzania

5. KIBUYU CHA AJABU

John B. Linsley

Kibuyu Cha Ajabu ni kitabu cha fumbo kwa sababu kina hadithi inayohusu mizimu wengi. Mhusika mkuu katika kitabu hiki ni Mganga Chubwa. Siku moja alifika katika nchi ya Yazalea na aligundua kuwa kila mtu alikuwa na huzuni. Lakini, Mganga Chubwa hakujuua kwa nini watu walikuwa na huzuni. Baada ya muda mfupi aliambiwa na mfalme wa Yazalea kuwa malkia wa nchi hiyo alikuwa amefariki na ilwahuzunisha wananchi wengi. Mganga Chubwa alimwambia mfalme kuwa angeliweza kumfufua malkia. Lakini, mfalme hakujuua kuwa Mganga Chubwa alikuwa tapeli! Mganga Chubwa hakuweza kumfufua malkia ingawaje alimtia matumaini mfalme angeweza kufanya kazi hiyo.

Baadaye Mganga Chubwa aliiba kibuyu cha mfalme. Mfalme alitafuta watu arobaini ili kumkamata Mganga Chubwa. Watu waliotaka kumsaidia mfalme walikuwa na moyo sana, lakini hawakufikiri kwa makini. Muda mfupi baada ya kuondoka kijijini watu hao walifika mtoni. Kulikuwa na mzee mmoja karibu na mto huo lakini wasaidizi wa mfalme hawakutaka kuzungumza na mzee huyu. Alikuwa mzee mwerevu na alijua habari za mganga Chubwa. Watu hawa walivamia mto na kuingia majini haraka. Wimbi lilikuja likawazoa wote waliokuwa mtoni, na hakuna aliyepona, wote walikufa maji. Kwa sababu ya msiba huu, na kushindwa kwa wasaidizi wa mfalme kuvuka mto, Mganga Chubwa aliweza kutoroka.

Mwanaume mmoja aliyeitwa Haruni alifika katika nchi ya Yazalea kujifunza kucheza muziki. Vilevile, alijifunza siri za mto uliopita katika nchi hii kwa sababu mzee mmoja alimwelezea habari zake. Haruni alisafiri sehemu nyingi za Yazalea, pia akapita na kuvuka mto na kugundua mahali Mganga Chubwa alipoishi. Haruni alicheza muziki mbele ya nyumba ya Mganga Chubwa na mke wa Mganga Chubwa alikuja kusikiliza muziki huu mtamu. Mke wa Mganga Chubwa aliupenda sana muziki wa Haruni na alimtaka Haruni amfundisha mume wake kucheza muziki. Haruni alikubali, lakini alitoa sharti kuwa alitaka kibuyu baada ya kumfundisha mume wake. Mke wa Mganga Chubwa alikubali na alileta kibuyu na kumkabidhi Haruni. Baada ya kupokea kibuyu hiki, Haruni aliondoka haraka na kurudi katika nchi ya Yazalea. Muda mfupi baadaye, Mganga Chubwa alipata habari kuhusu mambo aliyofanya Haruni. Aliamua kumfuata Haruni lakini Haruni alitembea mbio na mganga Chubwa hakuweza kumwona kabla ya kufika mtoni. Alipofika mtoni Mganga Chubwa hakujuua siri ya mto. Aliyavamia maji ya mto kwa haraka na ghafla likaja wimbi kali lililompiga kumbo Mganga Chubwa na kumfanya kuzama mtoni. Kwa bahati nzuri mawimbi yalikuwa makali sana hivyo yalimrusha juu juu mganga Chubwa na ghafla akajikuta amepachikwa katikati ya mti ulioota mtoni.

Mganga Chubwa alipiga kelele kuomba msaada na wanajeshi wa mfalme walikuja kumwokoa na kumkamata kwa makosa aliyokuwa amefanya ya kuiba kibuyu cha mfalme. Haruni alisifiwa sana na mfalme na alitajwa kuwa shujaa katika nchi ya Yazalea.

Mwisho...



John anafundisha juu ya Afrika

6. URITHI WA MTOTO WA FISI

Natasha Appenheimer

Kulikuwa na msitu uliokuwa na wanyama wengi. Msitu huu ulikuwa na mfalme mmoja tu. Simba aliwatawala wanyama wote, pamoja na mawaziri wake watatu, Chui, Nyumbu, na Mbuni. Simba alikuwa mfalme mzuri sana. Pamoja na mawaziri wake, alilitatua kila tatizo. Ukivunja sheria, uliadhibiwa. Kwa sababu ya utawala wa Mfalme Simba, kulikuwa na amani msituni.

Fisi Mwenye Madoadoa na watoto wake wawili walikaa msituni pia. Fisi Mwenye Madoadoa alikuwa na kaka mmoja. Kaka yake alikaa msituni, lakini alikuwa mgonjwa kwa muda mrefu. Kaka yake alikuwa na mtoto mmoja mdogo. Mama wa mtoto huyu alishafariki.

Siku moja, kaka yake alimwambia Fisi Mwenye Madoadoa kuja kumwona. Fisi alijua kuwa anafariki, na alitaka kumwomba kaka yake kumtunzia mtoto wake. Pia, Fisi alijua kwamba mtoto wake alikuwa mdogo sana, na asingeweza kuelewa juu ya urithi. Fisi alitaka kaka yake akabidhiwe shamba na nyumba yake hadi mtoto wake atakapokuwa mkubwa. Pia, alitaka Fisi Mwenye Madoadoa kuhamia nyumbani kwake na watoto wake. Fisi Mwenye Madoadoa alikubali, na kuondoka.

Baada ya Fisi Mwenye Madoadoa kuondoka, Fisi alidhani kuwa alihitaji kuwaambia marafiki zake pia kuhusu urithi wa mtoto wake. Rafiki zake walikuwa Pundamilia na Kima waliomsaidia kujengea nyumba yake. Fisi aliwaeleza kuhusu mipango yake, na rafiki zake walimwambia kwamba alihitaji kuandika maandishi juu ya mipango yake. Walimfahamu Fisi Mwenye Madoadoa. Alikuwa mvivu, na hakuwa na shamba. Fisi alikataa kuandika maandishi juu ya mpango wake wa urithi.

Siku chache tu baada ya kuzungumza na kaka yake na rafiki zake, alifariki dunia. Baada ya matanga, Fisi Mwenye Madoadoa alihamia kwenye nyumba ya kaka yake. Alikaa pamoja na watoto wake na mtoto wa kaka yake kwa muda mrefu. Mtoto wa kaka yake alikuwa mkubwa, lakini Fisi Mwenye Madoadoa hakumweleza kuhusu urithi wake. Fisi Mwenye Madoadoa na watoto wake walitumia shamba la urithi kujipatia faida. Hawakutaka kumpa Mtoto wa Fisi shamba na nyumba yake ya urithi. Waliamua kwamba hawatamweleza Mtoto wa Fisi kuhusu urithi wake.

Mtoto wa Fisi alikuwa mtu mzuri. Siku moja, aliamua kutaka kuo. Alimweleza Fisi Mwenye Madoadoa, lakini alimwambia kwamba alihitaji eneo la kulima kwanza, kwa sababu hawawezi kuishi katika shamba lile pamoja. Alimwambia Mtoto wa Fisi kuwa shamba na nyumba zilikuwa ni urithi wa Fisi Mwenye Madoadoa. Mtoto wa Fisi alihisi labda hii si kweli, kwa sababu alikumbuka kwamba yeye na baba yake waliishi pamoja katika shamba lile. Hata hivyo, Mtoto wa Fisi alisubiri.

Baada ya kuzungumza na Mtoto wa Fisi, Fisi Mwenye Madoadoa alifanya mazungumzo na rafiki zake. Aliwauliza Nyati na Ngedere kumpa msaada. Aliwapa vitu mbalimbali kama zawadi, na walikubali kusaidia Fisi Mwenye Madoadoa kumdanganya Mtoto wa Fisi.

Siku moja, Mtoto wa Fisi alikutana na Kima msituni. Kima alimweleza Mtoto wa Fisi kuhusu urithi wake. Mtoto wa Fisi alitaka kwenda kwa Mfalme Simba, lakini Kima alitaka kuzungumza na Fisi Mwenye Madoadoa kwanza. Kima alimtembelea Fisi Mwenye Madoadoa, na walizungumza kuhusu urithi wa Mtoto wa Fisi. Hata hivyo, Fisi Mwenye Madoadoa alimpa Kima chai pamoja na majani ya mti wa mtepei. Baada ya kunywa chai, hii Kima alipata kichaa.

Mtoto wa Fisi aliamua kwenda kwa Mfalme Simba. Alitaka msaada. Mtoto wa Fisi alieleza tatizo. Mfalme Simba alitaka Mtoto wa Fisi, Pundamilia, Fisi Mwenye Madoadoa, na rafiki zake Fisi Mwenye Madoadoa kufika siku iliyofuata. Fisi Mwenye Madoadoa alieleza hadithi yake, na rafiki zake walimuunga mkono. Rafiki zake walisema kwamba wao ndio waliojenga nyumba ile.

Wakati Mtoto wa Fisi na Fisi Mwenye Madoadoa walipokuwa wakigombana kuhusu nyumba ya urithi, Tembo alimpeleka Kima kwa Mganga Kenge. Mganga Kenge alimpa Kima dawa.

Mfalme Simba alimwuliza Mtoto wa Fisi kueleza hadithi yake tena. Nao Mawaziri wa Mfalme waliwauliza rafiki zake Fisi Mwenye Madoadoa maswali kuhusu nyumba ya urithi. Wote walijibu, na halafu waliwauliza Pundamilia maswali pia. Pundamilia alijibu, na majibu yake yalikuwa ya kweli. Alimwonyesha Mfalme Simba kwamba rafiki za Fisi Mwenye Madoadoa na Fisi Mwenye

Madoadoa mwenyewe wote walikuwa waongo. Kima naye aliitwa kwa mfalme an alifika kutoa ushahidi. Alikubalina na Pundamilia, na rafiki za Fisi Mwenye Madoadoa walikubaliana na Kima. Mfalme Simba aliamua kwamba Fisi Mwenye Madoadoa na watoto wake wahame msituni, na kamwe wasirudi. Aliamua shamba na nyumba ni urithi wa Mtoto wa Fisi aliyefariki.

Somo au fundisho tunalopata mwisho wa hadithi hii ni kuwa: “ukweli unafichua na uongo.”

7. MRADI WA KITABU

“ZIMWI LA LEO”

Noelle Sullivan

Kitabu nilichosoma kinaitwa “Zimwi la Leo.” Kutokana na jina hili ungefikiri kwamba ni hadithi ya watoto inayohusu zimwi. Lakini, hadithi hii ina taarifa iliyofichua mambo yaliyohusu ukoloni, ubeberu, na ulafi. Kitabu hiki ni kigumu kidogo, kwa sababu kina hadithi tatu zinazofanya hadithi moja. Kuna hadithi ya watoto wanaotaka kusimuliwa kuhusu mambo ya leo, kuna hadithi inayohusu babu yao, na katika hadithi hii kuna hadithi nyingine inayohusu matatizo yanayoweza kuletwa na pesa.

Kitabu kinaanza na watoto wawili waliopewa mradi mgumu na mwalimu wao. Mwalimu aliwaambia watoto hawa wawili kumwomba babu yao awasimulie hadithi inayohusu mambo ya leo badala ya mambo jana. Watoto waliogopa kwa sababu hawakujua kama babu yao alijua hadithi iliyohusu mambo ya wakati uliopo. Walipomwomba kuwasimulia hadithi, babu yao alikubali lakini aliwaambia kabla ya kufahamu mambo ya leo walihitaji kujua mambo ya jana ili kuweza kupambanua mambo yanayohusu leo na kesho. Babu aliwahusia kuwa wanahitaji kuelewa jana vizuri ili kupata mwanga wa kuelewa leo na kesho. Babu aliwasimulia wajukuu wake hadithi moja.

Hadithi ilihusu zimwi lililokuwa na vinywa vingi vikubwa na mikono mikubwa, lakini lilikuwa halina miguu miwili. Kwa kukosa miguu Zimwi lilisikia njaa na lilikuwa halina uwezo wa kupata chakula cha kutosha. Zimwi hili lilifika sehemu waliyokaa watu wanaojitegemea. Watu hawa walikuwa na maisha mazuri, mapenzi na umoja. Pia walikuwa na vyakula vingi vya kutosha. Watu hawa waliamua kulisaidia zimwi kwa kulipa chakula, lakini lilihitaji chakula kingi kujaza tumbo. Watu hawa ilibidi kufanya kazi ya ziada kulilisha zimwi. Huyu zimwi aliwaomba wafadhili wake waendeleo kutoa msaada wa chakula na zimwi aliahidi zawadi ya nguo na vitu vingine vizuri. Watu waliomsaidia zimwi walimwita zimwi huyu “Wantu” yaani “Kabaila”, kuashiria kuwa zimwi likikikaba chakula kwa hila zake.

Kazi za Wantu zilimfaidisha Kabaila, na Wantu walidhani kuwa Kabaila ni mzembe. Kabaila aliwalazimisha Wantu kujenga viwanda kuhifadhi vyakula, ingawaje Wantu hawakumpenda kwa

sababu kazi ya kumlisha kabaila ilikuwa kazi ngumu sana! Zimwi liliwaambia kuwa wakiendelea kufanya kazi viwandani, watoto wao watafaidika. Zimwi aliwalazimisha kulipa kodi ya kuishi kutokana na pesa walizopata kiwandani. Wantu walikuwa hawajui pesa bado. Kabaila aliwaletea ubepari. Waliweza kupata pesa kwa kufanya kazi viwandani, lakini kazi zilikuwa nyingi, ngumu, na zilizidi kazi za zamani.

Kabaila pia aliwaletea kamari na kuwaambia kwamba ilikuwa njia nyingine ya kupata pesa bila kufanya kazi ngumu. Walimlipa Kabaila kodi, na pesa zilizobaki walizitumia kuchezea kamari. Kabaila alishindwa kucheza kamari na wantu walifaidi pesa zake pia. Wantu walilibadilisha jina la Kabaila kuwa “Bepari.”

Baada ya muda baadhi ya Wantu walibadilika na kufanana na zimwi. Walikuwa na vinywa na mikono iliyofanana kama ya Bepari, na walikuwa walafi kama Bepari. Waligeuka nao kuwa mazimwi. Uhalifu uliongezeka. Wantu waliendelea kufanya kazi ngumu, lakini hawakupenda maisha yao kwa sababu mazimwi hayakuoga jambo lililosababisha viwanda na pesa kunuka vibaya. Kwa sababu hii mazimwi na Bepari walibadilisha majina yao na kuwa “Beberu”.

Siku moja, mzee mmoja alirudi nyumbani na kuikuta hali ya familia yake ni mbaya sana. Alijua kuwa pesa si kila kitu. Aliamua kuwasimulia hadithi hii. Hadithi hii inafundisha watu wa familia kwamba pesa zinaweza kuwaletea vitu fulani, lakini hawawezi kuzila. Umoja na ushirikiano unaweza kuwaletea furaha. Baada ya kuwasimulia hadithi hii, familia ilianza kufahamu kwamba hali ya maisha yao ilikuwa mbaya kwa sababu ya ulafi na utengano.

Hadithi hii aliyosimulia mzee huyu ilikuwa ni hadithi ya mwisho kusimuliwa na babu kwa wajukuu wake kuwaonyesha mambo yanayohusu leo. Hata hivyo watoto hawa walishindwa kuelewa hadithi aliyowasimulia babu kama ilikuwa ni hadithi inayohusu mambo ya leo. Babu aliwaambia kuwa hadithi yake ilihusu mambo ya leo, na wao walitakiwa kusimulia hadithi inayohusu mambo ya kesho.

Niliipenda hadithi hii inavyofundisha mambo yanayohusu wakati, hasa mambo yaliyopita yanayohusu historia kwani historia ni muhimu sana. Unaweza kujifunza vitu vingi sana katika kitabu hiki. Kwanza, kinafundisha kuwa ni muhimu kufahamu mambo yaliyopita kuweza kufahamu mambo ya leo na kuweza kufanya uamuzi mzuri kwa ajili ya kesho. Mazungumzo tuliyoifanya kuhusu mazingira yalifundisha taarifa kama hizi pia. Matukio ya leo yanatuletea historia. Kukata miti bila kupanda mingine kutaleta matokeo mabaya sana kesho. Kitabu hiki kinatufundisha kwamba hapo zamani watu walikuwa na umoja, walisaidiana, walifanya kazi pamoja na walipeana vitu kwa ajili ya mahitaji mbalimbali. Ukoloni uliwaletea watu ulafi na utengano. Ukoloni uliyaondoa mapenzi na umoja na kuwafanya watu kuishi bila furaha. Kitabu kinashauri tuchague umoja badala ya ulafi, tukuze undugu wa kusaidiana na kutunzana. Pia, kinafundisha kuwa pesa peke yake haziwezi

kutuletea maendeleo. Tukiwa na fedha bila vitu vya kutumia fedha zetu, pesa zitakuwa hazina maana. Pesa bila undugu na umoja ni hatari, kwa sababu pesa peke yake haziwezi kumsaidia mtu, bali undugu uliojaa upendo vikichanganywa na pesa vitaleta maendeleo na amani.

8. CHUO KIKUU CHA INDIANA UNIVERSITY

JITUKALI

MWANDISHI: HURAMU A. SAKAFU

Eugenia D. Williams

Hadithi hii ilitungwa kuonyesha vijana kwamba matatizo huwapata watu wote katika maisha. Kwa mfano, uzoefu unamsaidia kijana kufahamu kuwa kila mtu ana uzoefu tofauti katika maisha na matatizo yanatofautiana, kinachohitajika ni subira na uvumilivu na huenda mwisho mambo yakawa mazuri.

Hadithi inaanzia katika mji wa Nansio uliopo katika Kisiwa cha Ukerewe ndani ya Ziwa Victoria. JituKali alikuwa mzaliwa pekee kwa wazazi wake. JituKali alikuwa na tabia jema; aliwasaidia wazazi kufanya kazi katika shamba lao dogo wakati wazazi wake walipokuwa wakipunga upepo kando kando ya Ziwa Victoria katika Kisiwa hiki. Siku moja JituKali alikaa mbali na pwani huku akifikiria kuhusu kufunga safari ya kwenda Dar es Salaam. Alipowaambia wazazi wake juu ya mpango wake wa kusafiri kwenda mjini Dar, wazazi walihuzunika sana, lakini baadaye walikubali asafiri. Wazazi wake walimuasa kuwa wazo lake la kwenda Dar lilikuwa zuri lakini ilibidi ajichunge sana anapokuwa mjini. Jitu Kali alikuwa hana pesa hivyo ilibidi auze ng'ombe mmoja na punda mmoja. Alipanda meli hadi mjini Mwanza na baadaye alipanda gari moshi mpaka mjini Shinyanga. Kutoka mjini Shinyanga alipanda basi hadi mjini Dodoma waliposimama kwa muda na baadaye kuendelea hadi jijini Dar es Salaam. Alipofika Dar es Salaam, ilikuwa saa kumi na moja asubuhi. Siku nzima alitembea mjini akiwa na mawazo, hofu, na mashaka. Alihuzunika kwa sababu alikuwa hana pesa za kutosha na alikuwa hajui angefanya nini katika maisha yake. Mara nyingine, vitu vibaya hutokea hata kama mtu anajitahidi kufanya bidii kufanya vitu vilivyoy bora. Kwa mfano, ilipokuwa giza Jitukali alijikuta akiwa na vijana watatu wahuni waliomfundisha mambo mabaya. Vijana hawa walimfundisha Jitukali vitu vingi vibaya kama vile wizi, kwenda sinema, na kujiingiza katika mambo ya ulevi vitu vilivyomfanya kubadili tabia yake nzuri na kuwa mhuni na jambazi la mjini Maisha yalipozidi kuwa magumu Jitukali aliamua kutafuta mbinu za kunusuru maisha yake, hivyo alianza kuuza karanga. Jambo moja likitokea huwa linafuatiwa na jambo jingine. Jitukali alikuta akifanya kazi tena na akawa na mawazo mazuri kuhusu maisha yake mwenyewe. Baada ya kupata pesa aliamua kurudi kijijini Ukerewe akaanza kufanya kazi kwa bidii katika shamba lake na kupata pesa nyingi jambo lililompa furaha tena.



Wanafunzi juu yas mchanga usogeao

9. MUHTASARI: ROSA MISTIKA

Lynsey Farrell

Karibu na Ziwa Victoria nchini Tanzania, kulikuwa na familia yenye baba, mama na wasichana watano. Baba aliitwa Zakaria. Yeye alikuwa mlevi sana. Mke wa Zacharia aliitwa Regina. Mara nyingi Zakaria alimpiga Regina kwa sababu ya ulevi. Watoto wao waliitwa Rosa Mistika, Flora, Honorata, Stella na Sperantia. Rosa Mistika alikuwa kifungua mimba, ambaye ndiye mhusika mkuu katika hadithi hii.

Alipokuwa na umri miaka kumi na tano, Rosa alipata barua kutoka kwa mpenzi wake Charles. Baba yake alikasirika kwa sababu aliwachunga binti zake kama ng'ombe. Zakaria hakutaka Rosa Mistika kuzungumza na wavulana. Rosa aliadhibiwa na baba yake na tangu hapo hakupenda kuongea na mvulana yeyote. Rosa Mistika alikuwa mwanafunzi mzuri. Alifaulu mtihani wa darasa la

saba lakini familia yake hawakuwa na pesa za kutosha kumpeleka sekondari. Hii ni kwa sababu baba yake alikuwa mlevi na hakuweza kulipa ada za shule. Kuona hivyo Regina na Rosa waliuza ng'ombe na pombe kupata pesa ili Rosa aweza kuenda shule ya sekondari.

Rosa Mistika alikuwa na bahati mbaya. Shuleni hakuwa na marafiki wengi. Alikuwa na rafiki mmoja tu. Jina lake ni Thereza. Pia, mwalimu wa shule, Sister John, alimpenda Rosa Mistika. Lakini uhusiano wake huu na mwalimu ulimletea Rosa matatizo mengi. Wasichana wa shule walipolala mjini, Rosa alitaja majina wasichana watoro kwa Sister John. Baada ya kugundua kuwa Rosa ndiye aliyekuwa anatoa siri, wasichana wote katika shule hawakumpenda Rosa Mistika. Walichoma nguo zake na kuharibu daftari zake pia. Siku moja alipokuwa mjini Rosa aliwasikia wavulana wa mjini wakiongea kuhusu tabia yake. Alisikitika kwa sababu walimwona kama vile alikuwa kilema.

Siku moja Rosa alikutana na mvulana mmoja jina lake Deogratias. Walikutana na Deogratias katika dansi. Rosa alijisikia kumpenda sana Deogratias lakini Deogratias alikuwa mwongo. Deogratias alimwambia Rosa alitaka kumwoa. Deogratias hakutaka kumwambia Rosa kuhusu umri wake au mambo aliyofanya wakati wa utoto wake. Rosa alisikitika sana. Baada ya dansi Rosa alienda mjini kujaribu kujisahaulisha mawazo aliyokuwa nayo.

Maisha ya Rosa yalianza kuwa mabaya. Alipokuwa chuoni Morogoro Rosa alipata mimba ambayo aliitoa. Padri alijaribu kumsaidia, lakini hakujali kwani alishahisi kuwa maisha yake yameharibika. Alifanya mapenzi na wanaume wengi hata mkuu wa chuo! Habari hii ilienea chuoni kote na ikawa ndilo gumzo la kila siku, jambo lililomfanya Rosa kuikumbuka familia yake. Alienda nyumbani kuwaona wazazi wake. Baba yake alikasirika sana jambo lililomfanya Rosa kuondoka tena nyumbani. Aliporudi shuleni aligundua kwamba Bw. Thomas mkuu wa chuo, alishahama na mke wake. Rosa alisikitika sana na aliamua kutoroka shuleni.

Baada ya kuhama kutoka Morogoro, Rosa alienda kuishi mjini Mwanza. Siku moja, alipokea barua kutoka kwa Charles, mtu aliyejulikana sana kijijini. Charles alitaka kumwoa Rosa na alipenda kuishi pamoja naye. Walifanya mipango ya ndoa. Rosa bado alikuwa anasikitika akiwa na mawazo ya kutaka kufanya kitu kingine.

Charles na Rosa walienda kijijini kuwafahamisha wazazi wa Rosa pia kuomba ruhusa ya kufunga ndoa. Wazazi wa Rosa waliikataa ndoa hii. Baadaye, walihudhuria mazishi ya baba yake na mama yake Charles waliokufa. Rosa hakuwepo kwenye mazishi wakati huu kwa sababu alisharudi nyumbani kujiua. Alipondaponda kioo akatia maji na kunywa. Dada yake aliporudi alimkuta Rosa karibu ya kufa. Maisha ya Rosa Mistika yaliisha.

Hadithi hii ilihusu suala la jinsia. Mwanamke kama Rosa alihitaji malezi tofauti. Baba yake aliwachunga watoto kama ng'ombe. Hakujali watoto wake kupata elimu. Ilimbidi Rosa kuingia

duniani bila msaada wowote. Mtunzi wa hadithi hii alitaka kufahamisha wasomaji kuhusu mambo muhimu ya maisha hasa suala la elimu. Elimu ndiyo mwalimu wa dunia. Rosa alikosa elimu, na alitumbukia kwenye mataizo makubwa, an hatimaye alipoteza maisha yake. Elimu ndiyo msingi wa maendeleo.

10. Debe la Dhahabu **Charles J. Elfer**

Debe la Dhahabu ni kitabu kilichoandikwa na Mehta Abeid mwaka 1993. Kitabu hiki kilichapishwa na Heko Publishers mjini Dar es Salaam. Hadithi hii ina watu wakuu ambao ni Mfalme Jitu, Zaudi, Tozo, na Saki. Mfalme Jitu ni mfalme wa nchi ya Matembo. Yeye ni mtu mkubwa na alikuwa na jeshi lenye nguvu sana. Mfalme Jitu alikuwa na mke aliyeitwa Malkia Zaudi.

Mfalme na Malkia walikuwa na matatizo makubwa kwa sababu ufalme wao haukuwa na vyakula vya kutosha. Mfalme Jitu alifahamu kwamba watu wake walikuwa na njaa. Kuwasaidia watu wote, Mfalme Jitu aliamua kufungua mfuko wa akiba ambao ulifichwa karibu na ngome ya Mfalme. Mfuko huu wa akiba ulikuwa mkubwa sana. Hazina hii ilikuwa debe la dhahabu na Mfalme Jitu alitaka kutumia kununua vyakula kwa watu wake na ufalme huu. Kwa bahati mbaya, alipoenda kupata hazina yake hakuiona. Mfalme Jitu aliibiwa. Mfalme Jitu na Malkia Zaudi walifahamu kwamba mlinzi aliyeitwa Tozo aliiba hazina yao. Mfalme Jitu alimwuliza mke wake kumpa ushauri wake. Malkia Zaudi aliamuru Tozo kuwekwa katika jela kwa miaka kumi.

Mlinzi Tozo alikuwa na mtoto mdogo aliyeitwa Saki. Saki aliona wasiwasi mwingi kwa sababu alifahamu kwamba babake alienda jela. Wakati huo Saki alikuwa na miaka saba tu. Siku moja, Saki alijaribu kumkamata ndege mdogo kwa mtego. Saki alifanya mtego huu kwa ungo na kipande cha mti. Mwishoni, Saki alimkamata ndege huyu, lakini ndege huyu alikuwa tofauti sana. Ndege huyu aliweza kusema. Kwa kweli, ndege alijua namna ya kusema lugha nyingi. Baada ya Saki kumkamata ndege, saki na ndege walizungumza na waligeuka rafiki wazuri. Ndege huyu alikuwa na akili sana na alifahamu kwa nini Saki alikuwa na wasiwasi. Ndege alimsaidia Saki kumsaidia babake. Ndege alimwongoza Saki mpaka mahali muhimu sana. Karibu na mahali hapa, Saki na ndege walimwona Mfalme ya majoka. Mfalme ya majoka alimwambia Saki kwamba Malkia Zaudi alikuwa mtu mwovu na kwamba babake alikuwa bila ya kosa. Mfalme wa majoka alikuwa na mishangao miwili. Kwanza, alimpa Saki barua iliyoeleza uwongo juu ya Malkia Zaudi. Barua hii ni maalumu sana kwa sababu kusoma barua hii, mtu huhitaji unyoya wa ajabu. Baada ya hapo, Mfalme wa majoka alimpa Saki debe la dhahabu kupelika kwa ufalme wa Matembo.

Saki alirudi ufalmeni kumwambia Mfalme Jitu na kumsaidia babake. Saki alimwonyesha barua yake Mfalme Jitu. Kwa unyoya wa ajabu, Mfalme jitu alisoma barua hii na baadaye aligeuka

mfalme mwenye hasira. Alimwambia mke wake kuenda kumwona waziri mkuu kwa hukumu yake. Wakati ule, Mfalme Jitu aliona debe la dhahabu na alifurahi sana. Mfalme Jitu alitaka kumfanya Saki mfalme mpya. Saki alifurahi, lakini alipenda kumpa babake ufalme. Watu wote walishangilia. Mfalme Jitu na Tozo walinunua vyakula kwa ufalme mzima.

Somo moja kwa hadithi hii ni kwamba mtu anapofanya vitu vibaya, matokeo yatamrudia. Malkia Zaudi alifanya kitu kibaya kwa kuficha ukweli kuhusu debe la dhahabu. Mwishowe, Malkia Zaudi alishikwa kwa haki na Ufalme wa Matembo na alikwenda jela.

11. INSHA KUHUSU LABA MSICHANA SHUJAA

Rebecca Roeder

Hadithi hii inakuhusu familia moja iliyokuwa ikilinda mazao yao kwa bidii. Baba anaitwa Mzee Delo, na ni mkulima. Mazao anayolima ni maharagwe na mahindi. Pia anafuga mifugo kama vile ng 'ombe, mbuzi na kondoo. Hadithi inaanza huku ikionyesha kuwa familia imeshavuna mazao yote shambani na baba ameamua kwenda mjini Arusha kutafuta mnunuzi. Mzee Delo ana watoto watatu Laba, Garu, na Aboo.

Mzee Delo alipofika Arusha alimwona mtu aliyemfahamu, jina lake Konkumo. Delo alimwambia Konkumo kwamba alikuwa anakwenda mjini kutafuta bei nzuri ya mazao yake. Konkumo alimjibu Delo kuwa, atapata bei nzuri mjini Arusha. Konkumo na rafiki zake ni wezi. Usiku Konkumo na watu wengine watatu walikwenda shambani kwa Mzee Delo kujaribu kuiba magunia yake yote ya mahargwe na mahindi.

Watoto wa mzee Delo hawakuwa wapumbavu. Kwa kuwa walibaki nyumbani kulinda mali ya baba yao, walitengeneza mtego wa kutega wezi au wanyama wakali. Walitengeneza kamba mbili za mkonge, na kutoka shambani walifunga kamba hizi juu ya milango ya boma lao. Kamba zilikuwa zimefungwa kengele. Kama mlango ungefunguliwa, kengele ingelia. Mtego wao ulikuwa mzuri, kwani wezi walipoingia bomani kengele ililia na kuwaamsha mbwa wao wanne. Kwa sababu ya kelele za mbwa watoto wa mzee Delo nao waliamka. Laba na Garu hawakujua kama kulikuwa na mtu au mnyama aliyekuwa nje ya boma lao. Lakini waliposikia mlio wa bunduki walijua kwamba kuna mtu karibu na nyumba yao. Walimpiga risasi mbwa mmoja na kufa papo hapo, ndipo walipofanikiwa kuiba magunia ya mahindi na maharagwe.

Laba na Garu walipiga upinde na mishale. Laba alimpiga mtu mmoja mgongoni kwa mshale wa sumu. Walimwona mtu huyu baadaye akiwa mgonjwa mahututi huku watu kutoka kijijini wakiwa wanampeleka hospitali. Pia waliwapiga watu wengine wawili na mishale isiyo na sumu. Mishale hii ilikuwa na utomvu wa ndulele na pilipili. Konkumo na wezi wengine walifikiri kuwa mishale yote ilikuwa na sumu, na waliogopa sana. Walienda haraka kumtafuta daktari ambaye aliweza kuwasaidia

kupata dawa ya kutibu sumu ya mishale, lakini walihitaji daktari ambaye angewafichia siri pia. Konkumo alimjua daktari aliyeitwa Mganga Adili. Wezi wote watatu walimpa Mganga Adili pesa nyingi ili awasaidie.

Baada ya kuwatengenezea chai wezi hawa, daktari alienda moja kwa moja kituo cha polisi. Alijua mishale ilikuwa haina sumu, kwa kuwa wezi waliweza kutembea umbali mrefu. Pia alijua kuwa hawa wlikuwa majambazi ambao ni hatari kwa maisha ya watu. Polisi walimshukuru sana kwa msaada wake. Waliwakamata majambazi wote watatu, na walifurahi kufahamu kuwa mishale ilikuwa haina sumu! Mzee Delo alirudi shambani kwake na kukutana na mkasa ulioikuta familia yake, na kwa kuwa polisi walikuwa wamefika na lori kuja kuwasomba majambazi waliovamia nyumba yake, alilitumia lori hili kubeba mazao yake kuyapeleka sokoni. Msichana Laba alionekana shujaa, kwa kuwa yeye ndiye aliye fyatua upinde na mishale. Inspekta wa polisi alimwambia kwamba siku moja atakuwa askari hodari. Fundisho tunalopata kutokana na hadithi hii ni kuwa jinai hailipi. Ni lazima kuchapa kazi na kutumia akili ili uweze kufaulu. Fundisho jingine ni kuwa maisha ya wanawake wa kisasa yamebadilika sana. Wasichana wanaweza kufanya kazi ambazo mama zao hawakujaribu kuzifanya.



Rebecca Roeder akifundisha wanafunzi wa shule ya msingi

12. HAWALA YA FEDHA (AMANDINA LIHAMBA)

Sarah Smiley

Hawala ya Fedha ni ulinganisho na *The Money Order*, hadithi ambayo iliandikwa na Ousmane Sembene (Msenegal). Mchezo huu wa kuigiza unahusu Ibrahim Chande, mwanaume ambaye anaishi Afrika ya Mashariki. Yeye alipokea barua iliyotumwa kwa mpwa wake anayeitwa Abdul, na anaishi Ulaya. Abdul alimpelekea shilingi elfu mbili. Pesa hizi ni hawala ya fedha, si fedha. Shilingi mia tano ni kwa ajili ya mama yake Abdul, na shilingi elfu moja mia tano ni za Ibrahim kumsaidia matatizo yake kazini. Ibrahim alikuwa na madeni mengi. Watu walipogundua kwamba Ibrahim alikuwa na hawala ya fedha, walifikiri kuwa yeye ni tajiri. Watu wengi walimwomba pesa.

Ibrahim alijaribu kupokea malipo ya hawala ya fedha zake lakini hawazekani kwa sababu hana kitambulisho. Alihitaji uthibithisho wa kuzaliwa ili posta waweze kumlipa pesa zake, lakini hajui mwezi au tarehe gain alizaliwa. Anajua mwaka tu. Bila kujua tarehe kamili ya kuzaliwa wafanyakazi wa posta hawawezi kumsaidia. Ibrahim alienda sehemu ya kupigia picha ili kupata picha yake ya kitambulisho. Alipokuwa hapa, msichana mmoja alimwomba pesa. Ibrahim alisema hana pesa kwa sababu alishalipa pesa tayari. Mwuzaji alikataa kumpa Ibrahim picha zake kwa kuwa Ibrahim alikataa kumlipa gharama ya kupiga picha. Ibrahim alianza kufikiri kwamba Mungu hampendi.

Rafiki yake alikuwa amekasirika kwa sababu Ibrahim hakulipa madeni yake. Ibrahim anaweka rehani hereni za mke wake kama dhamana ya madeni yake. Kulitokea ghasia na uzushi kati ya Ibrahim na mpwa wake kuhusiana na hawala ya fedha, na vitu vingine. Watu walifikiri kuwa Ibrahim ni tajiri hata kama alikuwa hana pesa nyingi. Mwisho inathibitika wazi kuwa Ibrahim ana madeni mengi na alikuwa hana raha hata kidogo.

Hadithi hii inatufundisha kuwa usihesabu kuku kabla vifaranga hawajaanguliwa. Usiamini kila kitu unachosikia. Hata kama Ibrahim ana hawala ya fedha, haina maana kuwa maisha yake ni mazuri au rahisi. Anaweza kuwa na matatizo mengi bado. Ibrahim alijifunza kuwa tunahitaji pesa, lakini pesa si muhimu kuliko familia na furaha.

13. MUHTASARI: SHAMBA LA WANYAMA

Lynsey Farrell

Shamba la Wanyama ni hadithi iliyotungwa na George Orwell mwaka elfu moja mia tisa arobaini na sita. Orwell ni Mwingereza lakini Fortunatus Kawegera alitafsiri kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili mwaka elfu moja mia tisa sitini na saba.

Kitabu hiki kinahusu Shamba la Ibura. Mkulima wa Shamba la Ibura aliitwa Bwana Mtiki. Bwana Mtiki alikuwa mlevi ambaye hakuwatunza wanyama wake. Katika shamba lake kulikuwa na wanyama wengi. Mnyama mmoja, aliitwa Mzee, alikusanya wanyama wote kuwaeleza juu ya mawazo yake. Aliota ndoto kuwa amegeuka nguruwe aliyekuwa tayari kufa. Aliwaeleza wanyama wa Shamba la Ibura kuhusu ndoto yake ya uhuru, na kwamba wanyama wote watapata uhuru. Aliwaambia kuwa binadamu ni adui mkubwa wa wanyama na kwa hiyo walihitaji kuasi. Aliwaita wanyama wote kuwa ndugu na aliwaambia “hapa kuna tatizo tunalopaswa kulisawazisha.” (13) Baada ya mazungumzo aliimba wimbo *Ndugu zangu enyi wanyama*, na wanyama wote walikubali kwamba kulikuwa na tatizo, na tatizo lenyewe lilikuwa binadamu. Siku tatu zilipita na Mzee alifariki. Hata hivyo wanyama walianza kuandaa mapinduzi bila ya uongozi wa mzee.

Kulikuwepo nguruwe wawili, na majina yao waliitwa Mzushi na Mkimwa. Hawa walisaidia kuwakusanya wanyama wote ili kuchochea harakati za mapinduzi. Kwa pamoja waliamua kuwafundisha wanyama kuhusu mpango waliouita Unyama unyama. Walijiandaa kwa muda mfupi kiasi cha miezi mitatu, kabla ya siku ya mapinduzi ilivyokubaliwa, na walifanya mikutano ya siri kila usiku ili wawafundishe wanyama kuhusu harakati za mapinduzi. Baadhi ya wanyama walisita kuunga mkono mikutano hii, lakini nguruwe walisizitiza juu ya wosia na mtazamo wa Mzee kuhusu ukombozi. Waliwaambia wanyama kuwa ni mpango wao ulkuwa mzuri na bora ambao hatima yake ni kupata usawa. Bwana Mtiki alipoteza fedha nyingi baada ya kushindwa mashtaka yaliyomkabili. Alisahau shamba lake na wanyama wake. Wafanyakazi wa shamba hili nao walikuwa wavivu baada ya mkuu wao kutokuwepo shambani. Wanyama waliuona udhaifu wa mkubwa wao. Siku moja, Bwana Mtiki hakuwalisha wanyama na waliamua kumshambulia. Yeye pamoja na wafanyakazi wake walikimbia mbio kutoka shambani.

Baada ya mapinduzi, Mzushi na Mkimwa waliamua kuandika na kuwasomea wnyama wengine Sheria Saba. Sheria kuu ilikuwa “chochote kiendacho kwa miguu minne au chenye mabawa ni ndugu”. Pia, Mzushi alibadili jina la “Shamba la Ibura” na kuliita “Shamba la Wanyama”. Baada ya siku ya mapinduzi wanyama walitaka waishi pamoja na kila mmoja apewe usawa anaostahili. Wanyama walifanya kazi ngumu shambani. Nguruwe waliweza kugundua njia za kutumia vifaa vya binadamu ili wanyama waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Nguruwe waliamua kuwa wanyama wote walihitaji kujifunza kusoma na kuandika. Wanyama wachache waliweza kujifunza, nguruwe waliweza kusoma na kuandika bila dosari. Kwa kweli, nguruwe waliongoza shamba la wanyama vizuri.

Wanyama walioishi nje ya Shamba la Wanyama, nao walibadilika kwa sababu walijisikia huru. Wakulima waliamua kurudi kwenye Shamba la Wanyama. Mtiki alichukua bunduki na wengine walibeba fimbo. Mzushi alisikia kuhusu kurudi kwa binadamu, hivyo aliandaa shambulio

baada ya kusoma kitabu cha vita. Wakulima walianza vita na wanyama, waliokuwa tayari kupigana. Mwenge ulikuwa farasi, pamoja na mzushi walipigana vizuri kuliko wengine. Wao waliitwa ”Mashujaa wa wanyama”. Baada ya kupigana vita kwa muda, wanyama walifanikiwa kumpokonya Bwana Mtiki bunduki yake. Waliamua kupiga bunduki mara mbili kila mwaka kuashiria siku ya Vita Vya Zizi la Ng’ombe na Siku ya Mapinduzi.

Baadaye, Mzushi na Mkimwa waligombana kwa sababu Mzushi alitaka kuleta maendeleo shambani. Lakini, Mkimwa alikuwa na mipango yake mwenyewe. Wanyama walipiga kura kuamua jambo hili, na iliamuliwa kuwa mbwa wapewe kazi ya kumkamata Mzushi. Mzushi aliamua kuondoka shambani. Mkimwa alikuwa kiongozi mpya aliyewatawala mbwa na wanyama wote kwa kuwa walimwogopa.

Maisha shambani yalikuwa mabaya sasa. Mkimwa alikuwa dikteta. Nguruwe na mbwa walianza kuvaa nguo na kuvuta sigara kama wanadamu. Walianza kutembea kwa miguu miwili huku walisema “Wanyama wote ni sawa lakini baadhi yao ni sawa zaidi ya wengine”. Wakulima walikuja shambani kucheza karata. Wanadamu sita na nguruwe sita walikaa mezani. Wanyama waliangalia dirishani na hawakuweza kutofautisha kati ya nguruwe na binadamu.

Mwandishi wa hadithi hii anazungumzia kuhusu siasa na jamii. Alionyesha jinsi mawazo ya ujamaa yalivyokuwa mazuri lakini ujamaa haukufaulu kwa sababu ya vikwazo vingi. Kama alivyofanya Mkimwa, mtu mmoja anaweza kubadili maisha ya watu wengine bila kujali usawa. Mwandishi alizungumzia pia kuhusu historia ya nchi ya Urusi. Mkimwa alifananishwa na Stalin. Kitabu hiki ni muhimu kwa sababu kinaonya kuhusu kuufuata mfumo wa ujamaa kabla ya kuuweka ujamaa katika mtandao mkubwa au mpana.

14. MOTO WA MIANZI (Mwandishi: M.M. Mulokozi)

Kris Leefers

Katika kijiji cha Togasama kulikuwa na mtu mmoja aliyeitwa Mugoha. Usiku mmoja, rafiki wa Mugoha alimtembelea kijijini. Rafiki huyu aliitwa Mpunza na alimwua kamanda wa Wadachi (au Wajerumani) aliyeitwa Nyundo. Mpunza alizungumza na Mugoha kuhusu vita vya Wadachi na kazi muhimu katika mji wa Ikulu. Mugoha alikwenda Ikulu pamoja na jirani yake Nyawelu na mtoto wake Semuganga. Huko Ikulu walizungumza na rafiki aliyeitwa Mupangile. Mupangile ni mtoto wa Mfalme Mkwawa. Kwa sababu ya vita na Wadachi, Mfalme Mkwawa aliamia Kilolo kujificha. Kulikuwa na mtoto wa pili wa Mkwawa aliyeitwa Sapi. Sapi alikaa katika kijiji cha Idegesi. Lengo lao lilikuwa Sapi aungane na Mkwawa huko Kilolo. Mugoha, Nyawelu na Semuganga walikwenda pamoja mpaka Idegesi kumtafuta Sapi walipompata walimteka na kumpeleka hadi Kilolo.

Walifungasha visu, kamba, filimbi za mianzi, vifaa vya kuwashia moto, mavazi, dawa na kadhalika. Walikwenda usiku na walipumzika asubuhi na mchana. Huko Idegesi, walizungumza na chusu ambao walisema kwamba Sapi ni mgonjwa na hawezi kutembea. Tamko la siri la kuingia katika nyumba ya Sapi ni, “Moto wa Mianzi.” Mugoha alinunua punda na Tovi kwa sababu Sapi hakuwezi kutembea. Tovi alikuwa mtu ambaye alikuwa karibu na Sapi. Waliondoka usiku na walisafiri kwa muda wa siku tatu kupitia porini. Msituni walimwona mtu aliyejeruhiwa. Mtu huyu aliitwa Kafugwa na alisema kwamba Tovi alimpiga na aliiba punda wake. Baada ya muda mfupi, Kafugwa alikwenda pamoja na Sapi, Mugoha, Nyawelu na Semuganga.

Karibu na Kipengelo walimtembelea Lwang’a kwa sababu alipigana na Wadachi pia. Siku ya pili walipokuwa Kipengelo kulikuwa na mkutano wa watu na Bwana Mkubwa, Kamanda wa Kidachi, aliyeitwa Sakalani. Sakalani alisema kwamba Mfalme Mkwawa na Sapi ni waovu na alitaka kujua wako wapi. Baadaye, Tovi alifika na kusema kwamba Kafugwa alifanya jambo baya kwani alishafanya kazi na Wadachi. Mugoha alikwenda kumtafuta Kafugwa lakini alikuta alishaondoka. Nyawelu aliondoka pia. Lwang’a, Tovi na Sapi walimtafuta Kafugwa. Hawakuweza kumwona lakini walimwona Nyawelu. Alisema kwamba alimfuata Kafugwa lakini hakuwezi kumsimamisha. Usiku waliondoka na walikwenda mpaka mto wa Ruaha Ndogo. Muda mwingi walikuwa wakiwatoroka Wadachi.

Hata hivyo, siku moja walikunywa pombe nyingi na kulala fofofu. Wadachi walimkamata Mugoha kwa sababu walifikiri kwamba Mugoha alikuwa Sapi. Mugoha alichukuliwa na Wadachi huku wakisema kuwa yeye alikuwa Sapi kwa sababu alitaka kumlinda Sapi. Katika boma la Wadachi Sakalani walijifunza kuwa Mugoha hakuwa Sapi kwa sababu ya habari ya Kafugwa. Baadaye askari wa Wadachi walimkamata Sapi. Siku ya pili Sakalani alisoma amri ya Gavana wa Dar es Salaam. Amri ilisema kwamba Sapi na Mugoha waachiliwe huru. Watu walifurahi. Nyawelu alimwua Kafugwa kwa sababu alikuwa mtu mbaya aliyeshirikiana na wadachi. Sapi na Mugoha walifurahi. Baadaye Sapi alikwenda Kilolo na Mugoha, Nyawelu na Semuganga walirudi nyumbani kwao.



Kris anakunywa Chai saa nne asubuhi


**Kijakazi aliyependwa na Mfalme (Mwandishi: Marcell Lotto)
Shannon Montgomery**

Nilisoma kitabu kinachoitwa Kijakazi aliyependwa na Mfalme. Kitabu hiki kina hadithi sita. Jina la kitabu linatokana na hadithi ya mwisho. Hadithi hii ni kuhusu Mfalme aliyetwa Nino na mke wake, Semiramisi. Mke huyu alikuwa kijakazi, lakini Nino hakujali kwa sababu alipendezwa na uzuri wake. Siku moja Semiramisi alimwuliza Nino kama yeye alimruhusu kuwa malkia wake. Kwa sababu Nino alimpenda sana na alitaka kumfurahisha, yeye alikubali. Semiramisi alitaka kumwonyesha mume wake kwamba yeye aliweza kutawala ufalme. Mfalme Nino alikubali kumruhusu Semiramisi kuwa malkia kwa siku moja. Alipokuwa malkia, Semiramisi aliwaamuru mawaziri na viongozi mbalimbali kukutanika pamoja barazani. Nino aliwaambia kwamba siku hii Semiramisi alikuwa malkia na wao ni lazima wantii. Semiramisi aliwaambia viongozi kwamba jioni kutakuwa karamu na wao ni lazima warudi na wamletee zawadi. Jioni hii viongozi wote walimletea zawadi, ila mmoja. Mfalme Nino alisahau kumletea zawadi. Semiramisi aliamuru kwamba yeye auwawe. Mfalme Nino alikubali kwa sababu yeye alifikiri kwamba Semiramisi alifanyia masihara. Lakini kwa kipigo kimoja, kichwa cha Nino kilianguka chini na Semiramisi alijifanya malkia kweli. Hadithi hii inawafundisha kwamba pendo likizidi hutia kiwi. Vilevile, tunaangalia vijakazi ambao wanataka kulipiza kisasi!

Hadithi ya kwanza inaitwa “Diki atajirishwa na paka”. Katika nchi ya Uingereza alikuwepo kijana aliyeitwa Diki Wittington. Familia yake ilikuwa fukara na hawakuweza kumtunza. Diki alilerewa na bibi kizee mmoja ambaye alimwonea huruma. Diki alipofika umri wa miaka kumi na minne, bibi kizee alikufa. Diki alipenda kusikia habari za London. Yeye aliambiwa kwamba barabara za London zimetwa dhahabu. Pia, yeye alifikiri kwamba watu wote walikuwa tajiri na walikuwa na manifikio. Diki alikwenda London, lakini London ulikuwa tofauti kuliko alioyotazamia. Diki hakuwa na pesa, kwa hivyo yeye alilala kwenye baraza la nyumba ya tajiri. Asubuhi ya pili tajiri huyu, Bwana Fitzwaren alimwona Diki. Yeye alimwonea huruma na alimkaribisha Diki nyumbani kwake. Pale Diki alifanya kazi kupata pesa. Kwa bahati mbaya, Diki hakupendwa na mipshi yule. Vilevile, yeye alikaripiwa Diki sana na kumpa kazi hata asipumzike. Diki alimlaza upenuni penye panya na wadudu. Maisha yake hakufurahi. Siku moja, Diki alinunua paka. Yeye alimpenda sana. Kila siku Alisi ambaye ni binti ya Bwana Fitzwaren, na Diki walicheza na paka wake.

Bwana Fitzwaren alipenda kusafiri. Siku moja, Fitzwaren alipakia merikebu yake bandarini kwenda kufanya biashara nchi za mbali. Kila mmoja alimpa Fitzwaren zawadi kwa safari, ila Diki ambaye hakuwa na fedha wala kitu chochote cha kutoa. Alisi alimridhisha Diki kumpa paka wake kwa sababu merikebu ilikuwa na panya wengi sana na paka wake ni hodari sana kushika panya. Fitzwaren alimshukuru na alimwahidi Diki kumtunza paka.

Merikebu ya Fitzwaren ilisafiri mbali. Bahari ilichafuka sana kwa upepo mkali na alifikia pwani ya Afrika ya Magharibi. Fitzwaren akaona pwani yenye utajiri mkubwa. Mfalme ya nchi hiyo alikuwa mkarimu kwa wageni. Yeye alifanyia karamu kwa wageni. Lakini kabla ya wageni kuanza kula, panya wengi walianza kutoka na kuvishambulia vyakula. Mfalme alikuwa na huzuni na alimwambia Fitzwaren kwamba panya hawa walikuwa wanakuja kila siku kula chakula. Fitzwaren alimwambia Mfalme kuhusu paka wa kuwaua panya. Siku ya pili, Mfalme alitayarisha karamu tena. Mara chakula kiliwekwa mezani, panya wakatoka kama kawaida. Muda huu paka aliwarukia, wengine akiwaua, wengine akiwafukuza. Mfalme alikuwa na furaha sana. Fitzwaren alimwambia kuhusu Diki mwenyewe wa paka. Mfalme akamwonea huruma na Diki. Fitzwaren alimpa watoto wa paka ambao wamezaliwa mle merikebuni. Aliporudi Uingereza, Fitzwaren alimpa Diki zawadi nyingi ambazo alipelekewa na mfalme. Watu wote walifikiri kwamba yeye alistahili kuwa tajiri kwa sababu alikuwa na maisha magumu. Fitzwaren, Diki, na Alisi walikwenda Afrika ya Magharibi. Kule Mfalme alimpa Diki mali nyingi zaidi. Diki alioa Alisi na alirudi Uingereza. Baadye, yeye alikuwa meya wa jiji la London. Watu wote walikuwa na furaha. Ninafikiri, maana ya kitabu ni kwamba watu hawakukata tamaa hata walipokuwa na muda ngumu.

The background image shows a slum area. In the foreground, there is a large, messy pile of garbage, including plastic bags and other debris. In the middle ground, there are several simple, one-story houses with corrugated metal roofs. The houses are surrounded by lush green trees. The sky is clear and blue.

Takataka: Utafiti wa Kwanza kuhusu
Namna ya Kutambua Takataka na Maoni
ya Wakazi waishio Mijini katika Mikoa ya
Kaskazini Nchini Tanzania

na

Charles J. Elfer
Chuo Kikuu cha Georgia

1. UTAMBULISHO

Kama nchi nyingine ye yote duniani, Tanzania na nchi za ukanda wa Afrika ya Mashariki na Afrika kwa ujumla zina matatizo mbalimbali ambayo wananchi na serikali hujaribu kuzungumzia au kuhutubia namna ya kupambana na matatizo yanayowakabili wananchi. Uharibifu wa mazingira ni aina mojawapo ya tatizo ambalo watu wengi wanapenda kulizungumzia. Kwa mfano, nchi nyingi zinazuia kukata misitu ili kuzuia mmononyoko, pia huwashauri wakulima wake kujaribu kuepuka kilimo kisichofaa. Tatizo lingine ambalo watu wachache wanalitaja pia ni tatizo la takataka. Kwa ujumla takataka ni tatizo kubwa, hasa katika miji. Kwa kuwa maendeleo yanaanza kupatikana sehemu nyingi, takataka nazo zinajaa sana kwa sababu wananchi wanatumia vitu vingi kama vile mazao mapya, aina tofauti za vifaa vya ujenzi, ununuzi wa vyakula masokoni na kadhalika. Maendeleo haya yanawafanya watu wengi kubadili tabia zao, na kwa kuwa wanao uwezo wa kujihudumia kwa kujipatia bidhaa au vitu mbalimbali vya kuendeshea maisha yao, takataka nazo zinakuwa nyingi jambo ambalo linaleta matatizo mengi katika sehemu waishizo wananchi hasa sehemu za mijini.

Takataka zinaweza kuleta matatizo na madhara mengi. Kwanza, takataka zinaweza kuharibu afya za wananchi. Takataka zinaleta magonjwa kama vile kipindupindu, kuhara damu, na amiba. Mahali pachafu panaleta mkusanyiko wa mbu na hata mbwa mwitu. Tunajua kwamba mbu ni hatari kwa sababu wanaleta ugonjwa wa malaria. Mbu wanapenda mahali palipo na mkuasnyiko wa takataka kwa sababu ni rahisi kuzaana katika sehemu kama hizi.

Takataka zinaweza kuleta afya mbaya kwa binadamu na wanyama pia. Kwa mfano, ng'ombe na mbuzi wanapokula vitu vichafu ni dhahiri kuwa watakuwa wagonjwa na inawezekana wakafa. Wanyama kama hawa wanapokula vitu kama mifuko ya plastiki ni wazi kuwa wataathirika kiafya kwani matumbo yao hayawezi kulainisha vitu vigumu kama mifuko ya plastiki. Hii ni dhahiri kuwa watakufa na kumletea mfugaji huzuni na hasara katika mradi wake.

Takataka zinaweza kudhuru kulimo pia. Kemikali kutoka viwandani zinaweza kuharibu udongo na maji. Bila udongo mzuri na maji safi, kulima na kupata mazao mazuri itakuwa vigumu. Mifuko ya plastiki ni tatitizo kwa kilimo pia. Mifuko ya plastiki inapofunikwa chini ya udongo inazuia maji kusambaa katika ardhi na hivyo huzuia miti na maua kuota vema.

Pia takataka zinaweza kuleta matatizo kwa uchumi wa nchi au manispaa. Kupambana na tatizo la takataka nchini au katika manispaa ni jambo linalohitaji kutumia pesa. Ni kweli kwamba kuondoa takataka ni ghali sana, lakini maisha ya mwanadamu yanahitaji usafi jambo ambalo ni muhimu katika kutunza afya yake. Kutokushughulikia takataka ni kosa kubwa kwa sababu matatizo yanayotokana na takataka ni mengi, yenye usumbufu, na hatari nyingi. Kukabili tatizo la takataka linahitaji menejimenti nzuri kwa kuwa bila usimamizi mzuri wa namna ya kukabiliana na takataka; matatizo makubwa yanaweza kuikabili jamii ikiwa ni pamoja na gharama kubwa za kuwahudumia wananchi yapojitokeza magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu au kuharisha damu. Kulifanyia mzaha tatizo la takataka kutaliletea menejimenti yeyote matatizo makubwa ikiwa ni pamoja na kutafuta nyongeza ya pesa za kugharamia matatizo yatakayoletwa na takataka, na matumizi ya pesa hizi za wananchi yangeweza kuepukwa na kutumiwa kwa shughuli nyingine za maendeleo.

Bila kuwa na menejimenti nzuri, takataka itakuwa tatizo kubwa kwa jamii hata wakati ujao. Menejimenti nzuri inategemea elimu. Inategemea elimu kwa sababu takataka inahusishwa na utamaduni. Kila mtu ana maoni tofauti kuhusu takataka. Inavyoonekana kimtazamo *takataka kwa mtu mmoja ni uchafu usiokuwa na nafasi katika maisha yake ili hali kwa mtu mwingine takataka ni dhahabu*. Ni vema kuwa na programu inayozungumzia tatizo la takataka, na ni vema ikaihusisha menejimenti yeyote ile katika miji au manispaa ili kuwa na mtazamo na maoni yanayofanana kuhusu tatizo la takataka.



Charles anafundisha hesabu

MIBINU

Nimeanza utafiti kuhusu tatizo la takataka katika kanda ya Afrika ya Mashariki. Ninajaribu pia kujifunza kuhusu maoni na namna ya kuwafanya wananchi kufahamu na kutambua tatizo la takataka. Nilifika Tanzania mwezi wa tano kabla ya kuanza masomo katika chuo cha MS-TCDC. Nilikaa katika mji wa Moshi karibu na Mlima Kilimanjaro.

Kujifunza kuhusu maoni ya watu kuhusu tatizo la takataka nilitumia mbinu nyingi. Nilifikiri kutumia elimu na kazi kuwa ndiyo mbinu yangu ya kukusanya maoni. Hivyo niligawa vikundi vinne katika sehemu hizi mbili. Kikundi cha kwanza kilikuwa cha watu ambao walikuwa hawana elimu ya sekondari na walikuwa hawafanyi kazi katika sekta ya utalii. Kikundi cha pili kilikuwa cha watu ambao walikuwa hawana elimu ya sekondari lakini walikuwa wanafanya kazi katika sekta ya utalii. Kikundi la tatu ni cha watu ambayo walimaliza kitado cha nne na walikuwa wanafanya kazi katika sekta ya utali. Kikundi la nne ni watu ambayo walimaliza kidato cha nne na hawafanyi kazi katika sekta ya utali.

Nilizungumza na watu thelatini na mbili wakati nilipoanaza sehemu ya pili ya utafiti huu. Nilizungumza na watu wanane katika kila kikundi. Mahojiano yote nimeyarekodi katika kinasa sauti changu kidogo, na nitakaporudi Marekani nitatafsiri maelezo yote yaliyopo katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Baada ya kumaliza mahokijiano haya, nilifanya mahojiano mengine na niliwauliza watu wengine thelathini na mbili. Nilitumia vikundi kama nilivyovitaja hapo juu. Kabla sijafika MS-TCDC nilikwishazungumza na watu sitini na nne. Labda watu sitini na nne hawatoshi, lakini ninafikiri kwa kuwa ulikuwa ni utafiti wa mwanzo nadhani mambo bado ni mazuri tu.

HITIMISHO

Sikuja Tanzania kuwaambia wananchi kwamba wana matatizo. Ninafikiri Watanzania wanao uwezo wa kusema kama wana matatizo. Hata hivyo, ninajua kwamba nchi hii ina wakaaji wengi hasa katika miji yake. Kama watu wengi wataendelea kuhamia mijini, tatizo la takataka na la uharibifu wa mazingira yataendelea kuwa matatizo makubwa kwa nchi hii. Kuweza kuzuia matatizo haya, zinahitajika mbinu bora za kuwaelezea wananchi ni hasara gani, na matatizo gani yatakayowakumba kama hawakushughulikia tatizo la takataka na tatizo la uharibifu wa mazingira. Menejimenti zote hasa zile za mjini zinahitaji kubuni mbinu za kupambana na tatizo la takataka ambalo linaongezeka siku hadi siku. Ufumbuzi wa matatizo haya yatapatikana tu pale wananchi watakapoelimishwa na kueleweshwa nini hasa hasara za kutokumiliki takataka zao, na kubwa zaidi ni mateso kiasi gani wananchi watapata kama hawakuzuia uharibifu wa mazingira ambao kwa sasa unaonekana kuvuka mipaka. Ni jukumu la wananchi kulinda na kuweka mzingira yao katika hali ya usafi. Ni vema

wananchi wote wakakumbuka kuwa mvunja nchi ni mwananchi, na mjenga nchi ni mwananchi pia. Ni vema kutambua matatizo haya mapema na kuyatafutia ufumbuzi wa kudumu.

2. BAADA YA MIAKA AROBAINI: MAWAZO JUU YA UJAMAA

Jo Tague

Wanafunzi wengi wanasoma kuhusu sera ya Ujamaa nchini Marekani lakini wanafunzi na walimu wana matatizo makubwa ya kuielewa na kuifanyia kazi historia kuhusu Ujamaa. Wanafunzi wengi wanaweza kujifunza vitendo au matokeo juu ya sera ya hii ya Ujamaa lakini inawapa shida sana kuielewa. Kwa sababu hii ndiyo maana hapa nchini Tanzania wanahistoria wanahitaji kujifunza juu ya kumbukumbu ya sera hii na nini matokeo yake yalikuwa kwa nchi changa kama Tanzania. Kwa mtazamo wa karibu, watu wengi duniani wanaelewa kuhusu sera ya Ujamaa. Wanafahamu kwamba serekali ilikubali tamko la azimio la Arusha lililopitishwa mwaka elfu moja mia tisa sitini na saba. Azimio hili na hasa Mwalimu Nyerere alitaka watu wa Tanzania wajitegemee. Alitaka nafasi sawa kwa kila mtu, alitaka maendeleo katika maeneo ya mashambani, na alitaka kuboresha elimu. Zaidi ya hayo, Mwalimu Nyerere alijaribu kuanzisha Vijiji vya Ujamaa ili watu waweza kufanya kazi pamoja na kwa kushirikiana. Mwalimu Nyerere alitaka watu walioishi katika Vijiji vya Ujamaa kufanya kazi ya kilimo pamoja yaani kulima kwa jumua. Makala ya Azimio la Arusha ilihusu maendeleo ya Tanzania. Lakini, mambo haya yamekuwa kama habari au taarifa tu. Mara nyingi, watu wanasahau kwamba historia inahusu zaidi maoni. Pia historia ina maoni ambayo yanabadilika baada ya miaka kadhaa. Historia ni nzuri kwa sababu kama mtu angependa kusoma kuhusu sera ya Ujamaa baada ya miaka arobaini angeliweza kutumia wazo kama hili. Duniani watu wanatoa maana tofauti kuhusu sera ya Ujamaa lakini hapa Tanzania, ningependa kufahamu kwa nini watu wengi wana kumbukumbu tofauti juu ya sera ya Ujamaa.

Kwa kawaida nchini Marekani, wanafunzi wanasoma juu ya mawazo ya walimu wao kuhusu sera ya Ujamaa. Kwa sababu hii, ni muhimu kusoma na kufanya utafiti kuhusu mawazo ya Watanzania wanapokumbuka enzi ya Ujamaa. Kufanya utafiti wa aina hii niliongea na watu kumi, hapa MS-TCDC, wazazi wangu, na watu mbalimbali mjini Arusha. Waliniambia mambo mengi tofauti yanayohusiana na enzi za Ujamaa. Wengi nilioongea nao wanakiri wazi kuwa hawakuishi katika Vijiji vya Ujamaa. Wengi wanakiri kuwa sera hii haikufanikiwa, lakini Watanzania wote wanaendelea kuonyesha kiburi chao kwa kuwa walijaribu sera hii. Nafikiri hii ni muhimu kwa sababu, nchini Marekani, tunasikia habari mbaya tu juu ya matokeo ya sera za Ujamaa. Lakini, Watanzania wengi wanaendelea kuamini kuwa sera hii ilifaulu katika vijiji vingi pia. Lakini watu nilozungumza nao wanatofautiana juu ya maana ya sera ya Ujamaa. Wengine waliniambia kwamba

wakati wa Ujamaa walifikiri maana ya Ujamaa ilikuwa kuishi pamoja katika Vijiji vya Ujamaa. Watu wengine walifikiri kwamba serikali ilitaka nchi ya Tanzania kuwa bila tabaka. Kila mtu alinipa maoni tofauti kuhusu nini maana ya Ujamaa.

Katika insha hii, ningependa kuelezea mazungumzo maalum niliyofanya na mwanaume fulani mjini Arusha. Niliongea naye juu ya matatizo ya Ujamaa. Aliniambia kwamba tatizo kubwa kuhusu sera ya Ujamaa lilikuwa mawasiliano. Kila mtu katika vijiji vilivyoanzishwa alikuwa na uwezo tofauti wa kupata habari kuhusu sera ya Ujamaa. Wakati wa Ujamaa, kulikuwa na namna nyingi za mawasiliano. Watu wengi walikuwa na marafiki fulanifulani ambao walifanya kazi serikalini. Watu wengine walisoma magazeti, au wengine walisikiliza redio. Aidha, watu walio wengi walisikia juu ya sera za Ujamaa kutoka watu wengine. Watanzania wengi walijifunza kuhusu sera ya Ujamaa kwa mdomo. Walimu wengi nchini Marekani wamesoma juu ya matatizo ya mawasiliano wakati wa Ujamaa. Lakini, ninafikiri ni muhimu kusoma mabadiliko na kumbukumbu za leo kwa sababu ya aina nyingi za mawasiliano zilizokwisha kujitokeza miaka arobaini iliyopita. Wanahistoria wanahitaji kusoma umuhimu wa mawasiliano wakati wa Ujamaa na aina gain ya mawazo yaliyopo kuhusu Ujamaa mwaka huu wa elfu mbili na nne.

Kwa sababu ya mawasiliano haya, watu wengi walikuwa na mawazo potofu juu ya maana na sera ya Ujamaa. Zaidi ya hayo, wengi walikuwa na wamepotoshwa juu wazo la Ujamaa na matendo yalitokana na sera ya Ujamaa. Ninafikiri ni muhimu kusikia sauti na maoni tofauti kama mwanaume niliyezungumza naye.



Joanna anafundisha

Masomo ya historia yanahitaji watu ambao wanaweza kutoa hadithi zao. Mimi ninaogopa kuwa kizazi hiki kitapotea kabla ya kuweza kutoa maoni yao kuhusu Ujamaa. Pia nilijifunza kuwa historia ni juu ya maoni ya mambo tofauti. Historia siyo tu juu ya habari, matendo au matokeo bali ni mchanganuo wa mambo yaliyopita, yaliyopo, na yatakayokuja. Hii imethibitika wazi baada ya miaka arobaini, mawazo kuhusu sera ya Ujamaa bado yamebaki kuwa tofauti kwa kila mtanzania. Wanahistoria wanahitaji kuwauliza watu waojua juu ya mambo fulani juu ya uzoefu wao. Ingawaje miaka arobaini imepita lakini kila mtu ana mawazo tofauti kuhusu maana ya Ujamaa, na kila mtu anakumbuka nyakati hizi kwa matukio mbalimbali.

3. ELIMU KATIKA TANZANIA **Sarah Smiley**

Mradi wangu unahusu jiografia katika shule za msingi za Tanzania kwa sababu ninasoma jiografia katika Chuo Kikuu cha Kansas. Nimesoma jiografia kwa muda mrefu na ninaipenda sana. Ninapoingia duka la vitabu, hununua vitabu vya jiografia kila mara. Niliweza kununua vitabu vitano nchini Tanzania na nilivipenda vitabu hivi sana! Nilishangaa kuhusu masomo mengine katika vitabu kwa hivyo niliamua kusoma vitabu hivi pia.

ELIMU KATIKA TANZANIA

Kuna matatizo mengi katika elimu nchini Tanzania. Serikali ya Tanzania ingependa watoto wote kuhudhuria shule ya msingi lakini nusu tu ya watoto wanaweza kumaliza shule za msingi. Hata kama watoto wengine wanaweza kumaliza shule, wengi hawajifunzi sana kwa sababu hakuna vifaa vya kutosha kama vitabu, ramani, viti, na meza. Tatizo lingine linahusu walimu. Hakuna walimu wa kutosha na walimu wengine hawajahitimu chuo kikuu, kwa hivyo hawana ujuzi wa kutosha kufundisha wanafunzi wao. Serikali ya Tanzania imejitahidi kuboresha elimu, lakini bado kuna kazi kubwa ya kufanya.

JIOGRAFIA

Kuna aina tatu za jiografia: watu, ardhi, na mbinu za komputa. Jiografia ya watu inahusu utamaduni, lugha, dini, muziki, fasihi, miji, vijiji, siasa, sanaa, na uchumi. Jiografia ya ardhi inahusu mazingira, milima, bahari, udongo, mawe na mito. Jiografia ya mbinu za komputa inahusu ramani na kuchora ramani. Hapa Afrika, watu wanasoma jiografia za watu na ardhi zaidi kuliko jiografia ya

mbinu za komputa kwa sababu hakuna pesa au vifaa vya kusoma somo hili. Badala yake, Waafrika wanakuja Marekani kusoma somo hili.

VITABU VYANGU

Nimenunua vitabu vitatu vya jiografia kwa wanafunzi wa shule za msingi. Vitabu hivi viliandikwa na Wizara ya Elimu lakini vitabu ni vizee. Kitabu cha darasa la tano kiliandikwa mwaka 1977 na vitabu vya darasa ya sita na saba viliandikwa mwaka 1981. Hata kama jiografia haibadiliki sana, vitabu hivi havifai. Vitabu vinatumia majina ya makosa kama Zaire, Ujerumani Magharibi, na Burma. Kama walimu hawajui majina mapya, wanafunzi watakuwa na matatizo katika shule za sekondari na chuo kikuu. Pia, nimenunua atlas mbili. Atlas moja iliidhinishwa na Wizara ya Elimu na atlas nyingine haikuidhinishwa.

DARASA LA TANO

Kitabu hiki kinachoitwa *Wafanyakazi wa Afrika*. Kina sura kumi na sita. Sura ya kwanza inahusu dunia na ulimwengu. Sura ya pili inahusu bara la Afrika. Sura nyingine zinahusu nchi fulani. Kila sura inahusu historia ya nchi na mazao ambayo yanapandwa pale. Masomo yanazungumzia Burundi (Buni), Sudan (Pamba), Malawi (Chai), Zimbabwe (Tumbaku na Makaa), Liberia (Mpira na Chuma), Ghana (Kakao), Nigeria (Chikichi na Bati), Gambia (Karanga), Visiwa vya Kanari (Ndizi), Afrika ya Kusini (Kondoo na Dhahabu), Zambia (Shaba), Zaire (Almasi), na Libya (Mafuta). Sura ya mwisho inahusu uchukuzi na usafirishaji.

DARASA LA SITA

Kitabu hiki kinaitwa *Wafanyakazi wa Ulimwengu*. Kina sura ishirini na moja. Sura ya kwanza inahusu longitudo na latitudo. Sura ya pili inahusu dunia. Sura ya tatu inahusu hali ya hewa. Sura nyingine zinahusu nchi fulani. Kila sura inahusu historia ya nchi na sekta zao za uchumi. Masomo yanazungumzia Sri Lanka (Kilimo cha Chai), Marekani (Kilimo cha Mahindi), Malaya (Kilimo cha Mpira), Italia (Kilimo cha Matunda), Burma (Kilimo cha Mpunga), Canada (Kilimo cha Ngano), Brazil (Kilimo cha Buni), Cuba (Kilimo cha Miwa), India (Kilimo cha Pamba), Jamaica (Kilimo cha Migomba), Australia (Ufugaji wa Kondoo), Denmark (Ufugaji wa Ng'ombe), Canada (Upasuaji wa Mbao), Norway (Uvuvi wa Samaki), Kuwait (Uchimbaji wa Mafuta), Japan (Utengenezaji wa Meli), na Ujerumani Magharibi (Utengenezaji wa Motokaa). Sura ya mwisho inahusu biashara na usafirishaji.

DARASA LA SABA

Kitabu hiki kinaitwa *Wafanyakazi wa Afrika Mashariki*. Kina sura kumi na sita. Sura ya kwanza inahusu kipimio cha ramani. Sura ya pili inahusu ramani za kontua. Sura ya tatu inahusu nchi, uoto wa asili, na mgawanyiko wa watu wa Afrika ya Mashariki. Sura ya nne inahusu kilimo cha mazao ya biashara ya Kenya, Uganda, na Tanzania. Sura ya tano inahusu uchimbaji wa madini katika nchi hizi tatu. Sura ya sita inahusu viwanda katika nchi za Afrika ya Mashariki. Sura ya saba inahusu hifadhi za taifa katika Afrika Mashariki. Sura nyingine zinahusu Tanzania tu. Zinzungumzia nchi kuhusu kilimo, misitu, ufugaji wa myuki, uchimbaji wa madini, viwanda, vyama vya ushirika na biashara, na njia za usafiri. Sura ya mwisho inahusu majirani wa Tanzania.

ATLASI

Kila atlasi iliandikwa na waandishi tofauti lakini zote ni nzuri sana. Zina ramani nyingi, picha nyingi, insha nyingi, na grafu na chati tofautitofauti. Kuna maelezo kuhusu serikali ya Tanzania, maendelo, historia, mazingira, na urari wa biashara. Atlasi ni kamili lakini bei zake ni ghali zaidi kuliko vitabu vingine. Nchini Marekani, atlasi ni ghali pia kwa hivyo watu wengi hawana atlasi. Badala yake watu wengine wanatumia ramani za komputa.

TOFAUTI KATI YATANZANIA NA MAREKANI

Elimu ya jiografia ya Tanzania ni tofauti sana ukilinganisha na elimu ya jiografia ya Marekani. Wanafunzi wa Marekani wana vifaa vingi kama vitabu, karatasi, ramani, kalamu, filamu, tufe za dunia, na komputa. Walimu wa Marekani wanasoma elimu katika chuo kikuu na wanajua kuhusu kufundisha. Bado, elimu ya Marekani ina matatizo. Jiografia inafundishwa kwa shule za msingi, shule za sekondari, na chuo kikuu lakini wanafunzi hawajifunzi sana. Madarasani walimu wengi wanafundisha majina ya mahali tu badala ya kufundisha kuhusu mahali. Kwa Tanzania, vitabu vya jiografia vinafundisha kuhusu mahali. Wanafunzi wanajifunza mahali pako wapi, historia ya mahali, na vitu ambavyo vinafanya sehemu moja kuwa tofauti na sehemu nyingine.

Wanafunzi wa shule za msingi za Tanzania wanajifunza masomo ambayo nilijifunza katika chuo kikuu. Niliposoma jiografia ya ardhi, nilijifunza kuhusu hali ya hewa, latitudo na longitudo, aina za ramani, dira ya dunia, na mzunguko wa jua na dunia. Kabla ya chuo kikuu, nilikuwa sijawahi kujifunza vitu hivi. Nilishangaa kuona watoto wa Tanzania wanajifunza kuhusu masomo haya katika shule ya msingi. Masomo haya ni mazuri na ngumu. Kwa kawaida, masomo katika shule za msingi za Marekani ni rahisi na wanafunzi hawakumbuki sana.

Nilishangaa kuona wanafunzi wanajifunza kuhusu usafiri. Vitabu vyote vina sura ya usafiri. Kwa Marekani, hakuna wanajiografia wengi ambao wanafanya utafiti kuhusu usafiri. Vitabu hivi vina karasa sawasawa katika viwanda na kulimo. Kwa kawaida, vitabu kuhusu Afrika vinahusu

kulimo tu. Vinapohusu viwanda, mazulio ni mabaya. Kwa mafano, nilijifunza kuhusu matatizo ya viwanda vya nguo vya Tanzania. Sijawahi kujifunza kuhusu nguo za Urafiki.

Sijui kama shule zote zinatumia vitabu hivi. Nilipofundisha shule ya msingi, sikuona vitabu. Wanafunzi wengi hawakuwa na karatasi au kalamu kwa hivyo sidhani kama wao wana vitabu. Bila vitabu hivi, walimu hawawezi kufundisha kuhusu masomo haya. Wanafunzi wanahitaji kuona ramani na picha na kufanya mazoezi. Kila sura ina mazoezi ambayo yanawasaidia wanafunzi kujifunza na kumbuka masomo.

KUFUNDISHA

Mimi na wanafunzi wengine tulifundisha katika shule ya msingi karibu na TCDC. Shule hii inafundisha jiografia katika darasa la tatu. Natasha, mwanafunzi mwengine, alifundisha jiografia ya dunia katika darasa la tatu. Darasa lake halikufundishwa jiografia bado kwa hivyo wanafunzi hawakujua kitu cho chote kuhusu jiografia. Darasa lina ramani lakini ramani ilichorwa kwa mkono. Natasha alifundisha jiografia ya dunia katika darasa la nne pia. Wanafunzi hawa walijua sana dunia. Walijua namba ya mabara na bahari na waliweza kutambua Tanzania katika ramani ya Afrika. Darasa halikuwa na ramani. Nilifundisha jiografia ya Afrika katika darasa la nne. Nilishangaa kwamba wanafunzi walijua kuhusu bara lao. Walijua majina ya nchi zote. Walijua tofauti kati ya kusini na kazkazini na mashariki na magharibi. Walijua bahari, milima, mito, na majangwa pia. Darasa halikuwa na ramani. Kuna matatizo kuhusu elimu ya jiografia nchini Tanzania lakini wanafunzi wanaweza kujifunza mazulio mengi.

Vitabu Ambavyo Nilitumia

Atlasi kwa Shule za Msingi Tanzania. 2000. Macmillan Aidan: Dar es Salaam.

Atlasi ya Maarifa ya Jamii kwa Shule za Msingi. 1997. Ben and Company Limited: Dar es Salaam.

KULEANA. 1999. *The State of Education in Tanzania: Crisis and Opportunity.*

KULEANA: Mwanza.

Wizara ya Elimu. 1981. *Wafanyakazi wa Afrika Mashariki.* Dar es Salaam.

Wizara ya Elimu. 1981. *Wafanyakazi wa Ulimwengu.* Dar es Salaam.

Wizara ya Elimu. 1977. *Wafanyakazi ya Afrika.* Dar es Salaam.

4. MRADI WA MWISHO

KISWAHILI KAMA SOMO NA MADA KATIKA KIWANGO CHA CHUO KIKUU

Anna Rhea Lewandowski

Tangu nilipofika hapa Tanzania, nimeongea na wataanzania na watu wa nchi nyingine mbalimbali. Kwangu, ni muhimu sana kusoma lugha na fasihi pamoja. Mambo kama utamaduni, siasa, maendeleo na historia huletwa na lugha. Kutokana na sababu hii mimi nasoma lugha na fasihi

katika idara ya lugha za kiafrika. Hata nchini Marekani kuna utata kati ya maelezo ya fasihi na lugha, lakini watu wengi wameanza kuamini kwamba kujifunza lugha kunahusu fasihi na lugha pia. Hapa Tanzania nimesikiliza maoni kuhusu Kiswahili katika kiwango cha chuo kikuu. Nimesikitishwa kidogo kuona kwamba watu wengi niliokutana nao hawakujua juu ya nafasi ya kusoma Kiswahili hapa Tanzania au huko Marekani.

Mara nyingi nilipokutana na watu, swali la kwanza walilioniuliza lilihusu elimu yangu. Walitaka kujua kwa nini ninasoma Kiswahili hapa Tanzania. Mimi huwajibu kwamba kwa sasa nasoma Kiswahili katika Kituo cha TCDC, lakini nilikuwa nimeshasoma tena kiswahili huko nchini Marekani kwa muda wa miaka mitatu kabla ya kuja Tanzania. Pia walishangaa kwa nini sisomi juu ya maendeleo au mazingira. Waliniuliza pia kwa kusoma Kiswahili kama nitaweza kufanya kazi za maendeleo mjini Arusha. Bila shaka watu wengi wanafahamu kuwa wanafunzi walipo katika chuo cha TCDC wasoma mambo yanayohusu maendeleo na kwa kusikia tunasoma kiswahili wanashangaa sana.

Aidha wengi hawakujua kwamba sisi Wamarekani tunaweza kujifunza Kiswahili au kusoma masomo ya kiafrika. Nilipoeleza kwamba ninasoma lugha ya Kiswahili waliniuliza nimekwisha kaa Tanzania kwa muda gani. Wazo la kusoma Kiswahili nje ya Afrika ni jipya. Wengi wanaamini kwamba ninasoma Kiswahili kwa sababu labda kuna Waswahili wengi katika jimbo langu nchini Marekani. Mimi niliwaeleza kwamba walimu wangu wawili katika chuo kikuu ninachosoma wamefanya GPA na wamejifunza Kiswahili ili waweze kufundisha Kiswahili nchini Marekani. Bado wengi walitaka kujua nani anasoma Kiswahili na kwa nini. Kwa kuwajibu niliwaelezea kuwa kuna vikundi vinne vya wanafunzi wanaosoma Kiswahili. Kundi la kwanza ni la wanafunzi wanaotaka kumaliza mahitaji (yaani kukamilisha miaka miwili ya lugha), kundi la pili ni lile la wanafunzi wanaojihusisha na waafrika (yaani “heritage learners”), kundi la tatu ni lile la wanafunzi wanaotaka kufanya kazi Afrika, na kundi la nne ni lile la wanafunzi wanaotaka kueneza elimu ya Afrika sehemu mbalimbali duniani.

Baada ya kuelewa kwamba kuna nia nzuri kwa Wamarekani kusoma Kiswahili, pia walitaka kujua walimu wanafundishaje Kiswahili wanapokuwa nchini Marekani? Wengi hawakuwa na habari kuwa kuna vifaa vingi vya kufundishia kiswahili nchini Marekani. Kuna vitu kama vile: mtandao, filamu, redio, n.k. Kweli ni rahisi kujifunza na kufundisha Kiswahili kuliko lugha nyingine za kiafrika kwa sababu watu wengi wameshasoma na kuandika vitabu au kufanya utafiti juu ya kiswahili. Mara chache watu walinigundua kuwa ninasoma Kiswahili nchini Marekani lakini wengi walihisi huenda ninasoma isimu tu. Hata nchini Marekani kama nikitamka kuwa ninasoma na nina uwezo wa kuzungumza lugha zaidi ya tatu, wanaamini ninasoma isimu tu.

Hata hivyo nimegundua kwamba watu wengi hawajui kama wanaweza kusoma Kiswahili hapa Tanzania katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Nilipotaja shule au taasisi za Kiswahili huko Dar, mtu mmoja alisema “Umekosea. Ulitaka kuniambia kwamba unaweza kusoma Kiingereza- si Kiswahili”. Hakuniamini. Nilizungumza na watu wengine walioniambia kwamba hakuna sababu au faida ya kusoma Kiswahili.

Mambo haya yalinihuzunisha sana. Sijakutana na mtu ye yote (isipokuwa walimu wanaofundisha hapa) anayependa kusoma Kiswahili kama lugha, kama fasihi au vyote kwa pamoja. Hata nilipoenda kwenye maduka ya vitabu, nilishangaa kuona vitabu vilivyoandikwa kwa Kiswahili ni vichache mno. Ningependa kuona vitabu vingi vitokavyo Afrika- hata kama ni vya waandishi wasioweza kusema Kiingereza. Ninafikiri kuna upungufu wa elimu inayohusu fasihi katika vyuo vikuu.

Kuna sababu nyingi zinazosababisha tatizo hili. Kwanza nilikukutana na watu wasiojua kuhusu viwango vya elimu ya juu au wenyewe kutokuwa na viwango vya elimu ya kutosha. Au mara nyingine hata kama wameelimishwa, watu wa hapa Arusha wanafanya kazi zinzohusu mazingira na maendeleo zaidi. Milima inawavutia watalii wengi kwa hivyo mazingira ni muhimu sana. Pia, kwa sababu kuna vikundi vingi vinavyosoma kuhusu maendeleo hapa kituo cha TCDC, wananchi wamezoea kukutana na wana maendeleo wanaokuja chuoni.

Sababu ya pili ya kuona Kiswahili kama mada isiyo muhimu inahusu lugha nyingine nchini. Siku hizi watu wengi wanatilia mkazo elimu ya kiingereza badala ya Kiswahili. Sababu nyingine iliyo karibu na hii ni kuhusu elimu. Kuna tofauti kubwa baina ya elimu inayotolewa nchini Marekani na ile inayotolewa nchini Tanzania. Nchini Marekani ni rahisi kupata elimu. Hata kama huwezi kulipa ada za shule, unaweza kupata pesa kutoka serikalini na kuzirejesha baadaye. Nchini Tanzania ni vigumu sana kutafuta ada ya kulipia masomo na wakati huohuo kuendelea kusoma. Watu wengi wana nafasi ya namna moja tu, au kusoma au kufanya kazi. Watu wanapokuwa shuleni huchagua kusoma mada itakayowapa kazi na pesa kwa haraka. Kwa mfano, watu wengi wanasoma kompyuta au biashara. Labda hawapendi masomo haya lakini wanajifunza kwa sababu wanaamini watapata kazi zitakazowalipa fedha kwa haraka. Nchini Marekani ni tofauti. Wanafunzi wana uhuru kuchagua kusoma nini na kwa nini. Kwangu, naweza kusoma fasihi na lugha za Afrika kwa sababu zinanivutia. Sina wasiwasi mkubwa juu ya maisha yangu ya baadaye.

Ningependa kuona upanuzi katika kufundisha fasihi (zinazohusu fasihi andishi na fasihi simulizi) pamoja na masomo mengine ya lugha ya Kiswahili. Labda wakati ujao ingefaa kupendekeza wanaofundisha masomo ya lugha walipwe zaidi ili kuwavutia watu wengine kujiunga na kazi ya ualimu. Baada ya kufanya mradi huu, ningependa kuendelea kutofautisha utamaduni wa Tanzania na

Afrika nzima wa kutokujua ubora na umuhimu wa fasihi kama somo lililo rasmi sehemu nyingi duniani.

5. LUGHA KATIKA TANZANIA

Rebecca Roeder

Nilizungumza kuhusu lugha nchini Tanzania na watu wachache katika mikoa ya Arusha na Dar, na nilisoma magazeti pia. Mada hii inanivutia kwa sababu hali ya lugha nchini Tanzania inabadilika. Ninaweza kuzungumza kuhusu mada tatu—lugha za makabila, Kiswahili, na Kiingereza. Inaonekana kwamba lugha za makabila zinapungua nchini Tanzania. Sababu kubwa ni siasa. Mwalimu Nyerere alipokuwa rais, aliwaambia Watanzania kwamba umoja ni muhimu katika kuyaunganisha makabila yote nchini Tanzania. Alisema kwamba ni vema kufikiri kama nchi moja, si kama makabila mengi. Kwa hivyo, kwa miaka arobaini uliyopita, Watanzania wameamini kuwa umoja na amani kati ya makabila yao ndiyo silaha yao ya maendeleo. Sasa, wengi wanaoana kutoka makabila tofauti. Mara kwa mara, wanazungumza lugha ya Kiswahili, kama lugha ya wote, na watoto wao hawasomeshwi kwa lugha au utamaduni wa wazazi wao. Mwalimu Ndosi aliniambia kwamba mabadaliko haya ya ndoa, kwa kweli, yametukia kama miaka ishirini uliyopita hivi.

Kwa hivyo, Kiswahili kimegeuka kuwa lugha ya watu wote nchini Tanzania. Ingawa watu wa Uganda na watu wa Kenya wanasema Kiswahili pia, Kiswahili ni muhimu nchini Tanzania kuliko katika nchi hizi zingine, kwa sababu mbalimbali za kihistoria na kisiasa. Kiswahili pia ni lugha ya umoja kwa Afrika ya Mashariki na kinakua. Kwa mfano, baba yangu hapa Arusha alinisomesha neno *luninga* kwa *televisheni*. Mwalimu Ndosi aliniambia kwamba ni muhimu kutafuta maneno mapya ya Kiswahili kwa sababu Kiswahili kinakua kama lugha ya umoja. Kwa mfano mwaka huu kiongozi mmoja kutoka *Umoja wa Afrika* alitoa hotuba kwa kiswahili, ingawaje viongozi wengi kwenye mkutano huu hawakuweza kumwelewa.

Kwa kweli Kiswahili ni lugha muhimu sana nchini Tanzania. Lakini, Kiingereza nacho ni lugha muhimu pia. Nilisoma katika gazeti kwamba karibu asilimia themanini hivi ya Watanzania wanaamini kwamba watoto wanahitaji kusema Kiingereza na kukifaulu mashuleni. Sidhani kama kuna ushindani kati ya Kiswahili na Kiingereza. Inaonekana kwamba kila lugha ina ari fulani. Kiswahili ni lugha ya taifa, lakini Kiingereza ni lugha ya kimataifa iliyo na nafasi duniani kote. Kwa urasmi, masomo katika elimu ya sekondari, na elimu katika vyuo vikuu, isipokuwa masomo ya utamaduni na lugha, yanafundishwa kwa lugha ya kwa Kiingereza tu. Aidha, mara kwa mara, ni muhimu kusema Kiingereza kwa sababu ya kazi, siasa na hasa mambo yanayohusu nchi za nje. Watanzania wengi wanapenda kuzungumza Kiingereza.

Lakini, kuna matatizo yanayojitokeza katika elimu. Katika shule za msingi za serikali, elimu ya masomo yote, isipokuwa somo la Kiingereza yanafundishwa katika lugha ya Kiswahili. Mwalimu Ndosi aliniambia sababu kubwa ni kuwa walimu wengi wa shule za msingi za serikali hawazungumzi Kiingereza kizuri. Katika shule za binafsi, lugha ya elimu ni Kiingereza. Kwa hivyo, watoto kutoka shule za serikali, wanapoanza elimu ya sekondari, wanapata shida sana. Inavyoonekana walimu wengi katika shule za sekondari wanajaribu kuwasaidia watoto ambao hawazungumzi Kiingereza kizuri. Lakini mambo hayawezi kuwa sawa kati ya watoto waliotoka shule za msingi za serikali na wale watoto waliotoka katika shule za binafsi. Ninafikiri hapa kuna hali ngumu kidogo na labda hali hii inaweza ikachochea utengano kati ya watoto hawa na baadaye kuzusha na hata kuongeza tabaka kat yao, yaani tabaka la walio juu na tabaka la walio chini.



Wanafunzi darasani

6. MRADI WA MWISHO **NATASHA APPENHEIMER**

Huu ni utafiti wangu kuhusu ugonjwa wa Ukimwi nchini Tanzania. Kabla ya kufika nchini Tanzania, nilidhani kuwa mashirika yasiyo ya kiserikali ni muhimu sana katika kupambana na

Ukimwi. Sasa, nimeamini kwamba kazi ya mashirika yasiyo ya kiserikali ni muhimu, lakini kazi ya vikundi vya jamii ni muhimu zaidi.

Nchini Tanzania, niliangalia mambo mbalimbali kuhusu ugonjwa wa Ukimwi. Jambo la kwanza niliangalia nini kazi ya mashirika yasiyo ya kiserikali nchini Tanzania. Niliona maonyesho katika televisheni, matangazo, na vibao vya barabarani vilivyoelezea Ukimwi. Tepe nyekundu zilizoashiria ugonjwa hatari wa Ukimwi zilionekana katika kila mahali. Niligundua kuwa hii ilikuwa kazi ya mashirika yasiyo ya kiserikali. Watu wanaona matangazo yanayohusu Ukimwi sehemu nyingi. Visiwani Zanzibar, tulitembelea shamba la mwani, na niliona tangazo kuhusu Ukimwi kijijini. Nilijua kwamba tangazo lilihusu Ukimwi kwa sababu niliona utepe wa Ukimwi. Pia, niliangalia matangazo yaliyozungumzia kondomu katika televisheni, vibao vya barabarani, ndani ya baa za pombe, na sehemu mbalimbali za barabara. Matangazo haya yanayohusu Ukimwi yanaonyesha kondomu kila siku, lakini sijui kama watu wanaangalia.

Niliangalia vitu vingine kuhusu Ukimwi nchini Tanzania. Niliangalia kazi ya serikali kuhusu Ukimwi. Chumba kimoja hospitalini kilihusu Ukimwi. Mwuguzi aliwafundisha waathirika kuhusu chakula kizuri kinachofaa. Aliwafundisha watu wengine kuhusu Ukimwi pia. Kuna matangazo mengi kuhusu Ukimwi na yalihusu idadi ya waathirika nchini Tanzania na duniani kote, njia za kujizuia kupata Ukimwi, na kadhalika. Pia, nje ya chumba cha Ukimwi, kuna kondomu zinazotolewa bure. Muuguzi alijaribu kuwapa watu kondomu katika chumba kile cha wagonjwa wa Ukimwi, lakini watu walizikataa. Walipoziweka kondomu nje ya chumba kile cha wagonjwa watu walianza kuchukua kondomu.

Walimu mashuleni wanafundisha kuhusu Ukimwi. Katika shule ya serikali tuliyotembela, niliangalia matangazo kuhusu ugonjwa wa Ukimwi katika vyumba vya wanafunzi wa darasa la nne hadi darasa la saba. Shule za binafsi na shule za serikali zinafundisha kuhusu Ukimwi. Wanafunzi wanajifunza kuhusu Ukimwi katika shule za msingi na katika shule za sekondari. Mwalimu wa shule moja ya serikali alinielea kwamba wanafunzi wanajifunza kuhusu Ukimwi kwa kipindi kimoja kila wiki. Nilizungumza na kijana mmoja, Meshu, kuhusu ugonjwa wa Ukimwi shuleni, na aliniambia kwamba alijifunza kuhusu Ukimwi alipokuwa akisoma shule ya msingi na hata katika shule ya sekondari. Alijifunza mambo rahisi kuhusu Ukimwi katika shule ya msingi, na alijifunza mambo mengi kuhusu Ukimwi katika shule ya sekondari. Katika shule ya sekondari, alijifunza jinsi Ukimwi unavyomwathiri mtu, na ni kwa njia gani mtu anaweza kujizuia kuambukizwa Ukimwi, kwa mfano kutumia kondomu ni jambo muhimu na linaloweza kusaidia.

Pia, magazeti mengi yana habari zinazohusu ugonjwa wa Ukimwi. Magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yanaandika habari za Ukimwi. Pia huandika hadithi zinazohusu serikali, jamii, waathirika, hospitali, na jinsi dunia inavyopambana na Ukimwi. Kwa mfano, nilisoma barua kutoka gazeti moja

iliyohusu ugonjwa wa Ukimwi. Barua ilitoka kwa msichana mmoja na ilikuwa anaishi na baba yake. Baba yake alimwambukiza mama yake, akaugua na kufa. Baba yake naye alikufa na msichana huyu alibaki kuwatunza wadogo zake. Dada huyu naye alikufa pia. Barua hii si ya kweli lakini ni mfano wa matatizo yanayozipata familia zilizoathirika na ugonjwa hatari wa Ukimwi.

Kwa muda wa wiki sita nilizokaa Tanzania sidhani kuwa kazi ya mashirika yasiyo ya kiserikali ni muhimu zaidi kuliko mashirika mengine. Sasa, ninaamini kwamba kazi ya jamii ni muhimu pia katika kupambana na matatizo. Kazi ya vikundi katika jamii ni muhimu kwa sababu ya mambo mengi. Kwanza, watu wanajifunza kuhusu Ukimwi kutoka kwa wakijiji walioathirika, vikundi vya vijana na watu wa makanisa nao wanasaidia kuelimisha wanakijiji, mashuleni, mahospitalini, au katika mashirika yasiyo ya kiserikali elimu kuhusu ukimwi inatiliwa mkazo. Ni muhimu kufundisha kuhusu Ukimwi katika sehemu wanazoishi jamii mbalimbali, na ni muhimu pia kuwashauri waathirika namna ya kujitunza na kuepusha kuwaambukiza wengine. Wanafunzi wanajifunza shuleni, na watu wazima wanahitaji kujifunza kuhusu Ukimwi sehemu yeyote walipo. Watu wanaokwenda kutembelea chumba cha Ukimwi mahospitalini wengi wao ni waathirika tayari, na jamii inahitaji kujifunza kutokana na matatizo wanayopata waathirika. Mashirika yasiyo ya kiserikali yanajitahidi sana, lakini bado kuna upungufu katika kutoa elimu ya jinsi ya kujizuia. Pia, vikundi vya jamii vinahitaji kujijengea misingi bora ya namna ya kuendesha kampeni kuhusu ukimwi, na mara nyingi wasitegemee sana fedha za kuomba kutoka kwa wafadhili kwani wafadhili nao hawana pesa za kutosha kuhudumia miradi yote.

Ni bahati na ni muhimu kwamba kuna vikundi vya jamii au watu wa jamii wanaowafundisha watu kuhusu ugonjwa hatari wa Ukimwi. Wazazi wengi nchini Tanzania wanazungumza na watoto wao kuhusu Ukimwi. Wanawaeleza kuhusu njia za kujizuia na ukimwi. Watu wa makanisa nao wanawaeleza waumini wao kuhusu tatizo la ugonjwa wa ukimwi. Wanawashauri kuwa ni bora kuwa na mpenzi mmoja, na endapo ukiwa na zaidi ya mpenzi mmoja, unahitaji kutumia kondomu. Pia kama umeoa au kuolewa unahitaji kufanya mapenzi na mke wako au mume wako tu. Endapo huwezi kujizuia basi ni bora utumie kondomu. Makanisa nayo yanajaribu kuwafundisha watu namna ya kujizuia, ingawaje wanapiga vita matumizi ya kondomu

Kuna watu ambao wanafanya kazi ya kuwahudumia waathirika wa ukimwi ambao wako nje ya makanisa. Kwa mfano, tulitembelea shamba la Mzee Mrema. Mama Mrema ana programu za kuwasaidia waathirika wa ugonjwa wa ukimwi. Katika shamba hili wanafuma vikapu, na Mama Mrema anaviuza vikapu na kuwapa waathirika faida inayopatikana. Mama Mrema ana programu hii kwa sababu anajaribu kuwasaidia waathirika wa ukimwi hasa wanapopoteza kazi zao. Ni vigumu kwa waathirika kupata kazi, hivyo mama Mrema amejitolea kuwasaidia waathirika kupata pesa za kuendesha maisha yao ikiwa ni pamoja na kujipatia dawa za kuongeza maisha.

Pia, kuna vikundi vya jamii ambavyo vinawafundisha watu kuhusu Ukimwi. Kwa mfano, tulitembelea kikundi cha vijana. Vijana wanawafundisha vijana wenzao kuhusu Ukimwi. Wanacheza mchezo wa mpira wa miguu kuwavutia vijana. Wakati wa mchezo huwafundisha vijana wenzao kuhusu mambo ya Ukimwi. Jambo hili ni zuri, kwa sababu vijana wanawasikiliza vijana wenzao kwa sababu wako katika rika moja na wanaelewana kuhusu mambo ya vijana.

Pia, kuna huduma kwa watoto baada ya wazazi wao kufa kwa Ukimwi. Kwa mfano, kuna nyumba za watoto yatima. Nilitembelea nyumba ya watoto yatima karibu na kituo cha Danish, Cradle of Love Baby Home. Walikuwa na watoto wachanga wawili ambao wazazi wao walikufa kwa Ukimwi. Kulikuwa na watoto wachanga watano, lakini wawili tu ni watoto yatima kwa sababu wazazi wao walikufa kutokana na ugonjwa wa Ukimwi. Mtoto mchanga mmoja si mwathirika. Hana Ukimwi, lakini mama yake alishakufa kwa sababu ya Ukimwi, hata dada yake pia. Kulikuwa na mtoto mchanga mwingine ambaye mkurugenzi wa nyumba ya watoto yatima anadhani kuwa ana Ukimwi, kwa sababu mtoto huyu ni mgonjwa mara nyingi. Mtoto huyu anakaa na familia moja, lakini mkurugenzi ana wasiwasi kuwa mtoto huyu atafariki. Nyumba za watoto yatima kama hii ni muhimu kwa sababu kuna watoto wengi ambao wazazi wao wameshaathirika na Ukimwi. Watoto wengi hawana Ukimwi, na wanahitaji familia, na mara nyingi, familia zao haziwezi au hazitaki kuwatunza watoto ambao wazazi wao wana Ukimwi. Watoto wengi watakufa bila kupata msaada kutoka nyumba za watoto yatima, au watakuwa watoto wa mitaani wanaoishi barabarani tu. Hii ni mbaya sana kwa jamii na kwa nchi kama Tanzania.

Ni matumaini yangu kwamba huduma kwa waathirika wa ugonjwa wa ukimwi zitaendelea, na elimu kwa jamii kuhusu ugonjwa huu hatari itaendelea pia. Huduma za serikali na kazi ya mashirika yasiyo ya kiserikali ni muhimu sana, na ingawaje hazitoshi ni budi zizidi kuhimizwa ili kuwasaidia walioathirika na ukimwi. Huduma za jamii zinaweza kuwafundisha watu kuhusu tatizo hili, na zisitegemee sana pesa za wafadhili. Huduma kama hizi zinahitaji kuendelezwa nchini Tanzania kutatua matatizo yanayosababishwa na Ukimwi.

7. Mashirika yasiyo ya kiserikali ya wanawake na WODSTA Shannon Montgomery

Tanzania ina mashirika yasiyo ya kiserikali mengi. Kuna mengi ambayo yanaweka fokasi kwa wanawake. Mashirika haya yanaweza kuweka msingi kwa hoja nyingi kama afya, UKIMWI, dini, siasa, mchango wa utafiti, shughuli au kazi, elimu, msaada wa kisheria, haki za binadamu, sayansi ya uzalishaji, matitizo ya wanawake na watoto wao, au maendeleo yo yote.

Nilitembelea shirika lisiyo la kiserikali la wanawake linaitwa WODSTA. Shirika hili lipo mji wa Arusha. WODSTA ni acronym ya Kiingereza ambayo inamaanisha Women Development for Science and Technology Association. Lengo la WODSTA ni kuzidisha hali ya wanawake. WODSTA imeshatimiza mafanikio mengi. Watu wa WODSTA wana madarasa kufundisha Wamaasai kusoma na kuandika. Kila mwaka kuna maonyesha ya bidhaa za wanawake. Watu mia tatu na zaidi walifundishwa kuhusu ustadi wa biashara. Pia, WODSTA inawasaidia wanawake kupata mkopo. WODSTA inafanya kazi katika sehemu tano. Inafanya kazi na jinsia na maendeleo, inawawezesha wanawake, inahizima hifadhi ya mazingira, inahizima matumizi ya teknolojia sanifu, na inafanya kazi na maendeleo endelevu.

Sasa WODSTA ina mipango mikuu minne. Kwanza ni programu na wanawake wa Wamaasai. Wafanyakazi wa WODSTA wanawasaidia wanawake kuwekaa na kutia nguvu mashirika ya wanawake. Wanawake wanafundishwa kusoma na kuandika. Na wafanyakazi wa WODSTA wanawasaidia wanawake kupata mkopo. Pia, wao wanafundisha jamii kuhusu usawa wa jinsia. Programu hii inawasaidia wanawake kuongeza mapato ya familia na kuboresha afya na lishe ya familia.

Programu nyingine ni kwa mkoa wa Arusha. WODSTA inafahamisha walimu, wanafunzi, na wafanyakazi wa serikali kuhusu matatizo ya wanawake na elimu. Pia, wafanyakazi wa WODSTA wanatoa ufundishaji kuhusu jinsia na UKIMWI katika shule na jamii. Wao wanatetea usawa wa jinsia na muhimu ya elimu na wavulana na wasichana.



Shannon anafundisha jigrafiaya Amerika

Programmu nyingine ipo mji wa Arusha. Wafanyakazi wa WODSTA wanafundisha wanawake kutumia bustani za vyombo na majiko ambayo yanatumia teknolojia sanifu. Kwanza, wanawake wanafundishwa kutumia chombo kupanda na kuota mimea, hasa mboga na viungo. Programu hii inasaidia kupunguza pesa ambazo zinatumiwa kwa chakula. Pia, wanawake wanafundishwa kutumia majiko ambayo yanatumia fueli ndogo zaidi. Nilipotembelea WODSTA, wafanyakazi walinionyesha majiko haya. Wao wana majiko ya jua, majiko ya bio-gas, na majiko ya vikapu. Majiko ya vikapu yananivutia sana. Wafanyakazi wa WODSTA wanaoitwa “wonder baskets”. Vikapu hivi vina unga wa mbao na vitu vingine na vifuniko. Nguo maalum zinawekwa ndani. Mwanamke anaweza kuweka chungu au vyungu vyenye vyakula moto ndani. Halafu, anaweza kukaa kikapu nyumbani kwao au kuchukua katika soko au mahali pengine. Mwanamke anapofanya kazi nyingine, chakula kinapikwa ndani ya kikapu. Baada ya masaa machache, chakula ni tayari. Vilevile, WODSTA inatengeneza gogo maalum. Gogo hizi zintengenezwa kwa unga wa mbao. Gogo moja linaweza kupika mlo mzima katika jiko la jiwe. Majiko yote haya yanawasaidia wanawake kudunduiza pesa na muda. Pia, programmu hii ni nzuri kwa mazingira kwa sababu wanawake wanaweza kutumia kuni ndogo zaidi.

Mwisho, WODSTA ina programmu kufundisha wanawake kuhusu kulinda na kutengenezwa chakula cha mkebe, hasa mboga na matunda. Pia WODSTA inawafundisha wanawake kuhusu kilimo

endelevu na ustadi wa kilimo. Programmu hii inawasaidia wanawake kuongoza mapato kwa sababu wanawake wanaweza kuuza vyakula hivi, hata kama vyakula hivi si msimu wake. Pia, matunda na mboga inaweza kula mwaka mzima na vyakula hivi havitakuwa potevu.

Mimi ninafikiri kwamba shirika hili na mashirika yasiyo ya kiserikali mengine yanawasaidia wanawake kuboresha maisha ya familia yao. WODSTA ni mfano mzuri kwa sababu wanawake wanaweza kuboresha maisha yao kwa kujifunza kuhusu sayansi na teknolojia. Kwa bahati nzuri, mashirika kama WODSTA yataendelea kupata kuchangia ili kuwasaidia wasichana na wanawake.

8. Utamaduni wa vijana katika Afrika Mashariki

Lynsey Farrell

Kabla ya kuja Tanzania, nilifikiri kuhusu tofauti kati ya vijana wa Tanzania na vijana wa Kenya. Niliishi nchi ya Kenya, nikaamua kuweka fokasi katika vijana wa mji wa Nairobi. Nina mawazo machache kuhusu njia za kusoma utamaduni wa vijana katika Afrika. Mara nyingi unaweza kuona utamaduni wa vijana katika miji. Niliweza kuelewa kwamba vijana wa Kenya walitumia njia nyingi kuonyesha mawazo yao na kufikiri kuhusu mabadaliko ya nchi yao. Vilevile, watu wengine walitumia njia hiyo, lakini ni vijana waanzao utamaduni huo. Inaonyeshwa katika muziki wa vijana kama “bongo flava” kwa Tanzania au muziki wa Ogopa DJs kwa Kenya. Pia, vijana wa Afrika Mashariki wanabadili lugha yao ili kutangaza tabia maalum. Wanasema “Sheng” au “Swanglish” badala ya Kiswahili au lugha za makabila yao. Hatimaye, utamaduni wa marekebisho au utamaduni wa vijana unaonyeshwa upande wa usafiri wa umma. Ningependa kueleza kuhusu utamaduni wa vijana na makusudi kuhusu sababu ambazo zinaonyesha usafiri wa umma ni muhimu ili kuelewa Afrika Mashariki.

Asili ya mawazo ya utafiti wangu ilitoka kushirikiana na jamii ya mashirika yasiyo ya kiserikali. Nilifanya kazi katika shirika la vijana ambalo lilikuwa likileta haki ya vijana na kufundisha vijana kuwa viongozi wazuri. Nilipofanya kazi pale Kenya, niliona kwamba watu wengi walifikiri kulikuwa na kundi maalum kama wanawake au vijana lililohitaji kupata huduma za kubadili maisha ya vijana au wanawake. Kenya inaendelea kuandika katiba mpya na watu wengi wanataka kuweka ibara maalum katika katiba kutetea wanawake, walemavu, na vijana. Walakini, kuna upinzani kutoka serikalini na wengine nchini ambao wanasema vijana si maalum na wanahitaji kufanya kazi ngumu kuboresha maisha yao. Hata sasa, mdahalo kuhusu vijana na serikali unaendelea.

Watu wengi wanafikiria aina ya vijana ni watu kati ya umri miaka kumi na nane na miaka thelethini na tano. Ni tofauti katika mahali pa Amerika tunaposema vijana ni watoto tu.

Hawagawanyiki kutoka jamii. Lakini, mdahalo wa vijana ni njia muhimu kuelewa utamaduni wa Kenya. Labda kuna tatizo sasa kwa sababu watu wengi hawaelewi kwa nini vijana wanapenda kupata haki wenyewe. Umri ni muhimu zaidi ya vijana. Uzee unahitaji heshima. Vitu vinabadilika. Ninafikiri ni muhimu kuelewa mwanzo wa mabadiliko hayo.

Ninajua kuhusu mji kuu wa Nairobi bora kuliko mingine. Pale, watu wengi wanafanya kazi katika sekta ya jua kali au wanafanya biashara ndogo ndogo. Watu wachache wanaweza kumaliza masomo katika shule ya sekondari kwa sababu ni ghali sana kulipia elimu. Kuna watu tajiri sana na watu maskini sana, lakini kuna watu wachache katika tabaka la kati. Mara nyingi, watu ambao wanafanya kazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali ni watu wa tabaka la kati. Sababu kubwa za kuelezea tofauti ni idadi ya watu. Shirika la U.N.D.P. lilisema kwamba miji katika nchi za Afrika Mashariki inaongeza kwa haraka kuliko sehemu nyingine duniani. Mji wa Dar es Salaam ni mji ambao utakuwa unaongezeka zaidi kuliko miji mingine. Idadi ya vijana katika nchi ya Kenya ni kubwa. Karibu na asimilia themanini ya idadi yote ni watu wenye umri chini ya miaka thelethini na tano.

Vijana wengi hawawezi kupata kazi au nafasi ya kumaliza masomo. Wanahamia mjini kutafuta kazi lakini hakuna kazi. Wanakaa vibanda vya ovyo ovyo. Hawana huduma za afya, elimu au ustawi. Kabla ya badiliko la serikali ya Kenya, vijana wengi walilalamika kuhusu maisha yao na watu wa mashirika yasiyo ya kiserikali waliamini waliweza kusaidia. Walakini, niliona kwamba ilikuwa ngumu kusaidia matatizo kama hayo. Mara nyingi, nilifikiri kwamba watu wa tabaka la kati, hawakuweza kuelewa matatizo ya vijana wengi. Halafu, sasa ninafikiri ni muhimu kuelewa utamaduni wa vijana wa mji. Wanapenda nini? Wanasikiliza muziki gani? Wanaonyeshaje mawazo yao?

Nchi ya Kenya na nchi ya Tanzania, zote zina usafiri wa umma wenye michoro na semi. Barabarani kwenda Dar es Salaam kutoka Arusha, unaweza kuona usafiri mwingi wenye michoro na semi. Michoro ilikuwa na rangi mbalimbali. Kabla ya marekebisho ya usafiri wa umma katika Kenya uliweza kuona basi za umma, zilizoitwa matatu, zilikuwa na michoro ya watu maarufu, wa timu za mpira wa miguu au chapa kutoka nchi nje Kenya. Pia, katika Tanzania, basi kubwa za umma zina michoro kama hayo. Labda michoro ni biashara tu. Inawezekana michoro inavutia watu kuingia. Walakini katika nchi nyingi duniani, usafiri wa umma haukuwa na michoro au semi. Ninafikiri mahali pa umma kama kituo cha basi ni pazuri kuelewa na kufahamu jamii. Sasa, kwa sababu kulikuwa na mabadaliko katika Kenya, ninajua watu wengi wafanyao utafiti katika Kenya kuhusu lugha na utamaduni wa vijana katika Afrika Mashariki. Wanaanza kuuliza maswali kuhusu utamaduni wa vijana. Wanauliza kuhusu sehemu ya umma kama kituo cha basi au magari wa umma ili waweze kuelewa kwa nini kizazi kipya kinaanza kubadili utamaduni wao. Wanakaa mjini na

wanaathiriwa kwa utandawazi. Wakati ujao ningependa kuendelea kuuliza maswali kuhusu lugha na utamaduni wa vijana. Tanzania na Kenya ni nchi tofauti lakini watu wa nchi zote waligawana utamaduni pachapacha.

9. MRADI WA MWISHO

Noelle Sullivan

Siku tulipoenda kujifunza kuhusu kikundi cha maendeleo, kikundi kimoja cha wanafunzi kilienda kuzungumza na kikundi cha vijana, na kingine kilienda kuzungumza na kikundi cha akina mama. Nilishiriki katika kikundi cha pili, ambacho kilizungumza na akina mama. Tulipofika, akina mama walituelezea kuhusu shughuli zao, na mwanafunzi mmoja aliwauliza waume wao wanafanya kazi gani. Mama mmoja alimjibu kwamba waume zao hukaa, hunywa pombe, na hawafanyi kazi yeyote. Nilishangaa kwa sababu akina mama hawa walifanya kazi ngumu ambazo zilichokesha sana. Jibu la mama yule lilinifanya kufikiri juu ya nyumbani kwetu jinsi ambavyo wanaume na wanawake wanafanya kazi sawa sawa. Pia niliwaza au labda nyumbani kuna kazi za wanawake tofauti na kazi za wanaume? Nilitaka kujua jinsi wanawake wanavyofikiri kuhusu jinsia na kazi. Lakini, nilipoanza kuzungumza na wanawake kuhusu maisha yao, niligundua kupata ukweli kuhusu jinsia hapa mjini Arusha ni kitu kugumu, na sikuweza kufahamu kuhusu jinsia ilivyo hapa mpaka nitakapopata muda zaidi wa kufanya utafiti zaidi. Lakini, taarifa nilizopata ziliniridhisha.

Nilizungumza na wanawake watano waliokuwa wamemaliza elimu ya msingi tu. Wanawake hawa walikuwa na miaka kuanzia ishirini na sita hadi thelathini na nane. Wote walifanya kazi mbali na nyumbani kwao, na kazi walizofanya nyumbani zilitofautiana. Nilifikiri kwamba utoto wa kila mwanamke ungeathiri mawazo yao kuhusu jinsia na kazi wanazofanya, lakini niligundua kuwa mambo yalikuwa tofauti. Nilikuwa nimefikiri kwamba wanawake hawa waliokomaa na kufikia kuwa wazazi wa familia wangewafundisha watoto wao kufanya kazi zinzohusisha jinsia zao, lakini wanawake hawa walikuwa na mawazo tofauti kwa kuafiki kuwa, kila mtu anatakiwa kufanya kazi sawa bila kujali jinsia. Nilikuwa nimefikiri pia kwamba wanawake waliokuwa na elimu zaidi ya kiwango cha shule ya msingi wangukuwa na mawazo kuwa wavulana na wasichana wanatakiwa kufanya kazi bila kujali jinsia. Pia, nilikuwa nimefikiri kwamba wanawake hawakuwa maskini wa mawazo kuhusu jinsia na kazi. Kwa hivyo, nilitafuta wanawake wanaofanya kazi nje ya nyumba zao kuzungumza nao kuhusu jinsia.

Lakini, mawazo yangu kuhusu jinsia mjini Arusha hayakuwa na ukweli wowote. Wanawake niliozungumza nao walinifahamisha kwamba suala la jinsia na kazi hapa Arusha ni jambo gumu. Wanawake watatu walikuwa maskini kidogo na walikuwa wamelazimika kutafuta kazi kutoa msaada kwa familia zao. Walikuwa hawana waume. Mwanamke mmoja alikuwa ameolewa, na alikuwa na

mtoto mmoja. Aliniambia kwamba mume wake ni mnywa pombe na alikuwa na wanawake mbalimbali, na pia hakufanya kazi yeyote nyumbani, hivyo ilibidi kuachana. Sasa, anafanya kazi na anamlipa pesa mama yake kumtunzia mtoto wake. Mwanamke huyu alikubali kuachana na mume wake licha ya watu kumteta kuhusu kuachika kwake. Watu walimwambia ni vibaya sana mwanamke mwenye mtoto kuachika. Yeye alikuwa mkali na aliwaambia kwamba ni bora kuachwa kuliko kukaa na mwanamumw mlevi. Aliniambia kwamba atamfundisha mtoto wake kwamba ni jambo jema kila mtu afanye kazi nyumbani kwa usawa bila kujali jinsia. Alifikiri kwamba ni bora wanafamilia wafundishwe kufanya kazi zote sawa sawa, bila kujali jinsia, hivyo wavulana watapika na wasichana watalima shambani. Mwanamke huyu alikuwa haogopi kuzungumza na wanaume kuhusu mawazo yake.

Mwanamke mwingine alikuwa ametoka familia ambayo mama na baba waliwapiga watoto. Wasichana walifanya kazi zote za nyumbani, na walikuwa na elimu ya msingi tu. Sasa, ana biashara binafsi na anaendesha biashara hii peke yake. Yeye ana duka la kuuza bia. Watu wa eneo hili wanazungumza juu ya mwanamke huyu kwa kuwa wanafikiri kwamba yeye ni malaya. Lakini, yeye aliniambia kwamba hajui kwa nini watu wanafikiri kuwa yeye ni malaya wakati anajaribu kufanya biashara kama watu wengine. Aliniambia ana mpenzi mmoja tu, na hahitaji wanaume wengine. Alisema kwamba akiwa na mtoto, atamfundisha kwamba ni bora wasichana na wavulana wafanye kazi za nyumbani kwa usawa, na pia ni vizuri wanawake kuwa na biashara binafsi inapobidi.

Mfano wa tatu ni mwanamke anayefanya kazi na ana mume. Mume wake anafanya kazi pia, na wao wana pesa za kutosha kulipa ada za shule za binafsi. Alikuwa na elimu ya msingi tu. Mume wake anafikiri ana familia ya kisasa kwa kuwa watoto wake wanajua kiingereza na kiswahili (hawajui lugha ya kwanza za wazazi wao). Mwanamke huyu havai nguo za desturi kama kanga, kitenge, au nguo za batiki. Mara kwa mara, mume wake hayupo, na yeye anawapa watoto kazi za nyumbani. Lakini, wavulana wanafanya kazi tofauti na za wasichana. Wasichana wanapika na kusafisha nyumba, wavulana wanalima, wanatunza mifugo, na mara kwa mara wanapiga nguo pasi. Mume wake anapofika nyumbani, anawapa wavulana kazi ya kupika kwa sababu anafikiri ni vizuri vijana nao wajue kupika. Lakini, wakati mume yupo, mwanamke alisema anaridhika sana. Anamhudumia mume wake, na kukaa kimya. Nilishangaa kuona hayo, kwa sababu mwanamke huyu na mume wake walifikiri familia yao ilikuwa familia “ya kisasa,” ingawaje kazi na vitendo vya wana familia vilibadilika baba alipofika nyumbani. Wakati baba yupo kila mtu alifanya kazi tofauti isivyo kawaida: wavulana wanapika, na wasichana walikaa kimya.



Wanafunzi wanaigiza mchezo juu ya maeudeleo ya wanawake

Kwa kweli ni vigumu sana kufahamu kuhusu jinsia hapa mjini Arusha. Nilifikiri kwamba kazi za wanawake ukilinganisha na wanaume zingetegemea elimu au utoto wa mtu. Lakini nimegundua si jambo rahisi kuelewa kuhusu mambo ya jinsia katika mji huu. Ninajua kwamba mambo ya jinsia yanabadilika sasa, ingawa mabadiliko yanatokea polepole. Ninajua pia kwamba nchini Marekani au Canada kuna matatizo ya jinsia sawa sawa kama hapa mjini Arusha. Kwa kawaida wanawake ndio wanaofanya kazi za nyumbani, wanaume wanafanya kazi nje ya nyumbani. Lakini, kama Marekani au Canada, hapa Arusha wanawake wengi wanafanya kazi nje ya nyumbani, lakini wanawajibika kufanya kazi za nyumbani pia. Katika utafiti wangu, niliona wanawake hawakuwa na elimu kubwa, lakini wana mawazo mengi mazuri kuhusu mambo ya kijinsia. Sijui kama ni elimu, au utoto, au pesa ndizo zinazoathiri mawazo ya kijinsia ya wanawake, au ni kitu gani. Ninafikiri ni vigumu kuelewa, na ningependa kufanya utafiti mwingine kuhusu jambo hili, kwa sababu wakati mambo yanapobadilika, ni vizuri kufahamu kwa nini, na ni kwa njia gani mabadiliko yamejitokeza. Nilijifunza kwamba hali ya kijinsia inategemea mambo mengi, na labda mambo hayo yamejificha. Ningependa kuyafahamu zaidi.

**10. CHUO KIKUU CHA INDIANA UNIVERSITY
WATU WA MAHITAJI MAALUMU
Eugenia D. Williams**

Uchunguzi wa mradi wangu ni kuhusu programu za kuwasaidia watu wenye upungufu wa mahitaji muhimu katika nchi ya Tanzania na nchi ya Marekani.

Nchini Marekani kila jimbo lina programu mbalimbali za kuwasaidia watu wenye upungufu wa mahitaji muhimu. Programu moja hufanya kazi ya kuwashughulikia wenye upungufu kimwili na programu nyingine hufanya kazi ya kushughulikia wenye upungufu wa akili. Programu hizi kufanya kazi katika vikundi vinavyoshirikiana pamoja.

Kwa mfano; katika jimbo la Indiana kuna baraza la gavana, linaloitwa Governor's Council for People with Disabilities (GPCPD). Baraza hili lilianza kufanya kazi kuwasaidia wenye upungufu uliojitokeza miongoni mwa wanajimbo. Majimbo mengi yana programu kama hii, na programu hii ni kubwa na inatoa msaada kwa kiasi wakuu wa majimbo wanavyotaka. Pia kuna programu nyingine kama hii ambayo inatoa ridhaa nzuri, kuwasaidia watu wenye upungufu kujenga nguvu za asili za mwili.

Pia baraza la mkuu wa jimbo lilikuwa na programu nyingine iliyofanya kazi kuwasaidia wageni kubadilisha uraia na kujiunga na umma wa wana Indiana. Baraza hili liliwatia moyo watu na kuwaonyesha njia namna ya kupanda daraja kujiunga wa wenyeji kulijenga jimbo la Indiana. Baraza hili liliwatia moyo wageni wote kujisikia huru na kutoa mchango wao wa kulijenga jimbo la Indiana. Hali hii ya kushirikishwa wageni iliwatia wenyeji wengi moyo na kuwaona wageni kama ndugu zao, na hata kuanza kujitolea kuwasaidia katika mambo yaliyohusu maisha yao.

Nia kubwa ilikuwa kutengeneza mpango bora wa kuwasaidia wageni hasa walemavu ili waweze kushiriki maendeleo katika jimbo ikiwa ni pamoja na mambo ya elimu, tathmini ya mipango ya mazingira bora, na kuwasaidia wale wote waliokuwa na ulemavu wa aina yeyote. Mipango hii ilishirikisha pia uchunguzi makini wa kuona ni jinsi gani walemavu wanaweza kusaidiwa ili nao watoe mchango wao kwa ujenzi wa jimbo la Indiana.

Nchini Tanzania msaada kwa walemavu unatoka kwenye vikundi visivyo vya kiserikali (NGO). Vikundi hivi vinasaidia kujenga miundo mbinu ya kuwasaidia na kuwatia moyo walemavu waweze kujitegemea. Vikundi hivi vimechukua jukumu kubwa na vinajitahidi kuwafikia walemavu popote walipo. Mashirika mengi yamejiunga na yanasaidia walemavu kwa hali na mali. Vikundi hivi

vimekubali kubeba majukumu mazito , hivyo vinahitaji msaada mkubwa ili viweze kuwasaidia walemavu wengi zaidi.

11. MRADI WA MWISHO

MBUGA ZA WANYAMA NA UTALII

Rebecca Skiba

Katika mradi wangu, nitazungumzia vitu vizuri, matatizo, maswali, na labda majibu mintarafu mbuga za wanyama. Vilevile, nitabainisha matokeo ya utalii na mazingira yake. Mbuga za wanyama zinahifadhi miti, wanyama, na maliasili ya aina tofauti. Miti ya aina tofauti ina dawa za kusaidia magonjwa. Wanasayansi na watu wengine wanaosoma mwenendo wa wanyama wanajifunza kuhusu shuguli za wanyama. Pia, wanasayansi wanajifunza kuhusu wanyama udugu na mazingira wao. Mifumo ya ikolojia mbalimbali ni mizuri kwa afya ya mazingira katika dunia na inaleta usawa duniani pia. Mbuga za wanyama zinaelimisha watu kuhusu mazingira na umuhimu wa kuhifadhi wanyama na miti mingi. Mbuga za wanyama zinawapa watu furaha na kuboresha nchi na raslimali zake. Watu wanajifunza kuhusu mifumo ya ikolojia inayovunjika upesi na matatizo yaliyoletwa na utalii.

Biashara ya utalii ni sehemu muhimu sana katika uchumi. Watalii wanaitembelea Tanzania kuona raslimali zilizopo, na biashara hii ya utalii inaleta pesa nyingi. Kwa sababu utalii ni muhimu kwa uchumi, watu wengi hubadilisha maisha yao kwa kutumia biashara ya utalii. Kwa mfano, watu walijifunza Kiingereza badala ya Kiswahili ili waweze kuzungumza na wageni na pia kuwauza vitu vingi kama maji, vitu vya makumbusho, na hata vitu vinavyotengeneza takataka. Vitu hivi vinatokana na maendeleo na utandawazi. Maendeleo na utandawazi ni mazuri, lakini yanaleta matatizo pia. Kwa mfano tuangalie Kreta ya NgoroNgoro ambapo kuna hoteli nzuri ya kitalii. Wageni wanakuja na wanakaa hotelini baada ya safari ndefu. Hoteli hii iko karibu sana na mbuga za wanyama zinazotumia vyanzo vya asili kupata maji. Je, maji machafu kutoka hotelini yanakwenda wapi? Tatizo hili ni sawasawa na matatizo ya utupaji wa takataka.

Mbuga za wanyama zinaunganisha mambo yote kwa pamoja. Maendeleo yoyote karibu na mbuga za wanyama yanaanza kwa matatizo makubwa yanayohusu uharibifu wa mazingira. Mfano mmoja kuhusu matokeo ya maendeleo karibu na mbuga za wanyama ni Ziwa Manyara. Katika Ziwa Manyara, ndege walikufa kutokana na maji machafu. Wanasayansi waligundua dalili ndogo za kemikali ya sumu. Walifikiri ndege wengi walikufa kwa sababu ya kemikali katika maji ingawa si kawaida, lakini hawajajua kwa uhakika tatizo lilikuwa nini. Wanasayansi wanatafiti na kuchunguza

zaidi hivi sasa. Watu hawaendi karibu na mbuga za wanyama bila kuharibu mazingira na maisha ya wanyama waishio katika mbuga hizi.

Jibu la matatizo kama ugonjwa uliotokea Ziwa Manyara linaunganisha mbuga za wanyama pamoja. Sasa hivi mbuga za wanyama katika Afrika ziko pembeni ya nyingine na zinadumisha njia ya wanyama wenye tabia ya kuhamahama. Mbuga zinategemeza wanyama wanaotoka sehemu tofauti katika bara la Afrika ambao wanahama kutafuta maji, chakula, na kujamiana. Vilevile, wanyama wanaweza kuondoka sehemu moja kwenda nyingine wakijisikia vibaya au wakihitaji vianzo vya asili kwa ajili ya maji safina malisho. Kwa sababu mbuga za wanyama ziko karibu na mbuga nyingine, ni lazima serikali itunze afya ya wanyama na miti ya asili.



Wanafunzi wanajiandaa kutembelea jamii

Watu wanaoishi NgoroNgoro Kreta, yaani Wamaasai, wanatunza mifugo na wanahamama kutafuta vyanzo vya asili kama maji na majani ya malisho. Wamaasai walikuwa watu wazuri waliohifadhi mazingira katika mbuga za wanyama kwa sababu walikuwa ni watu wa mashambani tu. Sasa, Wamaasai wanaolima mazao ya vyakula wanapata matatizo kwa kuwa wanyama aina mbalimbali hasa mifugo inakula mazao yao na kuleta mmomonyoko wa ardhi, uharibifu wa maliasili, pia barabara. Wamaasai wanaokaa katika mahali pamoja huhama na kutafuta sehemu ya kulima mazao

zaidi. Serikali imeanza kuondoa mashamba ya Wamaasai katika mbuga za wanyama kwa sababu hiiuharibifu unaojitokeza

Hivi sasa viongozi wametoa kanuni za kutumia katika mbuga za wanyama. Kwa mfano watu hawawakaribii wanyama, hawapigi kelele na kuwakasarisha wanyama na wageni pia. Hakuna kukata miti ovyo kuacha takataka, kuendesha magari katikati majani kwa sababu ni hatari kwa wanyama wadogo na miti michanga, na ni lazima kuendesha magari polepole kulinda wanyama. Vilevile, viongozi wanawatia moyo wageni kutembelea sehemu nyingine zenye mbuga za utalii kwa sababu watu wengi katika sehemu moja inachangia kuharibu mazingira. Takataka na maendeleo ya haraka yanatishia mazingira na uhai wa wanyama. Watu wanahitaji kuelewa matatizo haya, lakini ni muhimu kuwa makini pia. Kuelimisha watu jinsi ya kutumia maliasili na kuheshimu mazingira ni jambo zuri duniani. Kupunguza utalii na kuhifadhi mazingira ya wanyama na kuhifadhi miti kutasaidia kuhifadhi mbuga za wanyama. Tunahitaji kufanya kazi pamoja kufikiri namna ya kutatua matatizo yanayozikabili mbuga za wanyama.

2004 GPA Student List

1. Eugenia Williams
4302 Millersville Rd.
Indianapolis, IN 4660205-2544
2. Joanna Taque
255 Willow Avenue
Wayne, PA 19087
3. Kristen Leefers
731 Burcham, Apt. E101
East Lansing, MI 48823
4. Noelle Colquhou Sullivan
510 NW 15th Ave.
Gainesville, FL 3601
5. Sarah Smiley
3394 Pimlico Parkway
Lexington, KY 40517
6. Anna Lewandowski
1227 Spaight St.
Madison, WI 53703
7. Rebecca Roeder
428 S. Clemens
Lansing, MI 48912
8. Natasha Appenheimer
508 Hamilton Street
Washington, IL 61571
9. Erin Ensley
11771 Montecito
Los Alamitos, CA 90720
10. Lynsey Farrell
6 Islington St.
Allston, MA 02134
11. Rebecca Skiba
1124 Stone Mill Run
Lawrenceville, GA 30045
12. Shannon Montgomery
1810 NW 23rd Blvd. Apt 10
Gainesville, Florida 32605
13. John Lynsley
169 Perkins Row
Topsfield, MA 01983
14. Charles Elfer
183 Woodstone Dr.
Athens, GA 30605